Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 7 Februari, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika *(Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):**

Mapitio ya Utekelezaji wa Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania Katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2011/2012 *(The Mid – Year Review of the Monetary Policy Statement of the Bank of Tanzania for the Year 2011/2012).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 68

**Kupunguza Msongamano Katika Hospitali ya Mkoa – Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kuna ongezeko kubwa la watu katika Manispaa ya Dodoma kutokana na ujenzi wa Vyuo Vikuu; na Hospitali ya Mkoa inayowahudumia wakazi hao haijaongezewa Madaktari Bingwa na Manesi ili kukidhi ongezeko hilo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kuongeza Madaktari Bingwa na Manesi katika Hospitali hiyo ya Mkoa?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ili kupunguza msongamano katika Hospitali hiyo ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister A. Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa lipo ongezeko kubwa la watu katika Mkoa wa Dodoma. Hali hii inasababisha kuongezeka kwa wagonjwa wanaopokelewa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na hivyo kusababisha msongamano.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya wauguzi katika ikama ya Hospitali ya Dodoma ni 546 na waliopo ni 208. Hospitali imejiwekea mkakati wa kuajiri wauguzi kila mwaka kadiri bajeti inavyoruhusu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 waliajiriwa wauguzi 11 kati ya 16 walioombewa kibali. Wauguzi wataendelea kuajiriwa kadiri watakavyopatikana kila mwaka kulingana na uwezo wa kifedha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Madaktari Bingwa Wazalendo ni wanne na wageni kutoka China ni sita. Madaktari wa kawaida wazalendo saba ambao wako masomoni wakisomea ubingwa wa fani mbalimbali. Madaktari hao wakimaliza masomo, hospitali itakuwa imeongeza idadi ya Madaktari Bingwa. Hivyo, Serikali itaendelea kuajiri Madaktari Bingwa na Wauguzi kadiri watakavyopatikana kila mwaka kulingana na uwezo wa kifedha wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mkoa, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imeshapata kiwanja cha ekari nane, eneo la Ilazo, kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kwa hivi sasa ameshapatikana Mzabuni na kuandaa *Site Plan.* Kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Halmashauri ya Manispaa imeomba shilingi bilioni 2.5, maombi maalum kutoka Hazina ili kuanza ujenzi wa hospitali hiyo. Hata hivyo, upo mkakati mwingine ambao unaendelea kupunguza msongamano kwa sasa wakati utaratibu wa kujenga hospitali hiyo ukiendelea. Mbinu hizo ni pamoja hizi zifuatazo:-

Kwanza, Halmashauri inaangalia uwezekano wa kuingia makubaliano na Hospitali ya St. Gema ili iweze kuwa Hospitali Teule.

Pili, Vituo vya Afya vya Polisi na Magereza hapa Dodoma Mjini vimefunguliwa.

Tatu, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi imepata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bahi.

Nne, Kituo cha Afya cha Hombolo kinatoa huduma za upasuaji wa dharura kwa maana ya akina mama wajawazito.

Tano, Ujenzi wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma utakapokamilika, utasaidia kupunguza wagonjwa kwenda Hospitali ya Mkoa wa Dodoma.

Sita, uwepo wa Hospitali nyingine za Mashirika ya Dini yasiyo ya Kiserikali kama vile *Dodoma Christian Medical Center (DCMC)* na Kijiji cha Matumaini, unasaidia kupokea baadhi ya wagonjwa.

Mwisho, katika Hospitali ya Mkoa linajengwa jengo la magonjwa ya akina mama wajawazito ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia vitanda 180. Jengo hilo likikamilika litapunguza msongamano kwa upande wa wajazito.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo Madaktari hawa wazalendo wanne tu na Wachina sita wanafanya kazi katika hali ngumu kutokana na wingi wa watu katika Mkoa wa Dodoma. Pamoja na hayo hakuna vifaa tiba wala dawa. Bajeti ya Hospitali ya Mkoa haijaongezeka tangu ongezeko la watu liongezeke Dodoma:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vifaa tiba na dawa katika Hospitali ya Mkoa ili kukidhi angalau nusu ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma?

(b) Mwaka 2009/2010 katika Bajeti ya mwaka huo tuliomba shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa wodi ya wanawake katika Hospitali ya Mkoa. Kwa sasa wanawake wanalala wawili mpaka watatu katika wodi ya wazazi. Tangu tuombe hizo fedha hatujapata hata shilingi moja kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa wodi ya wazazi. Je, Serikali ipo tayari kwa mwaka huu kwa bajeti hii inayoendelea; *review* bajeti itakapofanyika tupate hizo shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya kukamilisha wodi ya wazazi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo anayazungumzia Mheshimiwa Felister Bura hapa ni ya msingi kabisa na sisi sote tunajua kwa sababu hata sisi wenyewe ni wahusika katika jambo hili linalozungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Tunakuja hapa na familia zetu, tunakuja na waume zetu na wake zetu, tuna familia na wale wanaotusaidia. Hatuna haja ya kufanya *debate* kubwa hapa kusema kwamba,

kuna msongamano ambao unatokea pale; hili ni jambo la kweli, *UDOM* imeongezeka, barabara zetu sasa hivi zinapitika, inayotoka Mwanza mpaka hapa.

Kinachofanyika hapa sasa hivi kwa maana ya *policy* ni kwamba, sasa hivi *MSD* yenyewe tumeihamishia katika Kanda kuhakikisha dawa hizi zinapatikana. Kuna kitu tunachokiita *integrated logistic system* ambacho kinakwenda kuangalia aina zote zinazopatikana pale ili kuweza kuwa na madawa na dawa zinazokwenda pale ziwe zinalingana na hali halisi inayojitokeza pale. Kama alivyo-*address* hapa ni kweli kabisa kwamba, kuna tatizo la dawa na vifaa na haya mengine yote anayoyazungumza. Tutawasiliana na *RAS,* tutawasiliana pia na Mganga Mkuu ili tuli-*address* hili tatizo twende tukalione vizuri, tuweze kujua kiasi kinachohitajika. Kwa hiyo, *there is no problem;* hili tutakwenda kulifanya.

Sasa kuhusu shilingi bilioni 1.5 anayoizungumzia hapa ni muhimu kwa maana ya sura hii inayozungumzwa hapa, lakini tatizo nenda Kilimanjaro, nenda Mwanza au kokote kule, tatizo hili lipo hivyo hivyo kama tunavyozungumza hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuchika, alijibu hapa kwamba, tunalo hilo tatizo, tutakachofanya tutashirikiana na Mheshimiwa Felister Bura, kufuatilia wote kwa pamoja Hazina kuweza kujua kiasi hiki ambacho kimeombwa cha shilingi bilioni 1.5 kiweze kupatikana ili kuweza kukidhi hili tatizo ambalo analizungumzia Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa mlundikano uliopo katika Hospitali Kuu ya Manispaa ya Dodoma unalingana kabisa na mlundikano uliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa; na kwa kuwa tayari kuna Hospitali ya Wilaya imeshajengwa katika Kata ya Mwangata; je, ni kwa nini mpaka sasa hivi yale majengo hayafunguliwi ili kupunguza ule mlundikano uliopo katika Hospitali ya Mkoa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri, kama unaijua hiyo Hospitali ya Mwangata jibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita kabla ya kuja hapa, tumefanya ziara katika Mkoa wa Iringa. Nataka nikiri, tumekuja kwako kule Njombe na safari hii ilikatishwa katikati kwa sababu ya matukio mengine yaliyojitokeza pale. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, mimi nitakwenda, kwa sababu nitakwenda kumalizia kiporo cha ile safari. Nikitoka hapa nakwenda Kilolo, ndipo anapotoka Mheshimiwa Mbunge, nitakwenda pia Iringa Mjini Manispaa, kuangalia hali halisi ya hii hospitali ili tuweze kujua na kama mambo yote yameshafanyika na hela imepelekwa pale na kazi imekamilika ni kwa nini huduma isitoke kwa ajili ya Wananchi ili waweze kupata huduma hizo. Kwa hiyo, awe na amani, mimi namhakikishia kwamba nikienda pale nakwenda kumaliza safari hii ninayokwenda, tutahakikisha kwamba tunakwenda kuliona hili. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ongezeko la watu ni la kila Makao Makuu ya Mkoa ukiwemo Mkoa wa Singida; na kwa kuwa Mkoa wa Singida umeikarabati Hospitali ya Mkoa vizuri sana na madaktari wanajitahidi sana kufanya kazi lakini haina Daktari Bingwa hata mmoja na Madaktari wa Kawaida ni wachache mno ukizingatia ajali nazo ni nyingi na watu ni wengi. Je, Serikali itakuwa tayari kuitazama Hospitali hii ya Mkoa wa Singida kwa jicho la huruma kuhakikisha tunapata Daktari Bingwa hata mmoja na kutuongezea madaktari wengine wa kawaida ili kazi hiyo nzuri iweze kufanywa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, toa majibu ingawa hayo aswali inatakiwa uwe unayajua *by heart* hayahusiani na *original* swali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Kwanza, hili la hospitali tunataka tuwaambie Wabunge kwamba, kama tunataka kuona hospitali ya kisasa nzuri iliyojengwa vizuri ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, twendeni pale Singida

tukaone kazi iliyofanyika; ni kazi nzuri sisi tumekwenda kama Wizara kwa kweli tumeridhika na kazi ambayo inafanyika pale. Kwa hiyo, tunawapongeza sana wenzetu wa Singida kwa kazi nzuri waliyofanya.

Sasa kuhusu hili la madaktari; hapa unapouliza habari ya Madaktari Mheshimiwa Diana Chilolo, ukumbuke pia kwamba, yupo mtu anayehusika na utumishi yuko hapa sijui ametoka amekwenda wapi, alikuwepo hapa. Sasa sisi na Wizara ya Afya tutashirikiana na yeye, kwa sababu ni suala la vibali, hapa tunazo barua zinazokataa lakini eneo hili limeruhusiwa Serikali imesema kwamba lipo wazi.

Tunachosema hapa ni kwamba, Waziri wa Afya kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), tunampeleka daktari moja kwa moja kule, hakuna tena kupita TAMISEMI halafu ndiyo achukuliwe apelekwe kule na nini. Tutakwenda kuangalia hali halisi anayoizungumzia Mheshimiwa Chilolo ili tuweze kuona jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia kama ni ku-*reallocate* au kufanya lolote lile lakini tuweze kusaidia suala hii.

Na. 69

**Migogoro ya Ardhi Katika Vijiji vya Mwandiga na Kalalangabo**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Mipaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma - Ujiji katika Vijiji vya Mwandiga na Kalalangabo imekuwa na migogoro; matumizi ya ardhi ya Kijiji cha Mwandiga eneo la njia panda imekuwa kero kiasi cha kupelekea Mheshimiwa Rais kutangaza kufutwa kwa viwanja vilivyogawiwa bila utaratibu wa kisheria katika eneo hilo:-

(a) Je, ni lini Wizara, Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma - Ujiji zitakaa na kupata ufumbuzi wa kudumu wa mipaka hiyo?

(b) Je, ni hatua gani imechukuliwa mpaka sasa kutatua mgogoro wa ardhi ya Kijiji cha Mwandiga katika eneo la njia panda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli imeonekana kwamba kuna mgogoro wa mpaka kati ya Halamshauri ya Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma - Ujiji. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kupitia Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma imeagizwa na kuahidi kulipeleka suala hili kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa *Regional Consultative Committee (RCC)* kitakachofanyika mwezi Machi, 2012 ili kulipatia ufumbuzi suala hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Mwandiga eneo la Njiapanda, mgogoro uliopo katika eneo hili unahusu madai katika eneo lililogawiwa viwanja. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imekwishalipa jumla ya shilingi 4,845,788 kwa ajili ya fidia kwa Wananchi 14 kwenye maeneo ya soko na makaburi.

Fidia katika maeneo mengine yenye viwanja, zoezi la kuthamini mali limekamilika na taarifa yake itapelekwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuthibitisha. Fidia italipwa kwa Wananchi ambao viwanja vyao vimetwaliwa baada ya uthamini uliofanywa kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, tatizo la mgogoro wa ardhi Njiapanda ya Mwandiga linahusiana/linahusika na kutokufuatwa kwa utaratibu wa ugawaji wa ardhi. Serikali ya Kijiji, Kamati ya Ardhi ya Kijiji cha Mwandiga na hata wenye mashamba katika eneo lile, hawakuhusishwa kabisa, waliona tu watu wanavamia maeneo yao wanaweka *beacons* na kuchukua ile ardhi. Kwa hiyo, tatizo siyo uthamini na kulipa fidia, tatizo taratibu hazikufuatwa na katika ziara ambayo Mheshimiwa Rais aliifanya Kigoma mwezi Juni mwaka 2010, alimwagiza aliyekuwa Waziri wa Ardhi wakati huo, Mheshimiwa Capt. Chiligati, aende Kigoma kwa ajili ya kuangalia taratibu za kufuatwa kuondoa eneo lile na kulifuta ili Wananchi waweze kugawiwa upya maeneo yale. Napenda kufahamu ni lini Serikali itachukua hatua kwa

ardhi ya Kijiji cha Mwandiga ambayo imegawiwa bila kufuata utaratibu na ni lini Serikali itatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kufuta viwanja vile na kuanza upya ili Wananchi wa Mwandiga waweze kupata stahiki ya ardhi yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza hapa natokea Tanga; suala hili nimeanza ku-*deal* nalo kuanzia kule Sanya Juu halafu nikaenda Tanga pia. Eneo la Mwandiga linalozungumzwa hapa mimi ndipo nilipokuwa nanunua migebuka nalifahamu na eneo lile la mpakani kule Mto Mngoni, rafiki yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe anajua kabisa kwamba, hili eneo nalifahamu; yaani hapa sipati tabu kuelewa anazungumza kitu gani; hicho ndiyo nataka kukisema hapa na niliwaambia kabisa tunapokwenda pale nataka mnithibitishie mniambie ni kitu gani kinachozungumzwa. Kwenye hili nitamwomba Mheshimiwa Zitto Kabwe naye anisaidie kuhusu kauli ya Rais inayozungumzwa hapa; nimejaribu ku-*squeeze* kwa ngumu zangu zote na hivi tunavyozungumza hapa *DED* Kweka aliyeko Kigoma anajua kitu tunachokizungumza hapa. Nataka kujua kama ni kweli Rais alilizungumzia eneo hili analilosema Mheshimiwa Mbunge.

Hili nalielekeza kwa Mheshimiwa Mbunge, anisaidie kwa sababu taarifa nilizopata mimi kutoka Kigoma Ujiji zinasema eneo ambalo Mheshimiwa Rais alilizungumzia ni kuhusu viwanja vya Kibirizi, Masangwe, Nabangwe, kutokana na maeneo hayo kuwa milimani. Watu walikuwa wamepimiwa viwanja pale Mheshimiwa Rais akasema, hatuwezi kuendelea kwa sababu kuna mmomonyoko wa ardhi, udongo unakwenda moja kwa moja Ziwa Tanganyika. Sasa anachozungumza hapa anazungumza habari ya Mwandiga; Mwandiga ukitoka *reline* unakwenda Gungu, ukitoka Gungu unakwenda Kahampwa, Kahampwa unakwenda mpaka Mwandiga. Sina tatizo, nataka tu anisaidie, ukinisaidia ukaniambia na Mwandiga nayo ipo sehemu hiyo iliyozungumzwa na Mheshimiwa Rais; kwa maana hii mimi nataka nikushibitishie nitashirikiana na Mbunge nimsaidie nikihakikisha kwamba jambo hili haliendelei kwa sababu Rais atakuwa ameweka kauli yake pale na sisi hatuwezi kuipinga kauli ya Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli unajua majina yote hayo. Mheshimiwa Zitto umekubali?

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la mipaka la Kigoma linafanana kabisa na matatizo ambayo yapo katika Kata za Jimbo la Ukonga hasa katika Kata ya Chanika, Nzasa na Wilaya ya Kisarawe kupitia Mlima wa Kazimzumbwi na Kata ya Kitunda eneo la Kipela na Wilaya ya Temeke; na kwa kuwa matatizo haya ni ya muda mrefu na nimeshazungumza sana na kuyaandikia barua; je, Waziri sasa atawaambia nini Wananchi wa maeneo hayo kuhusu suala hilo ambalo ni sugu?

**SPIKA:** Hapa Rais hakuahidi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizi ni *details,* ninamwomba Mheshimiwa Mbunge anipe nafasi, nitawasiliana na Mkurugenzi Mtendaji ili tuweze kujua tatizo liko wapi halafu tutashirikiana kuweza kutatua tatizo hilo analolisema.

Na. 70

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Mtoni**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI** aliuliza:-

Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kumalizia ujenzi wa barabara sehemu ya Mtoni – Amani:-

(a) Je, Serikali itaanza lini ujenzi huo ili kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo utasimamiwa na nani kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la swali la Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mtoni – Amani, yenye njia mbili kila upande (*Dual Carriageway*), ulifadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Mfuko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi ya awamu ya kwanza ilikamilika na ilihusisha ujenzi wa upande mmoja wa barabara hiyo, ambayo ilifunguliwa na Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mwaka 2004. Katika ujenzi wa barabara hiyo, Mfuko wa Rais, ulichangia shilingi milioni 204 kati ya shilingi milioni 600 zilizotumika kugharamia ujenzi huo na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha ujenzi wa Mradi huo sehemu ya pili ya barabara hiyo, SMZ katika mwaka 2010 ilileta maombi na mchanganuo wa gharama za kukamilisha ujenzi wa sehemu ya pili. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zilihitajika. Kufuatia ombi hilo, Wizara ya Ujenzi iliwasilisha maombi hayo kwa Katibu Mkuu (HAZINA). Mnamo tarehe 5 Oktoba 2010, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia barua yake yenye Kumbukumbu Na. *MOCT/M.60/C.9/VOL.V/62* iliiarifu Wizara ya Ujenzi kuwa imepokea shilingi bilioni 1.6 kutoka Mfuko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara husika itaendelea na ujenzi wa Barabara ya Mtoni – Amani.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika**,** ahsante. Pamoja na kuwa Mheshimiwa Waziri amelieleza suala hili kwa njia ya ufasaha na ya kitaalamu, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Serikali tayari imeanzisha mchakato huo wa kuitengeneza barabara hiyo; je Serikali inaweza kukiri kwamba kuchelewa kutengenezwa kwa barabara hiyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa hatusomi.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika, kumesababisha barabara hiyo kuwa hatari kwa waendao kwa miguu na magari?

(ii) Kwa kuwa utengenezaji wa barabara hiyo ulikuwa umeanza muda mrefu na ikawa inatumika sivyo kwa kupitia njia moja kwenda na kurudi na sasa njia hiyo tayari imeharibika umeanza mchakato wa njia ya pili. Je, barabara hizo kwa sasa zitakwenda sambamba baina ya njia ya kwanza na njia ya pili kutokana na hatari iliyokuwepo ikitengenezwa barabara ile nyingine na ya pili tayari itakuwa imeharibika? Ningeomba nipate jibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa barabara hizo ziko wapi?

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika, zipo Mtoni Zanzibar.

**SPIKA**: Zanzibar, kiutekelezaji huyu siye anayetakiwa kujibu hili swali, lakini kwa sababu anashirikiana ajibu tu.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika, samahani hii ilikuwa ni ahadi.

**SPIKA:** Ahadi wamesema wametoa fedha.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika, ahadi ilikuwa Serikali ya Muungano, aliyotoa Mheshimiwa Mkapa.

**SPIKA:** Haya naomba ukae, ninaposema mimi wewe unakaa, kwa sababu ya ushirikiano tu lakini ahadi ilitolewa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia Shomari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, umenisaidia sana. Wizara ya Ujenzi ya Tanzania Bara haihusiki na barabara zilizoko Zanzibar, *coordination* iliyofanyika hapa ni kuhakikisha zile shilingi bilioni 1.6 zimepelekwa Zanzibar, ambazo zilitolewa kutoka kwenye Mfuko wa Rais. Nimeeleza hapa kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshakiri kwamba, imeshapokea shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kutengenezea Barabara ya Mtoni - Amani. Kwa hiyo, wenye jukumu la kuitengeneza hiyo Barabara ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Ujenzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, ningeshauri Wizara inayohusika kule Zanzibar, ikaishughulikie hiyo Barabara kwa sababu zimeshapelekwa shilingi bilioni 1.6 kutoka kwenye Mfuko wa Rais.

**SPIKA**: Ahsante. Kwa kuwa hilo swali lenyewe halipo lingine linalofanana, kwa hiyo, naendelea na swali linalofuata.

Na. 71

**Ujenzi wa Barabara ya Isuna - Manyoni**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kampuni ya *CGC* ya China ilishakamilisha ujenzi wa Barabara ya Isuna – Manyoni:-

(a) Je, ni lini majengo ya Mhandisi Mkazi yaliyopo katika Kitongoji cha Iwelewele yatakabidhiwa rasmi kwa Halmshauri ya Wilaya ya Manyoni?

(b) Je, ni lini *quarry* iliyopo upande mwingine wa barabara hii itakabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, majengo ya iliyokuwa Kambi ya Mhandisi Mshauri yaliyopo katika Kitongoji cha Iwelewele yatakabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni baada ya Wizara kupata mapendekezo kutoka Uongozi wa Mkoa wa Singida kuhusu matumizi yatayokusudiwa kwa majengo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini iliumilikisha Mgodi wa Mawe (*Quarry*) wa Iwelewele kwa Wizara ya Ujenzi kisheria na unalipiwa ada ya leseni kila mwaka. Mgodi huu utaendelea kumilikiwa na Wizara ili uendelee kuwa chanzo cha kokoto kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja katika eneo hilo la Mkoa wa Singida. Hivyo basi, kwa kuwa bado tunauhitaji Mgodi huo kwa matumizi ya matengenezo ya Barabara za Mkoa wa Singida, hatuwezi kuukabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Aidha, mitambo ya kusaga mawe (*crusher*) iliyopo kwenye mgodi huo ni mali ya Mkandarasi.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna barabara zinazojengwa ndani ya Wilaya ya Manyoni kama vile Itigi mpaka Rungwa na hasa kile kipande cha kutoka Itigi kwenda mpaka Itagata na nyingine kutoka Kalangali kwenda Kirumbu; na kwa kuwa Makandarasi wamekuwa wakijenga kwa kiwango cha chini sana kwa kutumia udongo na changarawe; na kwa kuwa hapo jirani tuna Mgodi mzuri tu huo wa Iwelewele: Je, Wizara inaweza kuwaruhusu Makandarasi hao kuweza kutumia Mgodi huo kwa ajili ya kuimarisha barabara hizo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema Mgodi huo wa Mawe, yaani *quarry* ulioko Iwelewele unamilikiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD* Mkoa wa Singida, ambao wanalipia hati zote kwa mujibu wa Sheria za Madini. Kwa hiyo, wale Makandarasi waliopewa kutengeneza hizo barabara ambazo amezitaja sasa, sifahamu kama ni Barabara za Halmashauri au ni Barabara za Mkoa, kama ni Barabara za Mkoa wataendelea wanaweza kuchukua sehemu hizo.

Kama ni Barabara za Halmashauri ningependa tu nitoe wito kwa Mheshimiwa Lwanji kuwa, tujaribu kuzungumza na kuangalia utaratibu ni namna gani tunaweza kufanya ili Wananchi wanaotumia barabara hizo alizozitaja nao waweze kusaidiwa kupata *quarry* kwa ajili ya kutengeneza hizo kokoto. Kuhusu kutengeneza ubovu wa barabara zile, kwa sababu walipewa kwa mujibu wa sheria, inawezekana likawa tatizo la Makandarasi wale na hivyo kama Mheshimiwa Lwanji ataniruhusu, naweza kuituma Bodi ya Makandarasi kupitia Sheria Na. 17 ya Mwaka 1997, ikaanze kuwachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuwafukuza.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Waziri aliyejibu swali sasa hivi ana *record* nzuri ya kuweka msukumo katika Miradi ya Barabara. Je, atakuwa tayari kuja Tunduru baada tu ya Bunge hili aone kasi ya utengenezaji wa barabara ya kutoka Tunduru hadi Namtumbo ili aongeze kasi kutokana na kasi isiyoridhisha inayofanywa na Mkandarasi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mtutura kwamba, barabara ya kutoka Tunduru kupitia maeneo yote yakiwepo Daraja la Rumesule, kupitia Peramiho hadi Mbinga, maeneo yote yale kwa sasa hivi yanashughulikiwa na Makandarasi. Kutoka Tunduru kuna Makandarasi watatu ambao wanashughulikia Mradi huo wa Barabara kwa kiwango cha lami na kuna Makandarasi wawili wanaendelea na kazi nzuri sana. Mkandarasi mmoja alikuwa anakwenda pole pole na hivi karibuni tumemtuma *Chief Executive* wa *TANROADS* kwenda kumsimamia vizuri ili na yeye ajiandae vizuri. Barabara ya kutoka sehemu ya Tunduru kuelekea kule Masasi nayo *African Development Bank* wameji-*commit* kwa ajili ya kuanza kuitengeneza kwa kiwango cha lami.

Ninamthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakwenda Tunduru lakini pia hata Mheshimiwa Rais, kutokana na ratiba yake amekubali kwenda maeneo hayo ya Ruvuma kwa ajili ya kuweka Mawe ya Msingi ya Miradi hiyo ya Barabara inayoshughulikiwa katika maeneo hayo.

Na. 72

**Kusitishwa kwa Kilimo cha Pamba - Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Serikali ilisitisha kilimo cha pamba Wilayani Chunya kwa sababu ya kuwepo kwa funza mwekundu ambaye alihofiwa kuenea nchi nzima:-

(a) Je, utafiti wa kumwangamiza funza huyo umefikia wapi?

(b) Je, Wananchi walioathirika kwa kukosa zao la biashara wamehamasishwaje kulima zao mbadala?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa SPika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kilimo cha pamba kimesitishwa katika Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Rukwa na Mbeya, ikiwemo Wilaya ya Chunya, kwa sababu ya kuwepo funza mwekundu. Funza huyo

alionekana kwa mara ya kwanza nchini mwaka 1925, Wilayani Songea, kwenye pamba pori (*wild cotton*). Mdudu huyu alikuja nchini kutokea Nchi ya Msumbiji na husababisha hasara kubwa katika zao la pamba katika Nchi za Malawi, Msumbiji, Zimbabwe, Zambia, Swaziland na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kusini yaliwekewa karantini tangu mwaka 1946 kama kinga kwa ajili ya kuzuia mdudu huyu kusambaa hadi katika maeneo ya uzalishaji pamba ya Kanda ya Mashariki (*ECGA)* na ya Magharibi *(WCGA)*. Mwaka 1999 watafiti walimwona funza mwekundu Wilayani Chunya katika Vijiji vya Kanga, Galula, Magamba, Wanzani na Chang'ombe. Kwa sababu ya kuhofia kuenea zaidi kwa mdudu huyo, Serikali ilisitisha kilimo cha pamba Mkoni Mbeya *(Cotton Quarantine Area, Order, 2000 G.N. No. 36/2000 R6P.136)*.

Utafiti wa funza mwekundu ulishirikisha wadau wote wa Halmashauri za Wilaya husika za Mikoa ya Kusini ikiwemo Wilaya ya Chunya. Aidha, utafiti huu ulidhihirisha kuwepo kwa funza mwekundu kwenye maeneo yaliyowekewa karantini tangu mwaka 1946. Pia ilionekana kuwa funza mwekundu ana uwezo wa kusambaa kwa kasi kubwa na kwamba ameshasambaa hadi Mpanda katika Mkoa wa Rukwa ambapo hakuwepo awali. Kwa sababu hiyo, Mpanda na Mkoa mzima wa Rukwa nao uliingizwa katika karantini.

Mheshimiwa Spika, mazao mbadala ambayo Serikali katika Mikoa husika inayahamasisha ni ufuta ambao ni zao linaloongoza kulimwa mabondeni Wilayani Chunya, likifuatiwa na alizeti pamoja na mpunga. Kwa ujumla, wakulima wamehamasika kwa kiwango kikubwa kulima mazao mbadala. Mazao mengine ni mahindi, nyanya na pilipili. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na Mheshimiwa Mbunge, kuwaelimisha wakulima fursa zilizopo za kulima mazao mbadala na kuyasindika.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa baada ya kusitisha kilimo cha pamba kuna Vijiji katika Kata za Galula, Kanga, Mbuyuni, Namkukwe, Kambi, Katoto na Ifumbo ambao Vyama vya Msingi vilikuwa vinakidai Chama Kikuu cha Ushirika cha Pamba fedha zao na Serikali imechukua deni hilo na kuahidi kwamba italipa, lakini mpaka leo haijalipa. Je, ni lini Serikali itawalipa wakulima wa pamba ili waendelee na shughuli zao zingine?

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni kubwa sana, sehemu moja walikuwa wanalima pamba imesitishwa, sehemu nyingine wanalima tumbaku, mwaka uliopita wa kilimo Mamlaka ya Tumbaku nadhani kwa idhini ya Wizara, wamesitisha asilimia tano ambayo Halmashauri zilikuwa zinakata kwenye makamapuni ya tumbaku ili kuleta maendeleo kwa Wananchi wanakata tatu, asilimia mbili zitarudishwa kwa wakulima. Nadhani kwa idhini ya Wizara ya Kilimo, mpaka leo asilimia mbili hiyo haijarudishwa kwa wakulima na hatujui inafanya nini. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa taarifa nilizonazo na *records* zangu ni kwamba, Serikali ilichukua madeni yote ya Vyama vya Ushirika na Serikali ilikwishalipa madeni hayo. Sasa labda tu nimshauri Mheshimiwa Mwambalaswa, kama kuna chama ambacho mpaka leo hii kina hakika kabisa kwamba hakikulipwa na kina sababu za msingi, basi tuwasiliane; lakini mimi ninavyojua Serikali ilikwishalipa madeni yote hayo na Vyama vya Ushirika vyote vilikwishalipwa. Wale wadai wote walikwisharidhika, naomba Mheshimiwa Mwambalaswa, labda alilete upya, lakini pia tuwe na ushahidi kwamba kweli hawa wanaodai ni madeni halali, maana ipo tabia pia ya madeni mengine ya nyuma kuibuka.

Kuhusu suala la asilimia mbili ya tumbaku, naomba niseme kwamba, hili tumelitambua, tunalifahamu na hivi jana tulikuwa tunafikiria tutalifanyaje hili katika mazingira ya sasa hivi maana yake linahusisha pia sheria ambayo tuliipitisha wenyewe hapa kuhusu asilimia tatu mpaka tano ya ushuru wa tumbaku. Kwa hiyo, naomba anivumilie kidogo, Wizara ya Kilimo tutaendelea kuwasiliana na TAMISEMI, kwa sababu suala hili linagusa wakulima pia linagusa Halmshauri za Wilaya ili tuweze kulipatia ufumbuzi

ambao ni mwafaka kwa upande wa Halmashauri. Wakulima ni Halmshauri, naomba atupe muda tuweze kufikiria namna ya kulipatia ufumbuzi.

**MHE. SAIDI AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa zao la pamba kule Mpanda limezuiliwa zaidi ya miaka 30 iliyopita; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba karantini imewekwa mwaka 1999; karantini ni jambo moja; je, ni hatua gani zimechukuliwa mpaka hivi sasa za kuweza kuwatokomeza hao funza wekundu ili Wananchi waweze kulima pamba katika maeneo yetu?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti katika pamba umefanyika kwa undani sana; namna ya kushughulikia wadudu na magonjwa ya zao hili, ambayo yanaongeza sana gharama za uzalishaji wa zao hili. Katika kufanya hivyo, moja ya mafanikio ambayo yamepatikana ni katika kuzalisha *BT Cotton* au pamba ambayo imebadilishwa vinasaba. Pamba hii ina upinzani mkubwa na hailiwi na mdudu huyo funza mwekundu.

Kwa hiyo, inatoa matumaini kwamba, tutakapokuwa tumebadilisha sasa Kanuni za Sheria yetu ya Mazingira, tutaweza kukuza pamba hiyo katika maeneo ya Chunya, Ruvuma na hata Mpanda na kuendeleza pamba hiyo katika eneo la Ziwa ambalo sasa tunalima pamba tunayolima sasa.

Faida ambazo zinaonekana kuletwa na pamba hii kwanza ni kuongeza nyuzi, nyuzi zake ziwe ndefu zaidi na thamani yake ni ya juu; inaongeza uzalishaji mara kumi, ina uwezo mkubwa wa kuvumilia ukame na faida hiyo ambayo nimeisema. Sheria zetu hazikubali tuanze kuitumia pamba hiyo na Wizara yangu inaandaa Waraka ambao utajadiliwa kwa mapana zaidi ili tuweze kuamua juu ya matumizi ya pamba hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Na. 73

**Uuzwaji wa Hoteli ya Moshi**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO)** aliuliza:-

Hoteli ya Moshi iliuzwa kwa mwekezaji kwa takriban miaka kumi na tano kwa malipo ya awali ya Tshs. 165,000,000 na mwaka 2004 mwekezaji huyo alifungua kesi Na. 147 akidai akabidhiwe hoteli hiyo lakini kabla ya kukabidhiwa mtu mwingine alipewa hoteli hiyo:-

(a) Je, ni utaratibu gani uliotumika kumpatia mtu wa pili hoteli hiyo?

(b) Licha ya hoteli hiyo kupewa mtu wa pili bado hoteli hiyo imefungwa na kuchakaa sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuifufua ili iweze kuanza tena kutoa huduma kama awali?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hoteli ya Moshi au kama ilivyojulikana Livingstone, ipo katikati ya Mji wa Moshi na ilikuwa inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Mnamo mwaka 1998, katika mpango wa kubinafsisha Mashirika ya Umma, Serikali iliiuza kwa Kampuni ya Wazalendo ya *Kibo Hotels Ltd* kwa kiasi cha shilingi 575,000,000 kupitia Mkataba wa Mauzo uliosainiwa tarehe 18 Septemba 1998, baina yake na Kampuni ya *Kibo Hotels Ltd.* Katika makubaliano hayo, ulikuwepo mpango wa uwekezaji ambao ni sehemu ya mkataba. Kwa ufupi katika makubaliano hayo, mwekezaji alitakiwa alipe fedha za mauzo kwa awamu nne na kufikia mwaka mmoja baada ya kusainiana mkataba wa mauzo awe amemaliza kulipa fedha yote; na pia alitakiwa kuifanyia ukarabati kufikia kiwango cha nyota tatu.

Kampuni ya *Kibo Hotels* ililipa kiasi cha shilingi 165,000,000 kama malipo ya awali na kukabidhiwa hoteli hiyo. Tangu mwaka huo, mnunuzi yaani *(Kibo Hotels),* hakutekeleza lolote; si kumalizia malipo yaliyokuwa na riba wala kufanya ukarabati uliokubaliwa kwa mujibu wa mkataba. Utaratibu wa kuirudisha hoteli mikononi mwa Serikali ulifanyika. Kupitia amri ya Mahakama ya mwaka 2004, Serikali iliichukua hoteli na kuiuza kwa Kampuni ya Kizalendo ya *Impala Hotels* ya Arusha tarehe 15 Machi, 2007 kwa masharti yale yale kama yalivyokuwa kwenye mkataba wa mwanzo wa *Kibo Hotels.*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Mwekezaji mpya, yaani *Impala Hotels,* baada ya kukamilisha maandalizi ya awali na kupata vibali vya ujenzi, alianza ukarabati. Wakati kazi hii inaendelea, Kampuni ya *Kibo Hotels* ilifungua kesi ya madai Mahakamani na kuzuia ukarabati usiendelee. Kutokana na mgogoro huo, ukarabati wa hoteli ulisimama. Kesi hiyo ilimalizika mwaka 2011, baada ya mlalamikaji, yaani *Kibo Hotels* kushindwa. Ni imani yangu kuwa, mgogoro huo umekwisha na *Kibo Hotels* ameridhika na ataheshimu uamuzi wa Mahakama.

Kazi ya ukarabati ilianza tena mwezi Novemba 2011, baada ya michoro kukamilika na kibali cha ujenzi kutoka Manispaa ya Mji wa Moshi kutolewa. Kandarasi ya ujenzi inafanywa na Kampuni ya SUMA JKT, ambao tayari wameshaanza upya kazi ya ukarabati. Mwekezaji anatarajia kukamilisha ukarabati mwishoni mwa mwaka 2012.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, mauzo ya hoteli hiyo kwa mwekezaji wa pili yalifuata Sheria na Kanuni za Mauzo?

(ii) Kama Sheria na Kanuni za Mauzo zilifuatwa; je, hoteli hiyo kwa mara ya pili iliuzwa kwa shilingi ngapi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mauzo kwa awamu ya pili ulifuatwa na *PSRC* na aliyeuziwa mara ya pili alikuwa ni *Impala Hotel* kama nilivyosema; na aliuziwa kama sehemu ya makubaliano ya kuondoa kesi ambayo ilikuwepo Mahakamani kuhusu iliyokuwa Hoteli ya *Seventy Seven* na makubaliano yalikuwa ni Dola za Kimarekani 462,291.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; mwekezaji wa kwanza wa *Kibo Hotels* alilipa milioni 165. Ningependa kujua ni lini sasa atarudishiwa fedha zake baada ya kushinda kesi hii?

**SPIKA:** Nadhani Waziri unayajua hayo? Majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwa kifupi sana kwamba, kwa mujibu wa makubaliano yaliyokuwepo kati yake na *PRSC*, utaratibu ulikuwa kwamba, akishindwa kwenye *investment plan,* ambayo walikuwa wamewekeana, basi mkataba huo utakuwa umevunjika na taratibu za kuvunja mkataba zitakuwa zimefuatwa. Kuhusu kurudishiwa fedha, ipo ndani ya mkataba kwamba ni nini ambacho kitafuata. Bahati mbaya sijauona mkataba wenyewe, lakini kifupi ni kwamba, walivunja kwa mujibu wa mkataba ambao walikuwa wamewekeana.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwa na tabia ya hawa wawekezaji wanaposhindwa kutimiza masharti hukimbilia Mahakamani na kesi hizi huchukua muda mrefu ambao unalipotezea Taifa na Wananchi pato. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wawekezaji hawa wababaishaji? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukabiliana na changamoto za wawekezaji wababaishaji au ambao hawafuati taratibu za mkataba; kwanza, kinachofanywa ni kuhakikisha kwamba, taratibu za mauzo kwa maana ya kutangaza na kupata watu wazuri wanaofaa zinafuatwa. Pili, imewekwa mikataba mizuri ambayo inahakikisha kwamba, pale ambapo linakuwa limetokea inakuwa ni rahisi kuvunja mkataba. Kwenda Mahakamani ni haki ya kila mtu na kwa maana hiyo, siyo rahisi kuweza kumzuia mtu kwenda Mahakamani. Kinga ya Serikali ni kuhakikisha mikataba inakuwa ni mizuri, ambayo haitoi nafasi kwa mtu kuvunja mkataba bila kufuata utaratibu.

**SPIKA:** Ahsante, tumewapa nafasi nyingi hapa kwa sababu maswali yao yalikuwa mafupi mafupi na kuwapo kwenye dakika tano zinazohusika. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Esther Midimu.

Na. 74

**Uharibifu wa Mazao Lukungu**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Askari wa Lukungu kuwa kituo kamili ili kiweze kupambana na wanyama toka Pori la Akiba Maswa na Hifadhi ya Serengeti wanaoharibu mazao?

(b) Je, ni lini Wananchi walioharibiwa mazao yao tangu Novemba 2010 watalipwa kifuta jasho ili kiwasaidie katika hali hii ya njaa?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, wa kati na mrefu wa kuhakikisha inakomesha tatizo la wanyama waharibifu katika ukanda huo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi, Serikali inakubaliana na wazo la kujenga Kituo cha Askari Lukungu. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha, Wizara haikutenga fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho. Wizara itaangalia uwezekano wa kutenga fedha kwenye bajeti zijazo ili kuweza kutekeleza Mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010, jumla ya Wananchi watatu kutoka Wilaya ya Bariadi waliwasilisha maombi ya fedha za kifuta jasho kutokana na uharibifu wa mashamba yao uliofanywa na wanyamapori. Wananchi hao ni Bwana Nkwaya Nkaviga kutoka Wilaya ya Shinyanga aliomba fidia ya Sh. 3,520,000; Bwana Thobias Masanja Ngitili kutoka Wilaya ya Bariadi aliomba fidia ya Sh. 62,129,600; na Bwana Emmanuel Mbiti kutoka Wilaya ya Bariadi aliomba fidia ya Sh. 47,820,000.

Mheshimiwa Spika, maombi yao yalikuwa na upungufu ikiwa ni pamoja na kutokufuata taratibu za kuomba fedha za kifuta jasho, ambayo huambatishwa na uthibitisho wa tathmini ya uharibifu ambao hufanywa na Afisa Kilimo wa Wilaya, Afisa Wanyamapori wa Wilaya na Afisa Mtendaji wa Kijiji. Baada ya tathmini kufanyika, maombi haya huwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ambaye humwandikia Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kuomba fedha hizo kulipwa kupitia Wilaya. Kutokana na upungufu huo, maombi hayo hayakuweza kushughulikiwa zaidi na walalamikaji walielekezwa kwa kuandikiwa barua ili waweze kufuata utaratibu huo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha thamani au uthamini unafanyika.

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa kati na wa muda mrefu wa Serikali wa kukabiliana na la wanyamapori waharibifu ni pamoja na hatua zifuatazo:-

(i) Wizara inaendelea kutumia Vituo vya Idara ya Wanyamapori kuendesha doria za msako wa wanyama kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zenye matatizo;

(ii) Kuendelea na utaratibu wa kutambua shoroba na mapito ya wanyama ili Wananchi wahamasishwe kuondoka maeneo hayo na kupunguza shughuli za kibinadamu ili wanyama waweze kupita bila kizuizi;

(iii) Kuendelea kulipa kifuta jasho au machozi pale ambapo matatizo yamekuwa yametokea;

(iv) Kuendelea kufanya utafiti wa kueneza matumizi ya mbinu mbadala ikiwa ni pamoja na pilipili na oili chafu kwenye maeneo ambayo uharibifu unatokea;

(v) Kutoa mafunzo kwa askari wa wanyamapori wa vijiji, yaani *Village Game Scouts* kushiriki katika doria za msako wa wanyamapori;

*(vi)* Kujenga vituo zaidi *(Game Post)* vya wanyamapori kulingana na uwezo wa kifedha; na

(vii) Kuhamasisha Wananchi kuanzisha Hifadhi za Jamii *(WMA)*.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Ndovu kuharibu mazao Wilaya ya Bariadi hususan Vijiji vya Lukungu na Matongo limekuwa sugu. Je, Serikali ina mpango gani kudhibiti tatizo hilo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la uharibifu wa mazao ya Wananchi kwa siku za karibuni limeongezeka sana. Mpango wa Serikali kama nilivyoeleza kwenye jibu langu sehemu ya (c) ni kwamba, tutaendelea kujenga vituo kwenye maeneo hayo. Vilevile tutaendelea kutoa elimu kwa Wananchi ili waweze kutoa nafasi kwenye maeneo ambayo wanyama hutawanyika na maeneo ya shoroba. Vilevile tutaendelea kutumia mbinu mbadala, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu ya kuweka pilipili pembezoni mwa mashamba pamoja na *oil* chafu ili kuzuia wanyama wasiweze kuharibu mazao ya Wananchi.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Pamoja na mikakati mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri amezungumzia, Jimbo langu la Mwibara robo tatu limezungukwa na maji ya Ziwa Victoria na wapo wanyama wengi sana ambao wanaitwa Viboko, wanaokula mazao ya Wananchi na kusababisha njaa Mwibara iwe ya kudumu:-

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba mikakati yote aliyoisema haiendani na kumdhibiti huyu mnyama aitwaye Kiboko atupe njia mbadala ya kuhakikisha kwamba hawa viboko wanashughulikiwa?

**SPIKA:** Haya, anajibu kwa sababu na yeye anajua hizo habari lakini ni swali lingine kabisa. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukabiliana na wanyama hasa Viboko hatua ambayo imekuwa ikichukuliwa mara nyingi ni kufanya sensa ya wanyama hawa na kuruhusu wavunwe ili kupunguza idadi yao. Kwa hiyo, kwa maeneo kama aliyoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na wenzetu walioko Kanda ya KBU Bunda ili kuweza kuchukua za namna hiyo.

**MHE. JITU V. SONI:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Ninaomba niiulize Serikali kutokana na kwamba hailipi fidia kamili katika mali au mazao yanayoharibiwa. Je, Serikali ina mpango gani kwa wale ambao wamefuata utaratibu; kwa mfano Wananchi ambao wanapakana na Tarangire, Kata ya Mkaiti, Galapo, Mamire na Endakiso, wamefuata utaratibu wote na mpaka leo hii bado fidia ya mazao yao haijalipwa na wanashindwa kununua hata mbegu ya kulimia mwaka huu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, suala lako litakuwa la jumla, kwa sababu siyo lililokusudiwa. Mheshimiwa Waziri, unaombwa majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Soni pamoja na Wabunge wengine ambao matatizo ya wanyama waharibifu yapo mara kwa mara kwenye maeneo yao kwamba; nia ya Serikali ni kuhakikisha tunalipa kifuta machozi na kifuta jasho mara tatizo linapokuwa limetokea na taarifa kufikishwa ofisini kwetu. Changamoto ambayo tumekuwa nayo ni utaratibu kutokufuatwa. Sheria hii imepitishwa mwaka 2009, Kanuni zake zimesainiwa mwaka 2011 (mwaka jana). Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa kabla ya hapo taratibu zilikuwa hazifuatwi vizuri.

Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa maeneo aliyoyazungumzia ya Galapo na mengine, utaratibu ulifuatwa na wenzangu wa Ofisini kuhakikisha kwamba tunalipa. Nimhakikishie tu

kwamba, kwa upande wa kwetu kama Wizara, pale ambapo taratibu zinakuwa zimefuatwa na madai kufikishwa kwa muda mwafaka, tutahakikisha kwamba tunalipa mara moja baada ya kuhakikisha kwamba taarifa zimetufikia.

Na. 75

**Kuweka Vyombo vya Uokoaji Baharini**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

Ajali nyingi za boti, mashua na majahazi zimekuwa zikitokea mara kwa mara baina ya Tanzania Bara na Visiwani na kupoteza maisha ya Watanzania wengi:-

Je, ni lini Serikali itaweka vyombo vya uokoaji baharini?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Vyombo vya Majini ya Mwaka 2003, chombo chochote kikiwa majini kina wajibu wa kukisaidia chombo kingine kilichopata ajali. Hivyo, ikitokea ajali kila chombo kilichopo karibu na tukio kina wajibu wa kutoa msaada. *SUMATRA* wanaratibu vyombo vyote vya Serikali na Taasisi zake kama vile Jeshi la Wananchi, Polisi, KMKM, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, *TRA, TEMESA,* Idara ya Uvuvi na kadhalika, ambavyo huwajibika kushiriki katika kazi ya utafutaji na uokoaji endapo vitaweza kufika au vikiwa karibu na tukio la ajali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha taratibu za vyombo vya uokoaji baharini katika eneo la Tanzania kwa kuwepo kwa Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Dar es Salaam, kinachoendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA),* kwa lengo la kupata taarifa za ajali mapema na kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji baharini. Pia mitandao ya simu iliyopo baharini na kwenye Maziwa hivi sasa inarahisisha taarifa kutoka eneo la ajali na kufika kwenye kituo cha utafutaji na uokoaji. Kituo hiki pia kina uwezo hata wa kuona meli za maharamia na kutoa taarifa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa Sheria ya Utafutaji na Uokoaji *(Search and Rescue Bill)* na pia Mpango wa Kitaifa wa Utafutaji na Uokoaji *(National Search and Rescue Plan).* Kupitia Sheria na mpango huo, taratibu na rasilimali zinazohitajika, upatikanaji na usimamizi wake, zitaainishwa kwa lengo la kuimarisha huduma ya utafutaji na uokoaji Baharini na kwenye Maziwa na huduma hiyo kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *SUMATRA* imekuwa ikiwahamasisha wamiliki wa vyombo vya usafiri wa majini kuzingatia Sheria na Kanuni za Usalama wa vyombo vyao. Serikali pia inatoa ushauri kwa wamiliki na waendeshaji wa maboti, mashua na majahazi, kutopendelea safari za usiku, kufuata taarifa za hali ya hewa na kuwa na vifaa vya mawasiliano kwenye vyombo vyao ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika, aidha, kuwasiliana haraka na vyombo kwa msaada wa kuokolewa haraka.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kuna ushirikiano upi kati ya *SUMATRA* na *Zanzibar Maritime Authority* wakati zinapotokea ajali katika Bahari au katika Maziwa?

(ii) Mheshimiwa Naibu Waziri katueleza kwamba kuna mpango wa kuunda hiyo *National Research and Rescue Plan* na mpango huu hauwezi kuwa wa Kitaifa kama Zanzibar haijashirikishwa. Je, Zanzibar imeshirikishwa vipi kupitia *Zanzibar Maritime Authority*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, tena kwa kifupi, muda umepita.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu suala la ushirikishwaji wa *SUMATRA* na *ZMA;* hizi Taasisi zimeundwa kwa Sheria mbili tofauti; *Zanzibar Maritime Authority* imeundwa na *Maritime Transport Act* ya 2006 na *SUMATRA* imeundwa kwa Sheria ya 2003. Hizi Taasisi mbili zinashirikiana kwa masuala ya ajali majini na pia zinabadilishana uzoefu mara kwa mara na pia Wizara mbili hizi; Mawasiliano na Miundombinu ya Zanzibar na Uchukuzi ya Bara, zinashiriki pia katika Mikutano mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *Search and Rescue Plan,* hii Sheria sasa hivi inaundwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya *ZMA* na *SUMATRA* na zile *input* zote zinashirikishwa pamoja. Mara Sheria hii itakapokuwa imeundwa, itafanyiwa utekelezaji wake Bara na Visiwani kwa kupitia hizi Taasisi mbili zilizoundwa kisheria; *SUMATRA* na *ZMA*.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mwaka 1996 wakati wa ajali ya *MV Bukoba* Serikali ilitamka kuunda Kikosi Maalum cha Uokoaji ambacho kitakuwa kinatoa huduma kwa haraka pale tatizo linapotokea kwenye vyombo vya majini; na kwa kuwa leo ni miaka 14 Serikali leo hapa inatuambia kwamba inaandaa *rescue plan:-*

Serikali haioni kwamba kuchukua mambo ya msingi kwa taratibu kiasi hiki kunasababisha maisha ya Watanzania kupotea kama ilivyotokea kwa *MV Spices* ambayo tumekwenda kuleta watu kutoka nje matokeo yake hatukuweza kuokoa kwa sababu wanatoka mbali na huduma inakuwa inachelewa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa vyombo vya uokoaji baharini na Sheria pamoja na taratibu zote zipo. Ni kweli mpango huu wa *National Rescue Plan* unaandaliwa sasa hivi lakini *SUMATRA* imeundwa mwaka 2003, *Zanzibar Maritime Act* imeundwa mwaka 2006 na huu ni utaratibu wa kuboresha hizi Sheria, lakini Serikali ipo imara katika kuhakikisha vyombo vya uokoaji na utafutaji vipo imara. Pia pale Mwanza, tuna taasisi ambayo inashughulikia masuala haya na kama linavyoeleza swali la msingi, tumeyashirikisha Makampuni ya Simu kwa ajili ya mitandao. Sasa hivi tunapata taarifa haraka na vyombo vya uokoaji vinakwenda haraka kwenye tukio baada ya taarifa hizi kupatikana.

Na. 76

**Uingiaji wa Wakimbizi Nchini**

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH** aliuliza:-

Kumekuwa na uingiaji nchini wa wakimbizi kutoka kwenye nchi tunazopakana nazo na baadhi ya wakimbizi hao wamezagaa kwenye pande nyingi za nchi yetu na kufanya vitendo viovu kwenye maeneo walimo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuwadhibiti wakimbizi hao na uharibifu wanaoufanya na kukabiliana na njia wanazopita kuingia nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni tumekuwa hatuna uingiaji nchini wa wakimbizi kutoka nchi tunazopakana nazo. Kwa maana hiyo, hatuna wakimbizi waliozagaa kwenye pande nyingi za nchi yetu kama asemavyo Mheshimiwa Mbunge. Kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi Namba 9 ya Mwaka 1998, upo utaratibu unaofuatwa na waomba hifadhi au wakimbizi wanaoingia nchini ili waweze kupata

hadhi ya ukimbizi. Kwa wale wanaopewa hadhi ya ukimbizi, kwa mujibu wa Sheria, hukaa au kuishi katika maeneo waliyotengewa (Makazi/Kambi za Wakimbizi).

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaothibitika kufanya vitendo vya uhalifu, tumekuwa tukiwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria, lakini pia kwa kushirikiana na *UNHCR*, Shirika ambalo linashughulikia masuala ya wakimbizi duniani.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa waingiaji haramu hawa tunaishi nao, tunakula nao na baadhi yao ni wafanyabiashara wakubwa katika nchi yetu. Je, Mheshimiwa Waziri anawaambiaje Watanzania kuhusu utafiti uliofanywa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la msingi anazungumzia juu ya wakimbizi, swali lake la nyongeza anazungumzia juu ya waingiaji haramu; hivi ni vitu viwili tofauti!

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hii ni changamoto kubwa tuliyonayo na inajulikana na ipo katika vyombo vya habari, lakini tunachukua jitihada ambazo tunaweza tukazichukua. Suala lenyewe ni kubwa ambalo linahusu hasa waingiaji haramu hawa hasa wanaotoka Somalia na wale ambao wanatoka Ethiopia; hayo ndiyo makundi makubwa ambayo tulikuwa nayo hususan kundi kubwa ni la wale ambao wanaingia kutoka Somalia.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua kadhaa; tumezungumza na Kenya, tumechukua hatua kadhaa kwa kuweza kujitengeneza sisi wenyewe kwa mujibu wa kufuatilia. Niseme kwamba, ni tatizo ambalo tumekuwa nalo lakini tutakabiliana nalo kwa *resources* ambazo tunazo na ninasema kwamba, ndivyo tunavyokwenda, tutaweza kushinda katika suala hili.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mkenda katika Jimbo la Peramiho, mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, kwa miaka mingi lilikuwa Makao ya Wakimbizi kutoka Msumbiji. Kwa bahati nzuri, baada ya Nchi ya Msumbiji kupata uhuru, eneo hilo sasa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Msumbiji, kumeshajengwa Daraja na kuwekwa mpaka kwa ajili ya kudhibiti wahamiaji haramu na hasa Wasomali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa eneo hilo la mpaka wa Tanzania na Msumbiji katika eneo hilo la Menda, litatangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali ili shughuli zote zinazotakiwa kufanywa katika mpaka huo zianze sasa kufanyika kihalali baada ya Tangazo hilo la Serikali kutamka hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli jinsi alivyoelezea historia ya suala hilo na kuhusu eneo la Ukinga ni kwamba, tupo katika utaratibu ambao baada ya kufungua lile daraja kama alivyosema, tupo katika utaratibu wa kuweka *one border post* ambayo itahusisha vyombo vyote ambavyo vipo nchini kwa mujibu wa makubaliano ambayo tumekuwa nayo na Serikali ya Msumbiji. Kuhusu upande wetu kuhusu uhalalishaji wa suala hili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni suala ambalo tupo tunalifanyia kazi na nimhakikishie itakapofika katikati ya mwaka, tutakapokuja katika kipindi cha Bajeti, nafikiri tutakuwa tumeziweka taratibu ambapo biashara halali ambayo anaisema tutakuwa tumeifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini hata kama tutaruhusu biashara halali, bado tuna tatizo la wakimbizi hawa ambao walikuja siku nyingi kwa sababu za ukimbizi, mambo yaliyokuwepo kati ya vita ya kugombea uhuru wao watu wa *FRELIMO.* Siyo tatizo kubwa kama maeneo mengine, lakini bado wapo watu wengi na hasa linajitokeza nyakati za kupiga kura, nyakati za uchaguzi, ambapo kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Wananchi wa maeneo hayo kusema kwamba, hapa kuna watu ambao ni wa nchi nyingine lakini bado kwa ukazi wao hapa, wamekuwa wakishiriki katika mambo ambayo hawatakiwi kushiriki. Kwa hiyo, suala ni kubwa kidogo lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunalifanyia kazi ili kuweza kuweka mambo sawa kisheria.

**SPIKA:** Haya, wanasema u-*gazette*. Tunaendelea, jamani ninyi huwa hamwangalii saa, suala lilikuwa ku-*gazette* hicho kitu. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, atuliza swali hilo.

Na. 77

**Ujenzi wa Maktaba ya Wilaya ya Kasulu**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Ujenzi wa Maktaba ya Wilaya ya Kasulu unaonekana kusuasua:-

(a) Je, tatizo ni nini?

(b) Je, ujenzi huo utakamilika lini ili wanafunzi na watu mbalimbali waweze kuitumia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Maktaba ya Wilaya ya Kasulu inajengwa kwa ubia kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA).* Hatua ya ujenzi huo mpaka sasa ni kukamilika kwa sehemu ya chini ya jengo hilo la ghorofa moja. Kusuasua kwa ujenzi wa Maktaba ya Wilaya ya Kasulu, kumetokana na uhaba wa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na ucheleweshwaji wa kupatikana kwa vifaa kutoka *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka huu wa Fedha (2011/2012), zitakazopatikana fedha za maendeleo, ujenzi huo utakamilika katika Maktaba hiyo. Juhudi zinafanyika kuwasiliana na *TANAPA* ili nao watoe vifaa vya ujenzi vilivyobakia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Sera ya Bodi ya Hudma za Maktaba Tanzania *(BOHUMATA)* ya kuanzisha Maktaba katika ngazi za Wilaya ni kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Wajibu wa Halmashauri ni kutoa jengo, samani na wahudumu. Wajibu wa Bodi ni kutoa mkutubi, vitabu na ushauri; hivyo, kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kutawezesha kuanzishwa kwa ushirikiano kati ya *BOHUMATA* na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na huduma za Maktaba katika Wilaya ya Kasulu, zitaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, kwa jitihada inazozifanya kuanzisha huduma za maktaba. Sambamba na hili, nachukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zote nchini zilizo katika hatua mbalimbali za kuanzisha maktaba katika Halmashauri za Wilaya zao.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Inaonekana Serikali haina uhakika kwamba fedha za maendeleo zitapatikana ili Maktaba ya Wilaya ya Kasulu iweze kukamilika; ndiyo maana kuna majibu kama fedha za maendeleo zitapatikana Maktaba hiyo itaweza kumalizika. Naomba Kauli ya Serikali je, fedha hizi zitapatikana au hazitapatikana;

na kama zitapatikana kwa mwaka huu wa 2011/2012 ni nini hatma ya kumalizika kwa Maktaba ya Wilaya ya Kasulu?

(ii) Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonekana kabisa kwamba juhudi zinafanywa kuweza kuwasiliana na *TANAPA*. Ninajiuliza swali; hizi juhudi zinazofanywa majibu haya hayana tofauti na yale majibu ya mchakato unafanywa au itakuwa hivi na hivi?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itupatie majibu ya uhakika; inagharimu muda kiasi gani na *resource* kiasi gani kuweza kufanya mawasiliano na *TANAPA* ambao wameonekana kuweza kusaidia kukamilika kwa ujenzi wa Maktaba ya Wilaya ya Kasulu ili Wananchi waweze kwenda ku-*access material* mbalimbali kwa ajili ya faida yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, leo nimeongea na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kasulu, amenihakikishia kwamba, katika bajeti yenu kule Halmashauri ya Kasulu na Mheshimiwa Mbunge wewe ni Mjumbe, sasa kama utakuwa hufahamu hili nitakushangaa; maana labda huingii kwenye vikao vile; mmepanga ninyi wenyewe shilingi milioni 25 kwamba ndiyo bajeti kwa ajili ya umaliziaji wa jengo hilo la Maktaba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la pili la *TANAPA* na Halmashauri kama nilivyosema, haya mambo ni ya Wana-Kasulu wenyewe; maktaba hiyo mnaijenga kwa ubia wa Halmashauri na *TANAPA* kadiri mlivyokubaliana kwenye vikao. Wewe Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa vikao hivyo, kwa hiyo, utakuwa unajua dhahiri mambo yanavyokwenda. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri tu kwamba, taarifa nyingi za maktaba hii zipo kwa Mkurugenzi na mimi amenithibitishia kabisa kwamba, atamalizia Maktaba baada ya mpango mzima mtakavyokubaliana. *(Makofi)*

Na. 78

**Mafunzo ya Uongozi na Ujasiriamali**

**MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. ZARINA S. MADABIDA)** aliuliza:-

Vijana wengi wanaomaliza masomo wanalazimika kujiajiri lakini hawana mafunzo ya uongozi na ujasiriamali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya mitaala ya shule na vyuo ili kuingiza masomo ya usimamizi wa biashara na ujasiriamali ili elimu hiyo iwasaidie katika shughuli za kujiajiri kwao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika shule za msingi, sekondari na vyuo, wanapata mafunzo ya ujasiriamali kupitia masomo mbalimbali wanayoyasoma katika ngazi zote hizo za elimu. Serikali kwa kutambua umuhimu wa somo la ujasiriamali, iliandaa Waraka wa Elimu Namba 2 wa Mwaka 2006. Waraka huu umeweka bayana masomo atakayosoma mwanafunzi wa shule ya msingi; yaani stadi za kazi na haiba na michezo na sekondari kuna *book-keeping, commerce, cookery, needle work* na *agricultural science*. Masomo hayo yana mada za elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara. Aidha, kutokana na Waraka huu, mitaala imeboreshwa ili kumuwezesha mhitimu aweze kupimwa ujuzi na maarifa *(Competence Based)*.

Mheshimiwa Spika, kuanzia darasa la kwanza hadi vyuo vikuu, wanafunzi wamekuwa wakifundishwa somo la stadi za kazi au ujasiriamali ngazi husika. Somo hili huwajengea uwezo wa kuweza kujitegemea kwa kujiajiri kutokana na ujuzi wanaoupata. Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)*, ina mkakati wa

kuendelea kuboresha mitaala na mihitasari ya masomo ili kuhakikisha kuwa elimu ya ujasiriamali inayoingizwa katika masomo yote ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu vinakamilika.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa masomo hayo ya stadi za kazi kwa shule za msingi na ujasiriamali kwa vyuo yanafundishwa kinadharia zaidi kuliko vitendo kutokana na ukosefu wa zana za kufundishia. Je, Serikali imejipangaje sasa kusaidia kupeleka zana za kufundishia na kujifunzia katika vyuo ili wapate elimu timilifu?

(b) Kwa kuwa miaka ya nyuma somo hilo halikuwa wazi katika mitaala; na kwa kuwa wanawake ni kundi muhimu sana duniani. Je, Serikali haioni haja sasa kusaidia wanawake waweze kupata somo la ujasiriamali kwa wale walio vijijini, mijini na walio makazini ili elimu hiyo iweze kuwasaidia katika kuendeleza maisha yao ya uzeeni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Mbunge anasema masomo haya elimu ya msingi, sekondari na vyuo, yanafundishwa kwa nadharia zaidi kuliko vitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, masomo haya huwa yanafundishwa darasani kwa nadharia kama silabasi inavyooneshwa, lakini vilevile wanafunzi hupata muda wa kwenda kujifunza kwa vitendo. Mfano, kwa shule za msingi wanakwenda kusuka, wanaweza wakasuka mikeka au wakafinyanga vyungu na kadhalika, lakini huwa masomo haya yanafundishwa kwa vitendo kutokana na maeneo husika. Kama nilivyosema, hata sisi wakati tulipokuwa tunasoma shule za msingi, kulikuwa na somo la sanaa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo dhana halisi ya neno stadi za kazi kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu wanawake kufundishwa somo la ujasiriamali kwenye elimu ya watu wazima, naomba nilichukue kama changamoto kwa Wizara ya Elimu, tutakwenda kulifanyia kazi.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni hivi majuzi tumesikia kutoka Wizara ya Elimu kwamba, wanafunzi wanaomaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika. Tumesikia kwamba, Serikali ina mpango wa kufanya mtihani wa kuwachuja wanafunzi hao wakiwa tayari wameshaanza kidato cha kwanza. Je, Serikali ina mkakati gani au inatoa tamko gani kwa wale wanafunzi ambao watabainika hawajui kusoma na kuandika ; itawafanyia nini wanafunzi hao ili waende sambamba na sayansi na teknolojia pamoja na kujiajiri wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili ni zuri sana na inaonekana wakati tukitangaza kwenye vyombo vya habari na kuweka nyaraka mbalimbali, basi labda haukutuelewa kwenye hili. Ni kweli kabisa, Serikali imesema wanafunzi wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza, watakaobainika hawajui kusoma na kuandika tutawarudisha.

Mheshimiwa Spika, hili ni kweli kabisa na ndivyo ilivyo na tukishawarudisha hatuna namna nyingine ya kuwasaidia kwenda kujiunga na mfumo mwingine usio rasmi kama *VETA* na sehemu zingine. Lakini tulisema vizuri sana wakati tukiendelea kutamka matamko haya na tumesema kwamba tarehe 28 Februari, zoezi hili litakuwa limeshafanyika kwenye shule zote za sekondari Tanzania nzima kwamba Wakuu wa Shule wawapime, labda hapa nataka kufafanua vizuri Waheshimiwa Wabunge siyo mtihani kama mtihani bali ni majaribio madogo ambayo shule nzima itahusika na walimu wote kuwapima wale wanafunzi tena ni kwa siku moja kuweza kujua zile *study* za KKK (kusoma, kuandika na kuhesabu).

Atakayetambulika na atakayegunduliwa kwamba yeye hajui kusoma na kuhesabu lazima arudishwe maana yake lazima kulikuwa na mfumo mwingine wa ufaulu mitihani kama alivyosema kwamba mwaka huu kulikuwa na udanganyifu mkubwa sana kwenye mitihani yetu.

**SPIKA:** Ahsante. *For the interest of time, there is no time*, Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum atauliza swali hilo. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad!

Na. 79

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Kijiji cha Nyashimbi na Puni – Shinyanga**

**MHE. AZZA H. HAMAD – (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM)** aliuliza:-

Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Nyashimbi na Puni, Shinyanga Mashariki wakati alipoongea na wananchi hao katika ziara ya kikazi na tayari maombi juu ya ahadi hiyo yalikwishawasilishwa ofisini kwake.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo:-

Serikali ina nia ya kuwapatia wananchi wote walio vijijini nishati ya umeme ambayo ni muhimu katika kuchochoea maendeleo yao, kwa maana ni kwa kusudi hili Wakala wa Nishati Vijijini ulianzishwa. Mipango ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Tanzania ipo, japokuwa haiwezi kutekelezwa kwa wakati mmoja kutokana na kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu hapa Bungeni swali namba 337 la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum tarehe 5 Agosti, 2011, kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati alipokuwa katika ziara ya kikazi kuelekea Wilaya ya Kahama. Serikali ilifanya tathmini kuanzia tarehe 14 Februari, 2011 kwa ajili ya kujua gharama za ujenzi wa njia ya kupeleka umeme katika Vijiji vya Nyashimbi na Puni, tathmini ambayo ilikamilika tarehe 2 Machi, 2011. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha kuwa kila kijiji kitahitaji kufungiwa *transfoma* moja ya ukubwa ya *KV* A 100, kujengewa njia ya usambazaji umeme ya msongo KV 0.4 yenye urefu wa kilomita mbili ikitokea Ibadakuli Shinyanga Mjini kuelekea Wilaya ya Kahama. Gharama za mradi katika kila kijiji ni shilingi milioni 69, 566,089.87.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* haikuweza kutenga fedha katika bajeti yake ya mwaka 2011 kutokana na uhaba wa fedha unaolikabili Shirika. Ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo, *TANESCO* imekwishapeleka maombi ya fedha za utekelezaji wa mradi kwa Wakala wa Nishati Vijijini *REA* na *REA* wameshaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Ahmed Ally Salum kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa miradi ya umeme Jimboni kwake kama ilivyojidhihirisha kwa barua yake aliyoniandika hivi karibuni tarehe 3 Februari, 2012 akifuatilia miradi ya umeme Jimboni kwake, ahsante.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili, kwa kuwa ahadi hii ni ya muda mrefu sasa toka mwaka 2007. Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Kijiji cha Puni na Nyashimbi katika bajeti ya mwaka 2012/2013, kuweza kuwatengea fedha kwa ajili ya kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa umeme kupeleka Bukombe, kupitia Kijiji cha Segese kilichopo Wilayani Kahama ambayo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais katika kampeni zake mwaka 2010? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kikalenda ahadi ya mwaka 2007 inaanza kuonekana kuwa ni ndefu, ni ya muda mrefu, lakini kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia

maombi ni mengi, mahitaji mengi ya maeneo ya vijiji na hata baadhi ya maeneo mjini bado hatujafikisha huduma hiyo kwa kiasi ambacho tungependa. Lakini juhudi kama tulivyosema zipo na ahadi yetu sisi ni kwamba kwenye bajeti ya fedha ya mwaka ujao mwaka 2012/2013, Vijiji vya Nyashimbi na Puni ni kati ya maeneo ambayo utekelezaji wake utazingatiwa na hivyo utakuwa umetengewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa kufikisha umeme Bukombe, maeneo ya Kahama na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mwanza, Shinyanga na Arusha, mradi ambao unajulikana kama *electric five* ambao fedha za ufadhili kwenye mradi huo zinatokana na mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, nayo imekuwa ahadi ambayo tumeisema kwa muda. Lakini niseme na kuwapa matumaini Watanzania kwamba tulipofikia sasa mkandarasi mshauri mwelekezi anatayarisha makabrasha ya tenda na tunatarajia mwezi wa tatu tenda itakuwa imetangazwa ili kumjua nani aliyeshinda ili aanze kutekeleza miradi hiyo. Miradi hiyo kama nilivyosema inahusu Wilaya ya Bukombe na baadhi ya maeneo ya Kahama, Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Magu, Bariadi pamoja na Mkoa wa Arusha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, kwa kuwa kampeni za mwaka 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa umeme wa Isengwa, Baragane, Lupiga, Mwandoya mpaka Kijiji cha Igobe na kwa kuwa mradi huu sasa hivi uko hatua za kukamilika, wananchi wa kisasa wanampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake na kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwenyewe alisema atakuja kuzindua mradi huu na wananchi wa Kisesa wanampongeza kwa kutekeleza ahadi yake mapema Je, Mheshimiwa Rais sasa hivi atakuwa tayari kuja kuuzindua mradi huu?

**MBUNGE FULANI:** Kwani Rais yupo hapa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunapokea hizo salamu za pongezi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Nishati inaendelea kuwapa matumaini na kuwahakikishia wananchi wa Tanzania wote ambao miradi ile tumekuwa tukiisema katika mikoa 16 inayotekelezwa, mmoja wao ukiwa ambao Mheshimiwa Mpina anausema, itatekelezwa ndani ya ratiba kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ombi la kumwomba Mheshimiwa Rais akazindue kama ambavyo Watanzania wa maeneo mbalimbali wangependa kushuhudia uzinduzi wa utekelezaji wa ahadi ambazo Chama chake anachokiongoza kimewaahidi Watanzania ni nyingi, lakini kwa hili mimi nisimame kama mjumbe, na mjumbe hauwawi, salamu nitazipeleka, ombi nitaliwasilisha ili kama ratiba ya Mheshimiwa Rais itaruhusu, basi atafika, vinginevyo tutapokea maelekezo yake ikiwepo mimi mwenyewe kufika katika eneo la tukio kushuhudia uzinduzi huo. Ahsante.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mji wa Kahama unakua kwa kasi na mahitaji ya wananchi ya umeme yanaongezeka pia kwa kasi hiyo; na kwa kuwa mwaka 2007 Rais alipofanya ziara Wilayani Kahama wananchi walimlalamikia juu ya ukiritimba uliopo wa kuunganishiwa umeme na kwa kuwa Mheshimiwa Rais zaidi ya mara mbili ndani ya Bunge hili alihidi kuja Kahama kutatua tatizo hili. Je, leo anawaambia nini wananchi wa Mji wa Kahama kuhusu tatizo sugu la kuunganishiwa umeme? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kweli kwamba tulishatoa maelekezo mara kadhaa na kila wakati sisi tunapotoa ufafanuzi wa majibu ya Waheshimiwa Wabunge tunawashirikisha wataalam wetu na kuwaagiza kushughulikia matatizo ambayo yanahusika. Hivi karibuni kwa miezi kadhaa iliyopita taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba, juhudi zilifanyika kwa wataalam wetu na sisi tumekuwa tukifuatilia kuboresha utendaji kazi wa Shirika. Lakini kama bado yapo nayachukua na tutaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Lembeli kujua chanzo ni nini, masuala ya kiufundi au ukitimba kwa sababu ya vifaa au ni nini hasa tatizo, tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Lembeli.

**SPIKA:** Ahsante. Kutokana na muda, tunaendelea na swali la mwisho na Mheshimiwa Selemani S. Bungara atauliza swali hilo.

Na. 80

**Matokeo ya Uchunguzi wa Kufa kwa Mifugo Katika Kisiwa cha Songosongo**

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA** aliuliza:-

Kati ya Julai, 2008 na 17 Desemba, 2009 kulitokea madhara ya kufa ng'ombe wapatao 68 na mbuzi 19 katika Kisiwa cha Songosongo baada ya kunywa maji yanayodaiwa kuwa na mabaki yaliyotokana na uzalishaji wa gesi, wataalam kutoka *ERC, AMINEX, NEMC, TPDC*, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Afya pamoja na *OCD* walifika Songosongo kufuatilia tukio hilo:-

(a) Je, Serikali inatoa majibu gani kwa wananchi wa Songosongo juu ya matokeo ya uchunguzi huo?

(b) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi waliopoteza mifugo yao juu ya kulipwa fidia?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani madhubuti ya kuzuia madhara hayo yasiendelee kutokea kwa viumbe hai vyote katika kisiwa hicho?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, maarufu kama Bwege. *(Makofi/Kicheko)*

Mbunge wa Kilwa Kusini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo ya Kisiwa cha Songosongo unafanywa na Makampuni ya Ndovu *Resources* kuanzia mwaka 1999 na *Pan African Energy* mwaka 2001. Kampuni ya Songas inazalisha gesi asili na kuisafirisha mpaka Dar es Salaam kuanzia mwaka 2004. Ndovu *Resources* imeshachoronga visima vinne, *Pan African Energy* wamechoroga kisima kimoja. Taarifa za kutokea kwa vifo vya wanyama ziliripotiwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *TPDC* na kwa kampuni ya Ndovu *Resources* tarehe 10 Agosti, 2009.

Baada ya taarifa hizo, juhudi zilifanyika katika kupata ukweli wa taarifa hizo. Juhudi hizo zilibainishwa kuwa Serikali ya Kijiji na Afisa wa Mifugo wa Wilaya ya Kilwa Masoko hakuwa na taarifa kuhusu hao ng'ombe 68 na mbuzi 19 waliosemekana kufa kutokana na kunywa maji yaliyosemekana yalikuwa na sumu. Maelezo tuliyoyapata ni kwamba vifo vya wanyama wengi kiasi hicho katika kisiwa kidogo cha Songosongo vingejulikana kila mahali, hivyo taarifa hiyo hiyo ya vifo vilivyosemekana ilikosa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira *(NEMC)* ya tarehe 12 Oktoba, 2009 ilithibitisha kuwa hakuna ushahidi wa vifo vya wanyama katika Kisiwa cha Songosongo. Vilevile katika taarifa ya *NEMC* ambayo ilihusisha uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ilionesha kuwa kulikuwa na viashiria vya dawa ya *thiodine* katika udongo wa eneo la tukio. Hata hivyo, *thiodine* haitumiki kwenye shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asili bali inatumika katika shughuli zingine. Kwa mfano, taarifa tuliyonayo ilishawahi kutumika katika shughuli za kilimo na hasa kunyunyizia au kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hapo juu hakuna ushahidi wa vifo vya wanyama hao na hivyo kukosa vigezo na sababu za kisheria kuhalalisha fidia yoyote.

(c) Mheshimiwa Spika, makampuni ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi ya asili yana mikataba na *TPDC* na yanafanya kazi kwa kuzingatia mikataba husika na sheria za nchi zetu. *TPDC* inasimamia makampuni hayo kikamilifu na kuhakikisha kwamba yanafuata taratibu zote za usalama wa mazingira chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mazingira nchini, *NEMC*. Madawa yote yanayotumiwa na makampuni haya ya utafiti na uchimbaji yanaidhinishwa na *NEMC* na *TPDC*. Kampuni ya Ndovu *Resources* na makampuni yote mengine yanayofanya shughuli za uchimbaji katika Kisiwa cha Songosongo yanaendelea kufuata kwa ukamilifu masharti yote ya mazingira salama chini ya usimamizi wa *NEMC* na *TPDC* na Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na jina langu la Ubwege, je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa jibu lake lina utata wananchi wanasema ng'ombe wao wamekufa na Maafisa wa Mifugo wanasema hawakufa. Je, yupo tayari mimi na yeye kuonana na watu hao kuhakikisha kwamba ng'ombe wao hawakufa? Yuko tayari kwenda Songosongo kuonana na watu hao?

Mbili, tangu 2009 mpaka leo mlikuwa hamjawajibu watu wa Songosongo, ni kwa sababu gani?

**SPIKA:** Mbwege! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kweli tumefanyia kazi jambo hili. Naomba niseme kwa dhati na tukiwa *serious* siyo kwamba labda tunafanya kwa sababu ya utani, hapana, hili jambo lishawahi kujitokeza kwenye Bunge lililopita, bahati mbaya au nzuri Mheshimiwa Bwege alikuwa bado hajawa Mbunge kipindi hicho. Lakini lilishawahi kuwasilishwa kwetu kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwepo kipindi kile. Lakini kwa ombi lake nipo tayari mimi na wenzangu kuangalia kama taarifa zote za Kiserikali pengine bado zina upungufu ambao tunaweza kuufanyia kazi. Kwa hiyo, hilo nakubaliana naye.

Lakini la pili, kama nilivyosema maelezo haya yanashabihiana na niliyosema awali kwamba, jambo hili lilijitokeza tangu mwaka juzi na lilishaulizwa na hata hapa Bungeni tulishawahi kusema, lakini pia ufuatiliaji kwa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao wa Wizarani na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara yetu lilishafanyika na tulishalifanyia kazi. Lakini bado nasisitiza kwamba kama inapendeza na ni muhimu na ni lazima kufanya hivyo tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuona kama iko namna pia tunaweza kuboresha ama kupata ukweli zaidi ya ule ambao ulipatikana kipindi kile. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha naomba tuendelee na shughuli zinazofuata. Kwanza kabisa naomba niwatambulishe wageni ambao tunao hapa Bungeni, kuna wageni wa Mheshimiwa John Cheyo, ambao ni Mheshimiwa Elias Lazaro, huyu ni Diwani wa Nkoma akifuatana na wakulima wanne, Mheshimiwa Diwani yuko wapi. Karibu sana na hao wakulima bila shaka ni wakulima wa pamba na nini. Tunawapongezeni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 45 wanaochukua Shahada ya Kwanza na wengine 82 wanaochukua *Diploma* kutoka Chuo cha Biashara *(CBE),* Dodoma. Naomba wanafunzi wa *CBE* wote wasimame walipo. Ahsante sana msome vizuri na muwe tayari kutafuta namna ya kujiajiri, ndiyo tunachozungumza hapa. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi tisa ambao ni raia wa kigeni wanaofundisha chuo kikuu cha Dodoma, we have those who are lecturing at University of Dodoma, you are welcome. Ahsante sana, karibuni sana, mnakaribishwa kwetu. *(Makofi)*

*Then* tuna wageni kutoka *INDECOM* ya Dar es Salaam ambao ni ndugu Alfred Mwenisongole na ndugu Mwaibale. Naomba hao wasimame walipo, ndugu Mwenisongole na Mwaibale, sijawaona. Ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi saba kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo. Wako wapi wanafunzi wa Hombolo, ahsante. Ndiyo nyie mtakaofanya kwenye Halmashauri zetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Naomba wasimame, sijui hawa kama wanajumuisha na wajukuu zake Mheshimiwa Batenga, sijui maana kuna wajukuu wa Mheshimiwa Batenga sikuambiwa majina yao, lakini yuko George Luzige na Nisi Gardener, nasikia hawa ni wajukuu wa Mheshimiwa Batenga, lakini wanasoma uko *UDOM*. Pia tunao wanafunzi wawili kutoka Ujerumani wamekuja kwa ajili ya kujitolea kufundisha katika Mkoa wa Kilimanjaro, *volunteer from German, they can stand*, ahsante sana, karibu sana na tunashukuru kwa kazi mnayokuja kufanya. *(Makofi)*

Wageni wengine wote mnakaribishwa hawa tunaosoma ni wale walioandikishwa katika ofisi yangu ya mawasiliano, lakini wageni wote mnakaribishwa, Bunge ni kwa ajili ya kusikiliza watu wote.

Waheshimiwa naomba nitangaze kazi za Kamati katika kipindi hiki. Yuko Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili, kwa hiyo saa saba mchana Kamati ya Viwanda na Biashara mtakuwa na kikao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa nane mchana katika Ukumbi Namba 227, Jengo la Utawala kutakuwa na kikao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya *Commonwealth Parliamentary Association,* Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA*, Tawi la Tanzania kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa B. Nadhani wenyewe mnajifahamu.

Pia, nina matangazo kutoka kwa Neema Kiula ambaye ni *Desk Officer wa SADC Parliamentary Forum*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa *SADC Parliamentary Forum* kwamba kutakuwa na kikao cha kazi leo tarehe 7, saa saba mchana katika ukumbi wa *Msekwa Lounge*, mtajua wenyewe, lakini Wajumbe nyie siyo wengi, hivyo naomba mkahudhurie pale kwa sababu mnatakiwa m-*coordinate* mambo yenu katika vikao vya *SADC*.

Pia Afisa Habari Ndugu Owen Mwandumbya anaomba niwatangazie kwamba Maafisa kutoka Shirika la Nyumba Tanzania yaani *National Housing Cooperation* wapo katika viwanja vya Bunge wakitoa maelezo kuhusu mradi wa nyumba wa Medeli pamoja na huduma mbalimbali za *National Housing Cooperation*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kutembelea banda lao lililopo karibu na jengo la habari kwa lengo la kupata maelezo mbalimbali kuhusu huduma hizi. Kwa hiyo, mnafahamu *National Housing* wanajenga nyumba zao eneo la Medeli, kwa hiyo mnaweza kupata maelezo zaidi.

Waheshimiwa mnapoongea tunawasikia wote, tafadhali mpunguze sauti wakati mkizungumza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnaalikwa kupita pale ili kupata maelezo na kuna utaratibu wa *mortgage financing* ambao mnaweza kufaidika nao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nimemaliza matangazo. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yaliyotolewa na Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nimekuona, ulikuwa na…

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Zambi.

**SPIKA:** Ndiyo, Mheshimiwa Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa kifungu cha 47 na cha 48 (2) na (3).

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi kupitia *TBC* Taifa Redio, zimetangazwa habari na nataka kuamini kwamba *TBC* ni chombo cha Serikali, ni chombo cha kuaminika na kwa hiyo kinapotoa taarifa tunategemea taarifa hizi ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kwamba Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Taifa, Muhimbili wameingia kwenye mgomo, lakini pia imeelezwa kwamba hali za wagonjwa katika Hospitali ya Taifa, Muhimbili pamoja na hatua zote na taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii tarehe 3 Februari, 2012, bado hali ya matibabu Muhimbili ni mbaya na sasa kufuatia taarifa hii ya Madaktari Bingwa kugoma hali imekuwa mbaya zaidi.

Lakini si hivyo tu, nimeongea na baadhi ya watumishi katika Hospitali ya Taifa, Muhimbili baada ya Madaktari Bingwa kuingia kwenye mgomo wagonjwa wanaanza kurudishwa na wauguzi pia wanatafakari wafanye nini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote yaliyotokea hili jambo nafikiria kwamba ni jambo la dharura hatuwezi kuendelea kujadili mambo mengine wakati jambo hili linalohusu afya za Watanzania linaendelea kuwa katika hali mbaya.

Kwa hiyo, kwa kutumia kifungu cha 47(3), naomba kwa dhati kabisa niwaombe Wabunge wenzangu mniunge mkono ili Serikali na Mheshimiwa Spika, kwa kutumia busara yako tuahirishe shughuli nyingine ili Serikali itoe tamko au Bunge lako lijadili hali hii ili Watanzania waelewe na kama Madaktari Bingwa kuna kigugumizi kwa Serikali kuwalipa madai yao ni nini mpaka tuingie kwenye hali hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge nitoe hoja ili tujadili jambo hili la dharura kwa Watanzania na kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI SAID BUNGALA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mliosimama naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge kwa namna zote suala la mgomo wa Madaktari tunali-*mishandle* na matokeo yake sasa linakuwa kama ni kitu ambacho hakionekani kitokee wapi.

Lilipoanza suala hili tulitaka tujadili hapa lakini tukasema Serikali itatoa kauli, Serikali ikatoa kauli, Naibu Spika akikaa hapa kauli ya Serikali ikapelekwa kwa Kamati inayohusika na wakati huohuo Serikali yenyewe ikasema kuna Kamati nyingine imeundwa. Kamati yenu ya Bunge bado iko kwenye shughuli hii hata hivi leo, sasa ninyi hamuoni kabisa, nasema kila siku kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwe watulivu hasa katika mambo makubwa kama haya. Hili ni suala kubwa sana, sasa tukisema hapa kila mtu aanze kusema kweli hatutaki kujibu hili swali, sasa mimi kwa kutumia busara ya kiti, hili siruhusu mpaka Kamati yangu irudi. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Unaongoza? Hakuna chochote kilichokaa hapa cha kutakiwa kuongozwa, hakuna kitu chochote cha kuongoza isipokuwa mimi, huwezi kuongoza kikao changu mimi. Tunaendelea!

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Hakuna taarifa yoyote. Waziri mhusika mtoa hoja! Waheshimiwa Wabunge, tunapokea utekelezaji wa Serikali katika hoja yetu ya Mkutano wa Tano kuhusu taarifa ya Kamati Ndogo iliyohusika na mambo ya gesi. Kwa hiyo, Waziri anachokifanya, anatoa majibu ya baadhi ya hoja yaliyotokana na ile Kamati. Akimaliza Mheshimiwa Waziri, tuliagiza Kamati yetu iliyohusika kupokea maelezo ya Serikali kama yamekaa vizuri au vinginevyo, kisha nitawaruhusu kujadili, lakini tutajadili mpaka saa saba tu kwa sababu tunarejea yaliyokuwa yamefanyika.

Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 37(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 na kwa kuzingatia kwamba tarehe 7/2/2012, Wizara yangu iliwasilisha mezani kwako na mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Nishati na Madini

kuhusu uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi nchini. Sasa naomba kuwasilisha taarifa ya Serikali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini iliyoshughulikia Sekta Ndogo ya Gesi Asili Nchini na kuwasilishwa Bungeni tarehe 18 Novemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Tano wa Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliwasilisha taarifa yenye mapendekezo 26 yaliyoridhiwa na Bunge na kuhitaji Serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo kuhusu uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi nchini.

Aidha, ni dhamira ya Serikali kuendelea na utekelezaji wa baadhi ya maazimio ambayo yanahitaji muda mrefu zaidi ili kukamilisha mchakato wake hasa yale yanayohusu utungaji na marekebisho ya Sheria, marekebisho ya mifumo mbalimbali na uimarishaji wa Taasisi zinazohusika na uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa ya utekelezaji, naomba kutoa maelezo mafupi juu ya uwekezaji wa *Pan African Energy Tanzania Limited* kati ya mwaka 2004 na 2009, kampuni hii iliwekeza kiasi cha dola za Marekani milioni 134,170,212 katika mradi wa kuendeleza gesi ya ziada chini ya mkataba wa kugawana mapato yaani *Production Sharing Agreement PSA* kati yake na Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya *Petrol Tanzania (TPDC)*.

Gharama hizo za uwekezaji zilipaswa kurejeshwa *Pan Africa Energy*, baada ya mauzo kuanza. Aidha, katika gharama hizo…..

**SPIKA:** Mnaotoka naomba mtoke kimyakimya, siyo tena mazungumzo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Aidha, katika gharama hizo, *Pan Africa Energy* walishajirejeshea kiasi cha dola za Marekani 79,846,171 na kubakiza kiasi cha dola za Marekani 54,324,041 kufuatana na taratibu za *Production Sharing Agreement.* Kwa maana hiyo, wakati wa ukaguzi kiasi hicho cha gharama kilikuwa bado hakijarejeshwa kwa mwekezaji, ukaguzi uliofanywa kati ya mwaka 2004-2009 ulibaini kuwa gharama zisizostahili anazodai *Pan African Energy* zenye jumla ya dola za Marekani 28,053,680 ziliingizwa kwenye vitabu vya hesabu kulingana na mkataba. Kwa kosa hili, kama mapato yatokanayo na mauzo ya gesi yangekuwa ya kutosha kwa kipindi hicho, Kampuni ya *Pan African Energy* ingejilipa dola za Marekani 28,053,680 na kuikosesha Serikali mgawo wake wa kiasi cha dola za Marekani milioni 20.1.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua taarifa, kuishauri Wizara na kutuongoza ili tuweze kwenda kulingana na utaratibu na maelekezo ya Bunge. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotuwezesha kuleta taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wote pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wenu mahiri uliosaidia Wizara yangu kutekeleza maazimio ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza maazimio ya Bunge letu Tukufu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, azimio namba moja (1), lilihusu Serikali hususan Wizara ya Nishati na Madini kusimamia sambamba na *TPDC* kutetea maslahi ya Taifa. Kuhusu utekelezaji wake; Serikali imepokea ushauri wa Bunge na tunaahidi Wizara itaendelea kusimamia sambamba na *TPDC* kutetea maslahi ya Taifa na napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba uhusiano wa Wizara na *TPDC* unaendelea kuboreshwa. Pamoja na kuboresha uhusiano, Serikali itaendelea kuelimisha wadau wengine ili waweze kuelewa umuhimu wa shughuli za *TPDC* kwa maslahi ya Taifa.

Aidha, kufuatia kukua kwa kazi kwa matumizi ya gesi asili na ugunduzi wa hivi karibuni katika maeneo ya kina kirefu cha Bahari, Serikali imeamua kuanzisha Kitengo cha Uendelezaji Gesi Asili chini ya Idara ya Nishati ambapo moja ya majukumu yake ni kuhakikisha usimamizi wa karibu unakuwepo katika miradi yote inayohusisha uendelezaji wa matumizi ya gesi asili. Kwa kufanya hivi tutahakikisha kwamba tija na ufanisi vinakuwepo katika miradi yote ikiwa ni pamoja na uzalishaji umeme, matumizi ya viwandani na

hata kwenye kilimo hapo baadaye pindi mipango ya uzalishaji wa mbolea kwa kutumia gesi itakapotekelezwa.

Pamoja na hatua zilizoelezwa hapo juu, Serikali imechukua hatua zifuatazo kwenye sekta hii ili kuboresha zaidi utendaji wake:-

Kwanza, kuanzisha Kitengo cha Uendelezaji wa Gesi Asili kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ndani ya Wizara ya Nishati na Madini.

Pili, Serikali imetoa kibali kwa *TPDC* kuwaajiri watumishi 51 kwa mwaka 2011/2012 na kwa mwaka wa fedha 2012/2013 mpaka mwaka 2014/2015, wanatarajiwa wafanyakazi wapatao 192 wataajiriwa. Serikali imeanza utayarishaji wa mpango kabambe wa matumizi ya gesi asili yaani *gas master plan*, rasimu ya mpango huo itakamilika mwezi Juni mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, azimio namba mbili (2), lilihusu mashaka makubwa katika uendeshaji wa sekta hii muhimu ya gesi asili. Utekelezaji wake ni kwamba Serikali imepokea ushauri wa Bunge na maelezo ya ziada ya kwamba kuanzia mwaka 2004 hadi mwaka *2009 Pan African Energy* ilitoa taarifa *TPDC* kuwa imetumia kiasi cha dola za Marekani milioni 134,170,212. Aidha, katika gharama hizo, *Pan African Energy* walishajirudishia kiasi cha dola za Marekani 79,846,171 na kubakiza dola za Marekani 54,324,041 kufuatana na taratibu za Mkataba wa *Production Sharing Agreement*.

Kuanzia mwezi Oktoba, 2007 *TPDC* ilifanya ukaguzi wa gharama hizo na kubaini kuwa gharama za kiasi cha dola za Marekani 64,496,756 ziliingizwa na *Pan African Energy* kwenye hesabu kimakosa kwa misingi ya *PSA*. Tarehe 12 Julai, 2011 *Pan African Energy* walikubali na kufikia makubaliano na *TPDC* kuwa kati ya gharama hizo dola za Marekani 28,053,680 ziliingizwa kimakosa katika hesabu na kiasi kilichobaki dola za Marekani 36,443,076 waliahidi kuzitolea maelezo. Kiambatanisho namba moja ambacho kinaonekana kwenye taarifa hii kinaelezea.

Kwa kuwa kampuni ya *Pan African Energy* haijatoa maelezo kuhusu kiasi kilichobaki cha dola za Marekani 35,443,076 walizokuwa wameahidi kutolea maelezo, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum ili kuhakiki kiasi hicho. Marejesho ya *Pan African Energy* kwa kipindi cha mwaka 2004/2009 ni dola za Marekani 79.85 kati ya dola za Marekani milioni 134.17, hivyo kuwa na bakaa ya dola za Marekani milioni 54.32.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maamuzi ya kupeleka masuala yote *ya Pan African Energy* kwenye Kamati ya Majadiliano ya Serikali yaani *Government Negotiation Team* iliyoundwa na Serikali ikijumuisha Wataalam kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Shirika la Maendeleo ya Petroli *Tanzania TPDC*, suala hilo la madai ni moja kati ya hadidu za rejea zitakazoshughulikiwa na *GNT*. Pamoja na kumwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakiki madai ya *Pan African Energy, TPDC* iliwapelekea *Pan African Energy notice of exception* ya tarehe 19/1/2012 kulingana na kifungu cha 1.7(b) cha *Annex (d)* ya *PSA*. Hii inafuatia *Pan African Energy* kueleza msimamo wao kupitia barua yao ya tarehe 26/10/2011 wakijibu barua ya *TPDC* ya tarehe 24 Oktoba, 2011 na maelezo ya ufafanuzi kuhusu mawasiliano hayo yanajitokeza katika kiambatanisho namba mbili.

Mheshimiwa Spika, barua za mawasiliano kati ya *TPDC* na *Pan African Energy* kuhusu hesabu zinazobishaniwa tumeziambatanisha kama kiambatanisho namba mbili. Nafikiri katika hilo mawasiliano yote kati ya *TPDC* na *Pan African Energy* yataonekana katika kiambatanisho namba mbili.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tatu (3), Kamati ilishauri kwamba mapunjo ya Serikali yanayofikia dola za Marekani milioni 20.1 yarejeshwe mara moja na riba kwa viwango vya Benki yaani *Time Value for Money*. Aidha, upelelezi ufanyike katika hesabu za *Pan African Energy* kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu. Maelezo ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Serikali imepokea ushauri wa Bunge, kwa kuwa Kampuni ya *Pan African Energy* haijatoa maelezo kuhusu kiasi kilichobaki cha dola za Marekani thelathini na tano milioni, laki nne na mia tano sitini, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum ili kuhakiki madai hayo kama nilivyoeleza.

Kutokana na uamuzi wa Serikali kupeleka masuala yote kwenye *GNT*, suala la madai ni moja kati ya hadidu za rejea kama nilivyosema. Matokeo ya uhakiki wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na yale ya majadiliano ya Kamati ya Majadiliano ya Serikali yaani *GNT* yataiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kulingana na mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba nne (4), lilihusu Kamati ilivyoshauri kwamba mkataba wa *Pan African Energy Tanzania* usitishwe. Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge na itazingatia taratibu zote za kisheria na kimkataba na itatafakari suala hili kwa umakini na itazingatia athari za hatua hiyo katika upatikanaji wa gesi ya kutosha kwa ajili ya kulinda uchumi wa nchi yetu.

Kwa mujibu wa mkataba wa *PSA,* utaratibu ufuatao itabidi ufuatwe. Kwanza, chini ya *Annex* (d) ya mkataba wa *PSA* kifungu cha 1.7(b), *TPDC* inatakiwa kutoa *notice* ya siku 90 kuhusu masuala ya hesabu na *Pan African Energy* inatakiwa kujibu hoja hizo ndani ya siku 90.

Pili, chini ya kifungu cha mkataba wa *PSA* 27.1 *TPDC* au *Pan African Energy* anaweza kutangaza mgogoro kwa kuwasilisha barua rasmi ya *notice* ya kuwepo kwa mgogoro kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

Tatu, ndani ya siku 30 ya kupokea *notice* hiyo *TPDC* au *Pan African Energy* kutegemea na yeyote atakayekuwa ametangaza mgogoro wanatakiwa kujibu katika kutatua mgogoro huo kwa maelewano ikiwa ni pamoja na kujadili suala hilo katika vikao vya pamoja vya *Advisory Committee*.

Nne, kama mgogoro hautatatuliwa kwa maelewano *TPDC* na *Pan African Energy* watawasilisha mgogoro huo kwa Wakuu wa Taasisi zao yaani *(Chief Executives)*. Iwapo Wakuu hao watashindwa kufikia muafaka ndani ya siku 15 au muda zaidi kadri watakavyoona inafaa, mgogoro huo unaweza kuwasilishwa kwa mtaalam mwelekezi yaani (*Technical Expert*) kwa kuwa mgogoro wenyewe ni wa kitaalam. Kwa masuala yasiyo ya kitaalam kama Uhasibu suala hilo linaweza kuwasilishwa Baraza la Usuluhishi (*Arbitration).*

Tano, Baraza la Usuluhishi litatumia taratibu za kuendesha mashauri chini ya *International Centre for Settlement of Investment Disputes*. Aidha, Baraza hilo litakaa Jijini London na litatumia Sheria za Tanzania katika kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo Serikali imeamua hatua zifuatazo kuchukuliwa:-

Kwanza, kutafakari athari hasi ambazo zinaweza kujitokeza kama mgogoro ungetangazwa mara moja ambazo zinaweza kuwa pamoja na kusimamisha shughuli za uzalishaji gesi, uendelezaji wa uchimbaji wa visima vipya na mazungumzo kati ya Serikali na wawekezaji wengine kwenye miradi mipya.

Pili, ili kuimarisha uhakiki uliokwishafanywa na *TPDC*, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum na ni *speciality* kwa gharama ambazo *Pan African Energy Tanzania* bado haujazitolea maelezo ya kuridhisha.

Tatu, Serikali imeunda Kamati ya Majadiliano itakayotoa mwelekeo wa kufuata juu ya suala hili kwa kuzingatia athari zake. Kamati hiyo itaanza kazi tarehe 20 Februari, 2012 na kuwasilisha ripoti ya majadiliano na *Pan African Energy* mwishoni mwa mwezi Machi, 2012. Kamati hiyo itatoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu hatua za kuchukua na maoni ya majibu ya *letter of exception* kama nilivyoielezea awali. Serikali imetengeneza hadidu za rejea ambazo zinagusa masuala yote yanayohusiana na tofauti baina ya Serikali na *Pan African Energy*.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tano (5), hili kimuhtasari Kamati inashauri utaratibu wa *Pan African Energy Tanzania* kujirejeshea gharama za usambazaji chini ya muundo wa *PSA* usitishwe mara moja. Maelezo ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Pamoja na maelekezo mazuri ya Bunge, Serikali ilishatoa maelekezo kuhusu utenganishaji wa gharama hii, kutekeleza ushauri kutoka kwa Mshauri Mwelekezi. Aidha, Wizara iliagiza *TPDC* na *Pan African Energy* kutekeleza ushauri wa Mshauri Mwelekezi kuanzia tarehe 1 Januari, 2010 na kuhakikisha kuwa gharama za usambazaji wa gesi zinatokana na *tariff* ya usambazaji wa gesi. Aidha, katika ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2010 uliofanywa na *TPDC* umethibitisha kuwa gharama hizo zimeshaondolewa kwenye *PSA*.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba sita (6), kiufupi lilitaka Serikali kama Msimamizi wa Mikataba inayo haki ya kukagua gharama za mwekezaji. Maelezo ya utekelezaji ni kwamba, katikati ya miaka ya 1990, Serikali ilisimamisha ajira kwa Wizara na Taasisi zake ikiwemo *TPDC*. Hivyo, kutokana na mabadiliko ya kisera yalisababisha *TPDC* kupunguza wafanyakazi kutoka wafanyakazi 440 hadi 63 tu. Idadi ndogo ya wafanyakazi waliokuwepo Wizarani na *TPDC* wakati wa uendelezaji wa mradi wa Songosongo ilisababisha shughuli za usimamizi na uendelezaji gesi kukosa ukaguzi wa mara kwa mara kama mikataba inavyohitaji. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2006, *TPDC* ilianza kuajiri wataalam mbalimbali wakiwemo wa Jiolojia, Uhandisi, Wanasheria na Wahasibu hadi sasa *TPDC* imeajiri wafanyakazi 45 wa fani mbalimbali.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wizara kwa kutambua umuhimu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na tatizo la upungufu wa wafanyakazi *TPDC* mwaka 2010 Wizara iliazima *TPDC* wataalam watatu ili waisaidie katika ukaguzi wa hesabu za *PSA* mbalimbali zinazosimamiwa na *TPDC*.

Pili, Serikali imetoa kibali kuwa *TPDC* kuajiri watumishi 51 kwa mwaka huu wa fedha kama nilivyoeleza awali na mchakato wa ajira utaanza mara baada ya kumaliza Mkutano huu wa Sita wa Bunge.

Tatu, kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013, mpaka mwaka 2014/2015, *TPDC* wataajiri wafanyakazi 192 wanaohitajika kwa awamu. Kwa kuanzia tayari Serikali imetoa kibali cha *TPDC* kama nilivyosema kuajiri wafanyakazi 51 kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba saba (7) lilihusu kugharamia urejeshaji au utunzaji wa mazingira wa maeneo ya uchimbaji wa gesi pindi gesi itakapokuwa inakaribia kwisha. Maelezo ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Kwenye mikataba yote ya sasa na miaka ya hivi karibuni kuna kifungu kinachoelekeza kuwa Serikali, *TPDC* na Mwekezaji kwa pamoja wataanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kuhifadhi mazingira ya maeneo ya uchimbaji wa mafuta ama gesi mara mafuta ama gesi inapokwisha na visima kufungwa yaani (*abandonment fund)*. Serikali imepokea ushauri huu na itahakikisha Mfuko huo unaanza ili kuhifadhi maeneo ya uchimbaji wa mafuta ama gesi wakati itakapokuwa. Suala hilo lipo katika hadidu za rejea zitakazofanyiwa kazi na Kamati ya Majadiliano.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba nane (8), Kamati ilishauri Mkataba kufanyiwa marejeo ama kupitiwa upya, utekelezaji wake ni kwamba, Serikali kwanza inaupokea ushauri wa Bunge. Lakini pia utaratibu wa kugawana mapato kama ulivyoainishwa katika vifungu vya 10.4 na 10.5 vya *PSA* ulilenga kuwa vitalu vyote tisa vingeendelezwa. Kwa vile *Pan African Energy* iliacha vitalu saba mazungumzo yameanza juu ya mkataba husika ikiwa ni pamoja na kurekebisha utaratibu wa kugawana mapato. Aidha, mazungumzo ya mwisho baina ya Serikali, *TPDC* na *Pan African Energy* yalifanyika kati ya tarehe 14 na 15 Aprili, 2011. Katika Mkutano huo iliundwa timu ya wataalam yaani (*task force)* kutoka *TPDC* na *Pan African Energy* ili kupitia mikataba na kushauri jinsi ya kugawana mapato na mambo mengine ikiwemo utaratibu wa ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa *TPDC* yaani (*participation)* katika mradi, utozaji wa mrabaha na kadhalika. Kikao cha kwanza cha *task force* kilifanyika tarehe 25 Mei, 2011 na kuandaa mapendekezo yanayotakiwa kufanyiwa kazi. Aidha, mwezi Januari, 2012, Serikali imeunda *GNT* yenye Wajumbe toka Hazina, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, *TRA*, Wizara ya Nishati na Madini kama nilivyoelezea ili kuendelea na kazi hiyo. Kamati hiyo itaanza kazi kama nilivyosema tarehe 20 Februari, 2012 na taarifa ya hii Kamati itawasilishwa mwezi Machi. Aidha, mapendekezo ya *task force* yamejumuishwa kwenye hadidu za rejea za Kamati ya Serikali ya Majadiliano yaani *GNT*.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tisa (9), Kamati inaishauri Serikali kuandaa rasimu ya Sheria ya Gesi Asili ili kuhakikisha rasilimali hii muhimu inatumika kwa maslahi ya Taifa. Maelezo ya utekelezaji ni kwamba Serikali inakubaliana na ushauri wa Bunge. Rasimu ya Sheria ya Gesi Asili imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kufanya maandalizi ya Muswada wa Sheria. Muswada huo unatarajiwa kuwasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge hili, aidha, rasimu ya Muswada imezingatia mabadiliko ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi (10), lilihusu kwa kiwango kikubwa ununuzi wa vitu unaofanywa na *Pan African Energy* kama mbia na *TPDC* lakini bila ya kuishirikisha *TPDC*. Maelezo ya utekelezaji ni kwamba Serikali imeupokea ushauri wa Bunge na zaidi ya hapo lengo la kifungu cha 17.3 katika mkataba huo ni kutoa vigezo vya kufikia bei ya ununuzi ikizingatia uchakavu (*depreciation),* kurudisha gharama (*cost recovering)* na misamaha ya kodi (*tax exemption)* kwenye vifaa hivyo kabla ya kufikia bei ya makubaliano. Katika kufikia bei ya kununua vifaa ushauri wa Bunge utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na moja (11), kwa kiasi kikubwa lilihusu kupitia upya baadhi ya vipengele vya mkataba kati ya Serikali na *TPDC*. Utekelezaji ni kwamba ushauri wa Bunge umepokelewa na hatua zimeanza kuchukuliwa. Kama nilivyosema pamoja na mambo mengine Kamati ya Serikali ya majadiliano *GNT* ambayo imeundwa itafanya pamoja na mambo mengine kudurusu upya baadhi ya vipengele vya mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na mbili (12), azimio hili liliona kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeonesha kutokuwa makini katika kupitia, kujadili na kusimamia mikataba kama hii inayoingia kwa niaba ya Serikali. Maelezo yake ni kwamba, itakumbukwa kuwa maandalizi ya mradi wa Songosongo yalianza mwaka 1994 ambapo ilikuwa vigumu kupata mwekezaji. Hali hii ilisababisha kuwepo na mikataba mingi ambayo pamoja na mambo mengine mwekezaji kuwa na uhakika wa uwekezaji alioufanya. Tangu utekelezaji wa mradi ulipoanza mazingira ya uwekezaji yalikuwa yakiimarika na hivyo kusababisha kufanyika durusu za mara kwa mara za mikataba pindi inapohitajika. Mpaka sasa mikataba ya Songosongo imedurusiwa mara tatu yaani mwaka 2001, 2004 na 2008 ambapo baadhi ya mikataba kama ya *ESCROW* imefutwa.

Mheshimiwa Spika, majadiliano yanaendelea kati ya wadau wote, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *TPDC*, *TANESCO, SONGAS* na *Pan African Energy* kupitia upya mikataba ya miradi na kufanya marekebisho yanayostahili. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepokea maelekezo ya Bunge na itaendelea kuzisaidia Wizara na *TPDC* kwa kuchambua na kusimamia mikataba kati ya Serikali na wawekezaji kwa maslahi ya Taifa, aidha, pale ambapo Serikali itabaini utendaji mbovu au uzembe umesababisha hasara, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote waliohusika. Hata hivyo, ushauri na maoni ya Kamati, Serikali imeupokea.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na tatu (13), Serikali kama msimamizi wa kutoa vibali vya ajira nchini kupitia Ofisi yake ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kufanya utafiti na tathmini ya ajira zinazoombwa ambazo vibali vyake vinatakiwa kutoka haraka ili maslahi ya Taifa yalindwe. Haya kwa kifupi ndio yalikuwa maoni na ushauri wa Kamati, hatimaye yalifanywa kuwa Azimio la Bunge. Serikali imepokea ushauri wa Bunge, zaidi ya hapo ni kwamba, kwa kuzingatia kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya gesi asili, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo pamoja na wadau wengine kama vile Makampuni ya Utafutaji Mafuta na Gesi inakamilisha majadiliano ya kutekeleza miradi ya kujenga uwezo (*capacity building*) kwa Serikali na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, lengo la mkakati huu ni kuongeza uwezo na kuendeleza na kusimamia sekta ndogo ya gesi asili. Kama ilivyoelezwa awali, Serikali imetoa kibali kwa *TPDC* kuajiri watumishi 51 kwa mwaka huu wa fedha na kibali kimezingatia uharaka wa watumishi wanaohitajika. Lakini pia kama tulivyosema, ajira zitaendelea kutoka mwaka hadi mwaka kwenye bajeti ya mwaka 2014 na 2015. Kuhusu suala la *succession plan* kwa upande wa *TPDC*, Serikali imeiagiza *TPDC* mikakati ya kuhakikisha kwamba kuna mpango thabiti wa kuachiana madaraka pamoja na kuajiri watumishi wapya.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na nne (14), kwa kiasi kikubwa Azimio hili, Kamati imeridhika kuwa kuna uhusiano mbaya kati ya *Pan African Energy* na *TPDC* na hasa ukizingatia kuwa mahusiano yao ni ya kimkataba na kila upande unao wajibu, una haki ndani ya mkataba. Serikali

imeupokea ushauri huu na hata hivyo, Serikali inakiri kuwepo kwa mawasiliano yasiyoridhisha kati ya *Pan African Energy* na *TPDC*. Kwa kuzingatia hali hiyo Wizara ya Nishati na Madini ilichukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kuwakutanisha wahusika na kujadili masuala yote yaliyoonekana kuwa na utata; na

Pili, kuandaa utaratibu wa manunuzi kwa kushirikiana *TPDC* na *Pan African Energy* na utaratibu huu umeanza kutumika kuanzia mwaka 2011. Aidha, mwaka 2010 Kampuni ya *Pan African Energy* ililazimika kubadilisha mfumo wa uongozi ikiwa ni pamoja na kumbadilisha Meneja Mkuu aliyekuwepo Tanzania wakati wa matatizo haya. Kamati ya Serikali ya Majadiliano iliyoundwa itashughulikia vilevile kuimarisha uhusiano kati ya *TPDC* na *Pan African Energy*.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na tano (15), hili lilihusu malalamiko ya *TANESCO* dhidi ya *Pan African Energy*, Serikali ilipokea ushauri wa Bunge na zaidi ya hapo kwa kutambua kuwepo kwa hali hii Serikali imewakutanisha *TANESCO* na *Pan African Energy*. Maafisa wa Taasisi hizi walipitia kwa karibu mfumo mzima wa uzalishaji na usafirishaji wa gesi na kukubaliana njia bora ya kubadilishana taarifa ili kupunguza malalamiko. Kutokana na maagizo ya Bunge, Serikali imeiagiza *Pan African Energy* kutoa taarifa za uzalishaji na usambazaji gesi kwa Wizara, *TPDC* na *TANESCO* kila siku na agizo hili linaendelea kutekelezwa. Tangu hatua hii ichukuliwe uhusiano na utendaji kazi wa Taasisi hizi mbili umeimarika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na sita (16), lilihusu Kamati kuishauri Serikali kufanya jitihada za ziada kuhakikisha visima vilivyoharibika vinaokolewa ili viendelee kuzalisha kama ilivyo kawaida. Utekelezaji wake ni kwamba, kwanza Serikali imepokea ushauri wa Bunge, lakini pia kazi ya kukarabati visima Na. SS5 na SS7 na SS 9 vilivyoathiriwa na kutu kali itafanyika baada ya kuchimba visima Na. SSA. SS maana yake ni Songosongo. Kwa hiyo, ni Kisima Songosongo Na. 5 au 7 na Songosongo Na. 9, hayo ndiyo majina au ubatizo wa visima hivyo vimepewa na wadau wakati wa kuingia mikataba hii. Hatua hii imechukuliwa kwa vile kazi ya kukarabati visima hivyo vitatu huchukua muda mrefu. Visima hivi vilichimbwa mwaka 1974 na kusababisha kukosekana kwa gesi ambayo inahitajika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani. Uamuzi wa kuharakisha uchimbaji wa kisima SSA badala ya kukarabati visima vyenye kutu unatokana na sababu zifuatazo:-

Kwanza, kitaalam hali ya visima vyenye kutu kwa sasa haitabiriki; inaweza kuchukua muda mrefu kufikia uamuzi wa kuvikarabati au vikashindikana kuvikarabati na kulazimika kuviziba, hivyo kuathiri kiwango cha upatikanaji wa gesi kwa mitambo ya umeme; na

Pili, kuchimba visima vipya, kwanza kabla ya kukarabati kunatoa uhakika kuwa gesi asili ya kutosha inapatikana haraka kwa matumizi ya mitambo ya umeme. Hivi sasa kisima cha SSA kinachimbwa Kisiwani Songosongo ambacho kinakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha futi za ujazo milioni 60 kwa siku. Aidha, *Pan African Energy* itakarabati kisima SS10 ambapo uwezo wake wa kuzalisha utaongezeka kutoka futi za ujazo milioni 50 kwa siku hadi kufikia milioni 60 kwa siku. Visima hivi pamoja na visima SS3 na SS4 kwa pamoja vitaweza kuzalisha gesi ya kutosha kwa mahitaji ya kuzalisha umeme na viwandani. Baada ya kuwa na gesi ya uhakika na ya kutosha ndipo ukarabati wa visima SS5, SS7 na SS9 utafanyika. Serikali inatambua umuhimu wa kuchimba kisima SSA kutumia mtambo unaoitwa *SAKSON PR5* ambao una uwezo mkubwa zaidi kuliko *CAROIL* 6 na ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na saba (17), katika hili Kamati inasisitiza *Pan African Energy* izilipe fedha ambazo zinabishaniwa haraka iwezekanavyo. Katika hili utekelezaji ni kwamba, kwanza Serikali imepokea maoni ya Wabunge, lakini pia taratibu za mkataba zitafuatwa na *TPDC* imeagizwa kuhakikisha suala hili linafuatiliwa na linamalizika haraka iwezekanavyo. Suala hili pia litafanyiwa kazi na Kamati ya Serikali ya Majadiliano *GNT* kama tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na nane (18), Kamati inaishauri Serikali kupitia upya mfumo wa utendaji wa Wizara utakaohakikisha maslahi ya Taifa yanazingatiwa. Serikali imeupokea ushauri wa Bunge na zaidi ya hapo kukosekana kwa sera mahsusi, sheria na mpango kabambe yaani *Gas Master Plan* unatoa mwanya kwa baadhi ya wadau wa sekta wenye nia mbaya kugonganisha Serikali na Taasisi zake na mara nyingine kwa maslahi yao. Hivi karibuni tumeshuhudia mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ulivyopigwa vita na baadhi ya wadau wakidai kuwa mradi huo hauna manufaa ya kiuchumi. Wizara inajivunia kuona Taasisi imara za *TPDC* na *EWURA* ambazo zimekuwa zikitoa ushauri

Serikalini kuhusu hatua muhimu za kuchukua ili kuhakikisha kuwa sekta ya gesi asili inaimarika kwa maslahi ya wadau wote.

Mheshimiwa Spika, pia hali ya kutoshirikiana iliyokuwepo miaka ya nyuma kati ya Wizara na *EWURA* imerekebishwa na kwa kweli imeboreka ambapo ushirikiano kati ya Wizara na Taasisi za *TPDC* na *EWURA* umezidi kuimarika katika kusimamia masuala ya uendelezaji wa gesi asili nchini ili kuhakikisha kwamba rasilimali hii ya gesi asili inaendelezwa na maslahi ya nchi yanalindwa. Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi zote husika ili kuhakikisha kuwa sekta hii inaendelezwa vizuri kwa maslahi ya nchi kwa kuzingatia matakwa na sheria za Taasisi husika. Pia tunatarajia kwamba kuwepo na Sheria ya Gesi Asili kutachochea maendeleo katika sekta ya gesi asili kwa kuwa sheria hiyo itaeleza kwa uwazi majukumu ya Wizara na Taasisi zinazosimamia sekta za gesi asili. Sheria hiyo itawasilishwa katika Mkutano wa Saba kama tulivyosema kwa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba kumi na tisa (19), hili lilihusu vipengele vya utunzaji wa visima vilivyopo kwenye mkataba vizingatiwe na Kampuni inayohusika kuharibika kwa visima hivyo iwajibike kwa kuvikarabati visima hivyo kwa gharama zake. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Ushauri wa Bunge unapokelewa baada ya kugundulika matatizo ya kuwepo kwa kutu katika visima vya gesi vya SS5, SS7 na SS9 mwishoni mwaka 2010. Wizara ya Nishati na Madini iliiagiza *TPDC*, *Pan African Energy* pamoja na *SONGAS* kufanya tathmini ya uwezo wa visima hivyo pamoja na kuandaa mpango wa kuvikarabati. Hatua za haraka zilizochukuliwa ili kuhakikisha kunakuwepo gesi ya kutosha ni kuchimba kisima cha SSA na kukarabati kisima cha SS10. Maelezo kuhusu mpango huu yapo kwenye jibu la azimio namba kumi na sita (16) kama nilivyoeleza hapo awali. Kuhusu nani awajibike na uharibifu wa visima SS5, SS7 na SS9 Serikali imeliweka kama mojawapo ya hadidu za rejea za Kamati ya Serikali ya Majadiliano ili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini (20), katika hili Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwa katika Sheria ya Gesi itakayotungwa ni lazima iainishe ugatuaji *(unbundling*) kwa upande wa utafutaji, usafirishaji na usambazaji. Serikali umeupokea ushauri wa Bunge na katika rasimu ya Sheria Mpya ya Gesi Asili iliyoandaliwa ambayo itawasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge. Suala la kutenganisha utafutaji, uzalishaji na usambazaji ni miongoni mwa masuala yaliyozingatiwa kama ilivyoelezwa katika taarifa hii hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na moja (21), *TPDC* ikiwa ndiye msimamizi wa Sekta ya gesi kwa niaba ya Serikali, Kamati ilishauri shughuli zote za uwekezaji katika Sekta ya Gesi zisifanyike bila ya kuihusisha *TPDC*. Serikali imeupokea ushauri wa Bunge. Kwa mujibu wa Sheria ya Utafutaji wa Mafuta ya mwaka 1980, Wizara hutoa leseni ya utafutaji na uendelezaji kwa *TPDC*. Aidha, *TPDC* ni mbia katika mikataba yote ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi (*PSA*) hapa nchini. Katika mikataba hiyo ya utafutaji, wawekezaji, yaani kampuni za kutafuta mafuta hushiriki kama wakandarasi wa TPDC tu. Kuhusu uchimbaji wa visima vipya Songo Songo, maelezo ya kina yametolewa katika majibu ya Azimio Na. 16.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na mbili (22), katika hili Kamati ilikuwa na maoni kwamba fedha zinazotolewa na wabia wa *TPDC* zitumike kwa mafunzo yaliyokusudiwa. Serikali imepokea ushauri wa Bunge na katika hili Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa, suala hili halirudiwi tena. Aidha, Serikali inaendelea na uchunguzi kuhusu matumizi ya fedha hizi na hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kwamba wamezitumia isivyokuwa halali. Serikali imebaini utata uliopo kati ya madhumuni na jina la kifungu kinachohusu mafunzo, hivyo Serikali itarekebisha kifungu hiki ili kupanua wigo wa madhumuni ya kifungu kitumike kwa ajili ya kujenga uwezo (*Capacity Building*) kwenye Sekta ya Nishati badala ya mafunzo (*Training and Technology Transfer*) tu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na tatu (23), katika hili ushauri na maoni ambayo baadaye yalikuja kuzaa azimio yanahusu matumizi ya fedha zilizotolewa na Serikali kuondoa tofauti ya bei ya umeme Mikoa ya Lindi na Mtwara. Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Aidha, Serikali inakubali kuwa ni muhimu na ni vizuri kuwa taratibu za fedha zifuatwe. Wizara ya Nishati na Madini itaendelea kuzingatia Sheria na bila kuathiri Mamlaka ya Bunge katika utekelezaji wa Bajeti na Kifungu husika kitarekebishwa katika mwaka wa fedha 2012/13 ili kuondoa tofauti zilizojitokeza katika tafsiri na matumizi ya fedha zilizotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na nne (24), katika hili maelekezo, maoni, ushauri na baadaye kwa kiasi kikubwa yalijielekeza kuhusu kalenda ya ulipaji wa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 216 zilizotumika kuendeleza Mradi wa Gesi Asili wa Songosongo. Serikali imepokea ushauri wa Bunge na zaidi ya hapo Serikali imeishauri Wizara ya Fedha kuandaa mpango wa kulipa deni hilo ili uweze kutekelezwa. Serikali ilisaini mikataba 21 ya Mradi wa Uendelezaji Gesi ya Asili ya Songo Songo tarehe 11 Oktoba 2001 pamoja na *TPDC, TANESCO, Songas, Pan African Energy (T), FMO, EIB, IDA* na *TDFL*. Miongoni mwa mikataba iliyosainiwa ni mkataba wa *Power Purchase Agreement* (*PPA*). Mkataba huu ulisaniwa kati ya kampuni ya *Songas* na *TANESCO*. Mradi wa *Songas* ulianza kuzalisha umeme kutumia gesi asili kuanzia mwezi Julai 2004.

Mchanganuo wa gharama za uendeshaji, ulipaji wa mikopo na mitaji umeainishwa kwenye Kiambatisho Na. (F) cha mkataba wa *PPA*. Mpangilio wa kimkataba ni kuwa mikopo ya Serikali toka Mashirika ya Fedha, Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden – (*SIDA*) inahitajika kulipwa na Serikali baada ya kupokea malipo kutoka kampuni ya *Songas*. Aidha, *TANESCO* wanawajibika kimkataba kumlipa *Songas* malipo yaliyoainishwa kwenye mkataba ikiwa ni *Capacity Charge* na *Energy Charge*.

Serikali ilikopa Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya na SIDA jumla ya Dola za Marekani 209,582,499 ambapo deni hili linatakiwa kulipwa pamoja na riba ya Dola za Marekani 138,031,674 kwa kipindi cha miaka 12 hadi 16. Kulingana na Mkataba (*PPA*) kati ya *TANESCO* na *Songas*; *Songas* wanawajibika kuingiza sehemu ya Malipo ya Mkopo (*Principal*) na Riba (*Interest*) kwenye gharama za *Capacity Charges* katika Ankara ya kila mwezi kwa *TANESCO*. *TANESCO* wanawajibika kulipa kiasi hicho kwa *Songas*, kisha *Songas* wanawajibika kuyapeleka malipo hayo Serikalini (Hazina) na rejea ipo katika ufafanuzi huu upo kwenye kifungu cha 4.2(d) cha *IDA Subsidiary Loan Agreement*, 2.6(d) cha *EIB On-Lending Agreement* na 2.5(d) cha *Loan Assumption Agreement*.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na tano (25), Kamati imebaini kuwepo kwa kasoro katika ulipaji wa kodi miongoni mwa Makampuni. Kamati inashauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) iongeze udhibiti katika ukusanyaji wa kodi, sekta ndogo ya gesi kwa kushirikiana na mamlaka na taasisi nyingine za Kiserikali na sekta husika. Serikali imepokea ushauri huu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) imeanza kufanya ukaguzi maalum wa *PSA* husika kuanzia Januari, 2012. Ukaguzi huu utaiwezesha kuondoa kasoro zote zitakazoonekana wakati wa ukaguzi. Mamlaka ya Mapato itaongeza udhibiti katika ukusanyaji wa kodi katika maeneo yote yatakayoonekana yana udhaifu.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba ishirini na sita (26), Azimio hili lilielekeza kwamba ili kulinda misitu na kupunguza gharama kwa wananchi, Kamati inashauri *TPDC* iwezeshwe ili kuweza kutekeleza miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari. Serikali imepokea ushauri wa Bunge.

Aidha, Serikali imeona umuhimu wa ushauri huu na tangu mwaka 2010/2011, ilianza kuiwezesha *TPDC* kwa kuiruhusu kubakiza asilimia hamsini (50% *retention*) ya mapato yatokanayo na mauzo ya gesi asili ili iwekeze katika miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa miradi hii, Serikali imeiruhusu *TPDC* kukopa fedha kwa riba nafuu Dola za Marekani milioni 55 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji gesi asili Dar es Salaam kwa nia ya kuokoa matumizi ya mkaa ambayo yanakadiriwa kwa mujibu wa taarifa tulizonazo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na vyanzo vingine ikiwemo Shirika la *TPDC* kuwa magunia 40,000 yanatumika kwa siku.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na shughuli za kila siku za Serikali ni matokeo ya uongozi wa pamoja na mshikamano mkubwa kati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake. Napenda kumshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Adam K.A. Malima kwa kunisaidia, kunishauri na pia kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Bwana Eliakim Maswi kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na hivyo kuiwezesha Wizara kuleta Taarifa hii ya Utekelezaji mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba tena niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa January Yusuf Makamba pamoja na

Mheshimiwa Daina Chilolo ambaye ni Makamu Mwenyekiti kwa ushauri wao wa kila siku na nia yao ya kutaka Wizara itekeleze wajibu wake na kutatua changamoto za Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa napenda kueleza kwamba hii taarifa aliyosoma Mheshimiwa Waziri iliwasilishwa hapa Bungeni na naamini mmegawiwa. Lipo li-*book* hapa. Katika kueleza maelezo ya Serikali ilikuwa inatoa azimio lilikuwaje na walivyotekeleza. Sasa nitakampomwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na yeye ametoa taarifa yake kwa maana ya Kamati ambayo walipata muda wa kupitia haya majibu ya Serikali. Kwa hiyo, ningependekeza Mwenyekiti atakaposoma asome Azimio na maoni ya Kamati ilikuwaje kuliko kurudia yale ambayo tayari Waziri ameeleza. Maana akisoma ile taarifa yake akisoma Azimio, anaeleza Serikali ilivyotekeleza, halafu anasema maoni ya Kamati. Tunachokosa sisi hapa ni maoni ya Kamati.

Kwa hiyo, naomba sana Mwenyekiti akifika atasoma Azimio namba moja hili, halafu atasoma na maoni ya Kamati katika Azimio hilo. Tukienda hivyo tutakuta tunaweza kumaliza kitabu chake chote hiki cha jinsi Kamati yake ilivyoshughulikia majibu ya Serikali. Namna walivyotekeleza ameshasema Waziri. Kwa hiyo, naomba Mwenyekiti ukifika ufanye hivyo, halafu wakija kuzungumza na Wabunge nao sasa hatufungui mjadala wa gesi. Tunapokea taarifa ambayo Kamati yetu ndogo ilitumia muda mwingi sana kuifanyia kazi ikawasilisha, Serikali ikasema naomba tupewe muda. Kwa hiyo, namwita Mwenyekiti aje awasilishe taarifa yake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (K.n.y. MHE. JANUARY Y. MAKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika ahsante. Naomba sasa nitoe maoni ya Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi nchini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya gesi nchini.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 18 Novemba, 2011, Kamati yangu iliwasilisha taarifa juu ya uendeshaji wa Sekta ndogo ya gesi nchini. Katika Taarifa hiyo Kamati ilitoa Maoni 26 ambayo Bunge lako Tukufu liliyapokea, likayaridhia na kuyaazimia.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuwasilisha Taarifa yake, Serikali ilitoa taarifa kuwa imeyapokea maazimio hayo na itayafanyia kazi na kuleta taarifa Bungeni katika Mkutano huu wa Sita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za utekelezaji wa maazimio. Kama ambavyo Waziri wa Nishati na Madini alivyowasilisha Taarifa yake ya utekelezaji wa maazimio. Napenda kutoa maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Azimio namba moja (1), Serikali hususan Wizara ya Nishati na Madini itambue kuwa pamoja na *TPDC* kuwa msimamizi wa Sekta ya gesi kwa niaba ya Serikali, lakini Wizara ya Nishati na Madini ndiye mdau mkuu katika Mikataba hii yenye utata kwa niaba ya Taifa na hivyo anapaswa kusimama sambamba na *TPDC* kutetea maslahi ya Taifa kwani Wizara ilikuwa haifanyi hivyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali. Serikali imepokea ushauri wa Bunge na tunaahidi Wizara itaendelea kusimama sambamba na *TPDC* kutetea maslahi ya Taifa na napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mahusiano ya Wizara na *TPDC* yameboreshwa. Pamoja na kuboresha mahusiano Serikali itaendelea kuelimisha wadau wengine ili waweze kuelewa umuhimu na shughuli za *TPDC* kwa maslahi ya Taifa.

Aidha, kufuatia kukua kwa kasi kwa matumizi ya gesi asili na ugunduzi wa hivi karibuni katika maeneo ya kina kirefu cha bahari, Serikali imeamua kuanzisha kitengo cha Uendelezaji Gesi Asili chini ya Idara ya Nishati ambapo moja ya majukumu yake ni kuhakikisha usimamizi wa karibu unakuwepo katika miradi yote inayohusisha uendelezaji na matumizi ya gesi asili. Kwa kufanya hivi tutahakikisha kuwa tija na ufanisi vinakuwepo katika miradi yote ikiwa ni pamoja na uzalishaji umeme, matumizi ya viwandani na

hata kwenye kilimo hapo baadaye pindi mipango ya uzalishaji wa mbolea kwa kutumia gesi itakapotekelezwa.

Pamoja na hatua zilizoelezwa hapo juu Serikali imechukua hatua zifuatazo kwenye sekta hii ili kuboresha zaidi utendaji wake:-

(a) Kuanzisha kitengo cha uendelezaji gesi asili mwaka wa fedha 2012/2013 ndani ya Wizara; na

(b) Serikali imetoa kibali kwa *TPDC* kuajiri watumishi 51 kwa mwaka 2011/2012 na kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2014/2015 wataajiriwa wafanyakazi wapatao 192.

Serikali imeanza utayarishaji wa mpango kabambe wa matumizi ya gesi asili (*Gas Master Plan*). Rasimu ya mpango huo itakamilika tarehe 30 Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa. Aidha, Kamati inashauri pamoja na kuanzisha kitengo cha kusimamia masuala ya kisera ya uendelezaji wa gesi asili, nguvu zaidi zielekezwe katika kuimarisha utendaji wa TPDC katika masuala ya gesi asilia kwa kupeleka wataalam na rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba mbili (2), Kamati imejiridhisha bila shaka kwamba kwa kipindi cha 2004 hadi 2009 Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imejirudishia isivyo halali gharama zinazofikia jumla ya dola za Kimarekani milioni 28.1 sawa na fedha za Kitanzania bilioni 46.3. Kutokana na kujirudishia fedha hizo isivyo halali kumefanya Serikali kukosa gawio lake linalofikia dola za Kimarekani milioni 20.1. Aidha, mpaka wakati Kamati inaandaa ripoti hii, Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT) imeshindwa* kuwasilisha uthibitisho wa uhalali wa kujirudishia gharama nyingine zinazofikia jumla ya dola za Kimarekani milioni 36. Hali hii inaonesha mashaka makubwa katika uendeshaji wa sekta hii muhimu ya gesi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali; Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kuanzia mwaka 2004 hadi kufikia 2009, *PAT* ilitoa taarifa *TPDC* kuwa imetumia kiasi cha Dola za Marekani 134,170,212. Aidha, katika gharama hizo, *PAT* walishajirudishia kiasi cha Dola za Marekani 79,846,171 na kubakiza Dola za Marekani 54,324,041 kufuatana na taratibu za *PSA*. Kuanzia Oktoba 2007, *TPDC* ilifanya ukaguzi wa gharama hizo na kubaini kuwa gharama za kiasi cha Dola za Marekani 64,496,756 ziliingizwa na *PAT* kwenye mahesabu kimakosa kwa misingi ya *PSA*. Tarehe 12 Julai 2011, *PAT* walikubali na kufikia makubaliano na *TPDC* kuwa kati ya gharama hizo, Dola za Marekani 28,053,680 ziliingizwa kimakosa katika mahesabu na kiasi kilichobaki Dola za Marekani 36,443,076 waliahidi kuzitolea maelezo.

Kwa kuwa Kampuni ya *PAT* haijatoa maelezo kuhusu kiasi kilichobaki cha Dola za Marekani 35,400,560 kati ya Dola za Marekani 36,443,076 walizokuwa wameahidi kutolea maelezo, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum ili kuhakiki kiasi hicho. Marejesho ya *PAT* kwa kipindi cha mwaka 2004 hadi 2009 ni Dola za Kimarekani milioni 79.85 kati ya Dola za Kimarekani milioni 134.17 hivyo kuwa na bakaa ya Dola za Marekani milioni 54.32. Kutokana na maamuzi ya kupeleka masuala yote ya *PAT* kwenye Kamati ya Majadiliano ya Serikali *(Government Negotiating Team – GNT)* iliyoundwa na Serikali ikijumuisha wataalam kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu na *TPDC*, suala hilo la madai ni moja kati ya Hadidu za Rejea zitakazoshughulikiwa na *GNT*.

Pamoja na kumwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakiki madai ya *PAT, TPDC* iliwapelekea *PAT Notice of Exception* ya tarehe 19/01/2012 (Kiambatisho Na. 2) kulingana na kifungu 1.7(b) cha *Annex* D ya *PSA*. Hii inafuatia *PAT* kueleza msimamo wao kupitia barua ya tarehe 26 Oktoba, 2011 (Kiambatisho Na. 2) wakijibu barua ya *TPDC* ya tarehe 24 Oktoba, 2011 (Kiambatisho Na. 2).

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imepokea taarifa ya hatua za Serikali. Aidha, Kamati inaitaka Serikali majukumu aliyopewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) na Kamati ya majadiliano ya Serikali (*GNT*) yakamilike na Bunge lipewe taarifa katika Mkutano wa Saba.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tatu (3), kwa kuzingatia kuwa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walifanya udanganyifu wa makusudi kwa kipindi cha 2004 hadi 2009 na kusababisha Serikali kukosa gawio lake inalostahili, Kamati inashauri mapunjo hayo ya Serikali yanayofikia dola za Kimarekani milioni 20.1 yarejeshwe mara moja na kwa kuwa mapunjo hayo ni ya muda mrefu, marejesho yake yaambatanishwe na riba kwa viwango vya benki *(Time Value for Money).* Aidha, upelelezi ufanyike katika hesabu za *PAT* kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu vifungu vifuatavyo:-

(i) Kifungu 350 kwa kosa la kuweka mahesabu yasiyo sahihi katika kitabu cha mahesabu;

(ii) Kifungu 315 kwa kosa la kughushi;

(iii) Kifungu 316 kwa kutoa taarifa za uongo; na

(iv) Kifungu 317 kwa kutoa taarifa za mahesabu za kughushi na ushahidi ukipatikana Kampuni ya *Pan African Energy* Tanzania *Limited* Wafanyakazi wote waliohusika katika udanganyifu huu washtakiwe kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kwa kuwa Kampuni ya *PAT* haijatoa maelezo kuhusu kiasi kilichobaki cha Dola za Marekani 35,400,560, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum ili kuhakiki madai hayo.

Kutokana na uamuzi wa Serikali kupeleka masuala yote ya *PAT* kwenye Kamati ya Majadiliano ya Serikali *(Government Negotiating Team (GNT),* suala la madai ni moja kati ya Hadidu za Rejea zitakazoshughulikiwa na *GNT*.

Matokeo ya uhakiki wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na yale ya majadiliano ya Kamati ya Majadiliano ya Serikali, yataiwezesha Serikali kuchukua hatua sitahiki kulingana na mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imepokea hatua za utekelezaji. Kamati inasisitiza kwamba, mapunjo ya Serikali yanayofikia dola za Kimarekani milioni 20.1 yarudishwe mara moja. Aidha, Serikali ichukue hatua za kufanya uchunguzi wa kijinai kama ilivyopendekezwa na Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Azimio namba nne (4). Kutokana na *Pan African Energy Tanzania (PAT*) kukosa sifa za uaminifu, Kamati inashauri Mkataba wa *Pan African Energy Tanzania (PAT)* usitishwe. Aidha, utekelezaji wa kuvunja mkataba huu uende sambamba na kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria na za kimkataba zinazingatiwa, uwepo wa usalama wa visima na mitambo na uwepo wa uhakika wa huduma ya upatikanaji wa gesi nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali, Serikali imepokea ushauri wa Bunge na itazingatia taratibu zote za kisheria na za kimkataba na itatafakari suala hili kwa umakini na kuzingatia athari za hatua hiyo katika upatikanaji wa gesi ya kutosha kwa ajili ya kulinda uchumi wa nchi yetu. Kwa mujibu wa mkataba wa *PSA* utaratibu ufuatao inabidi ufuatwe:-

(i) Chini ya *Annex D* ya mkataba wa *PSA,* kifungu cha 1.7(b), *TPDC* inatakiwa kutoa notisi ya siku 90 kuhusu masuala ya mahesabu na *PAT* anatakiwa kujibu hoja hizo ndani ya siku 90; na

(ii) Chini ya kifungu cha mkataba wa *PSA* cha 27.1, *TPDC* au *PAT* anaweza kutangaza mgogoro kwa kuwasilisha barua rasmi ya notisi ya kuwepo kwa mgogoro:-

(a) Ndani ya siku 30 ya kupokea notisi hiyo, *TPDC* au *PAT* wanatakiwa kujibu katika kutatua mgogoro huo kwa maelewano ikiwa ni pamoja na kujadili suala hilo katika vikao vya pamoja vya *Advisory Committee*;

(b) Kama mgogoro hautatatuliwa kwa maelewano, *TPDC* na *PAT* watawasilisha mgogoro huo kwa wakuu wa taasisi zao (*Chief Executives*). Iwapo wakuu hao watashindwa kufikia muafaka ndani ya siku 15 au muda zaidi kama watakavyoona inafaa, mgogoro huo unaweza

kuwasilishwa kwa Mtaalam Mwelekezi (*Technical expert*) kwa kuwa mgogoro wenyewe ni wa kitaalam. Kwa masuala yasiyo ya kitaalam kama ya uhasibu suala hilo linaweza kuwasilishwa Baraza la Usuluhishi (*Arbitration);* na

(c) Baraza la Usuluhishi litatumia taratibu za kuendesha mashauri chini ya *International Centre for Settlement of Investment Disputes-ICSID*. Aidha, Baraza hilo litakaa mjini London na litatumia Sheria za Tanzania katika kutatua mgogoro huo.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, Serikali imeamua hatua zifuatazo kuchukuliwa:-

(i) Kutafakari athari hasi ambazo zinaweza kujitokeza kama mgogoro ungetangazwa mara moja ambazo zinaweza kuwa pamoja na kusimamisha shughuli za uzalishaji gesi, uendelezaji wa uchimbaji visima vipya na mazungumzo kati ya Serikali na wawekezaji wengine kwenye miradi mipya.

(ii) Ili kuimarisha uhakiki uliokwishafanywa na *TPDC*, Serikali imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum *(Special Audit)* wa gharama ambazo *PAT* bado hawajazitolea maelezo ya kuridhisha.

(iii) Serikali imeunda Kamati ya Majadiliano itakayotoa mwelekeo wa kufuata juu ya suala hili kwa kuzingatia athari zake. Kamati hiyo itaanza kazi tarehe 20 Februari 2012 na kuwasilisha ripoti ya majadiliano na *PAT* mwishoni mwa mwezi wa Machi 2012. Kamati hiyo itatoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu hatua za kuchukua na maoni ya majibu ya *Letter of Exception*.

(iv) Serikali imetengeneza Hadidu za Rejea ambazo zinagusa masuala yote yanayohusiana na tofauti baina ya Serikali na *PAT*.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, pamoja na maelezo ya Serikali, Kamati inasisitiza taarifa ya utekelezaji wa azimio hili iletwe Bungeni. Aidha, Kamati inashauri Serikali izipitie upya hadidu za rejea na maeneo yote ambayo taarifa ya Kamati ilionesha mashaka yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba tano (5), Kamati inashauri utaratibu wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kujirejeshea gharama za usambazaji chini ya muundo wa *PSA* usitishwe mara moja. Aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya gesi asili katika matumizi ya viwandani na majumbani, jitihada za uhamishaji wa matumizi hayo ziongezeke na gharama za usambazaji zirejeshwe kwa kutumia *tarrif* za bei.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali, pamoja na maelekezo mazuri ya Bunge, Serikali iliishatoa maelekezo kuhusu utenganishaji wa gharama ili kutekeleza ushauri kutoka kwa Mshauri Mwelekezi, *BEICIP Franlab*. Aidha, Wizara iliiagiza *TPDC* na *PAT* kutekeleza ushauri wa *BEICIP Franlab* kuanzia tarehe 1 Januari, 2010 na kuhakikisha kuwa gharama za usambazaji wa gesi zinatokana na *tariff* ya usambazaji wa gesi. Aidha, katika ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2010 uliofanywa na *TPDC* umethibitisha kuwa gharama hizo zimeondolewa kwenye *PSA*.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa azimio hili. Aidha, tunashauri mpango wa kuanzisha Kampuni ya usambazaji gesi nchini utekelezwe kama ulivyopangwa bila kuahirisha.

Mheshimiwa Spika, Azimio namba sita (6), Serikali kama msimamizi wa mikataba inayo haki ya kukagua gharama za mwekezaji. Mikataba yote ya *PSA* ina vipengele vinavyoipa uwezo huo Serikali au msimamizi wa Mkataba kwa kutambua uwiano wa mgao wa Serikali na usahihi au uhalali wa gharama za mwekezaji. Katika PSA ya Songosongo haki hiyo ya kukagua gharama za *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT*) imepewa *TPDC* kwa mujibu wa kifungu 21.2. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa Serikali imezembea kusimamia suala hili na hivyo kutoa fursa kwa mwekezaji kudanganya na kujilipa fedha nyingi za walipa kodi wa Tanzania kinyume na taratibu za Mkataba. Kamati inapendekeza mapungufu haya yarekebishwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali, katikati ya miaka ya 90 Serikali ilisimamisha ajira kwa Wizara na Taasisi zake ikiwamo *TPDC*. Hivyo, kutokana na mabadiliko ya kisera yalisababisha *TPDC* kupunguza wafanyakazi kutoka 440 hadi 63 tu. Idadi ndogo ya wafanyakazi waliokuwepo Wizarani na *TPDC* wakati wa uendelezaji wa mradi wa Songosongo ilisababisha shughuli za usimamizi na uendelezaji gesi kukosa ukaguzi wa mara kwa mara kama mikataba inavyohitaji. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2006, *TPDC* ilianza kuajiri wataalam mbalimbali wakiwemo wajiolojia, wahandisi, wanasheria na wahasibu. Hadi sasa *TPDC* imeajiri wafanyakazi 45 wa fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara kwa kutambua umuhimu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na tatizo la upungufu wa wafanyakazi *TPDC*, mwaka 2010 Wizara iliiazima *TPDC* wataalam watatu ili wasaidie katika ukaguzi wa hesabu za *PSA* mbalimbali zinazosimamiwa na *TPDC*;

(ii) Serikali imetoa kibali kwa *TPDC* kuajiri watumishi 51 kwa mwaka huu wa fedha na mchakato wa ajira utaanza mara baada ya kumaliza Mkutano huu wa Sita wa Bunge; na

(iii) Kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 mpaka 2014/2015, *TPDC* wataajiri wafanyakazi 192 wanaohitajika kwa awamu. Kwa kuanzia tayari Serikali imetoa kibali cha *TPDC* kuajiri wafanyakazi 51.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji. Kamati inasisitiza wafanyakazi 51 wanaotarajiwa kupatikana, Kitengo cha Ukaguzi kipewe kipaumbele. Aidha, kwa sekta hii na sekta nyinginezo, Serikali ijenge utamaduni wa kutofautisha haja na umuhimu wa watumishi kati ya sekta moja na nyingine kabla ya kutoa maamuzi ya kusitisha ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Azimio namba saba (7), kwa mujibu wa mkataba wa gesi (kiambatisho E, Aya ya 13), "Katika kipindi ambacho gesi itakuwa imekwisha (*depleted*), basi mapato yatokanayo na mauzo ya mabaki ya mitambo ya gesi yatatumika kulipia gharama za kurejesha au kutunza mazingira ya eneo la uchimbaji wa gesi katika hali iliyo salama". Kamati haipendezwi na utaratibu huo na inaishauri Serikali kupitia *TPDC* kutafuta utaratibu mzuri utakaokubalika kisheria ambapo Kampuni ya *SONGAS* itawabidi watenge fungu la pesa la kugharamia urejeshaji au utunzaji wa mazingira wa maeneo ya uchimbaji wa gesi pindi gesi itakapokuwa inakaribia kwisha. Aidha, Serikali isikubaliane na vipengele kama hivi mara nyingi wawekezaji hawa huondoka kama sio kutoroka baada ya kumaliza uchimbaji wa migodi au vitalu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Serikali, kwenye mikataba (*PSA*) yote ya sasa na ya miaka ya hivi karibuni, kuna kifungu kinachoelekeza kuwa Serikali, *TPDC* na Mwekezaji (*Contractor*) kwa pamoja wataanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kuhifadhi mazingira ya maeneo ya uchimbaji wa mafuta au gesi mara mafuta au gesi inapokwisha na visima kufungwa (*Abandonment Fund)*. Serikali imepokea ushauri huu na itahakikisha Mfuko huu unaanza ili kuhifadhi maeneo ya uchimbaji wa mafuta au gesi. Suala hilo lipo katika Hadidu za Rejea zitakazofanyiwa kazi na Kamati ya Majadiliano.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, Kamati imezingatia kauli ya Serikali ya kupokea ushauri. Aidha, tunaitaka Serikali itoe taarifa juu ya majadiliano ya kuanzisha Mfuko husika na ratiba ya utekelezaji wake katika Mkutano wa saba wa Bunge.

Mheshimwa Spika, Azimio Na. 8 - Mkataba wa *PSA*, kifungu cha 10.4 na 10.5 vimetoa utaratibu wa namna ya kugawana mgao unaotokana na faida ya gesi iliyopatikana kutoka eneo lenye gesi iliyothibitishwa *(proven gas)* na gesi isiyothibitishwa *(unproven gas)*. Mgao huu utabadilika kwa mujibu wa ushiriki *(participation)* wa *TPDC*.

Aidha, kwa kuwa gesi ya ziada inaweza kuzalishwa kutoka katika eneo ambalo gesi imethibitishwa au ambalo gesi haijathibitishwa na *Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* wana haki ya kupata sehemu ya mapato yatokanayo na mauzo ya gesi ya ziada *(additional gas)*. Kamati inaona kuwa siyo sahihi kuendelea na utaratibu huu, kwani kwa kufanya hivyo ni kumlipa *Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* mara mbili *(double payment)* ya kile anachostahili kwa kuwa *Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* inanufaika kwanza na marejesho ya utafutaji wa gesi kwenye visima ambavyo tayari vilikuwa vimeshathibitishwa na *TPDC* kuwa na gesi na pili anagawana mapato na *TPDC*.

Kamati inasisitiza utaratibu huu wa ugawanaji wa mapato katika mazingira haya unahitaji kuangaliwa upya kwa kuwa hapo awali *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* alipewa unafuu huu kwa kutegemea kuwa angetafuta na kuendeleza vitalu tisa vya gesi na siyo viwili kama ilivyo sasa kwenye eneo lile lile la uzalishaji tofauti na alivyotakiwa kufanya kwa mujibu wa *PSA*. Kamati inashauri mkataba kufanyiwa marejeo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Utaratibu wa kugawana mapato kama ulivyoainishwa katika vifungu vya 10.4 na 10.5 vya *PSA* ulilenga kuwa vitalu vyote tisa vingeendelezwa. Kwa vile *PAT* iliachia vitalu saba, mazungumzo yameanza juu ya mkataba husika ikiwa ni pamoja na kurekebisha utaratibu wa kugawana mapato.

Aidha, mazungumzo ya mwisho baina ya Serikali, *TPDC* na *PAT* yalifanyika kati ya tarehe 14-15 Aprili 2011. Katika Mkutano huo, iliundwa timu ya watalaamu *(Task Force)* kutoka *TPDC* na *PAT* ili kupitia mikataba na kushauri jinsi ya kugawana mapato na mambo mengine ikiwemo utaratibu wa ulipaji kodi, ushiriki wa *TPDC (participation)* katika mradi, utozaji wa mrabaha n.k. Kikao cha kwanza cha *Task Force* kilifanyika tarehe 25 Mei, 2011 na kuandaa mapendekezo yanayotakiwa kufanyiwa kazi. Aidha, mwezi Januari, 2012, Serikali imeunda *Government Negotation Team* yenye Wajumbe toka Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, *TRA, TPDC* na Wizara ya Nishati na Madini kuendelea na kazi hiyo.

Kamati hiyo itaanza kazi tarehe 20 Februari, 2012 na kuwasilisha ripoti ya majadiliano na *PAT* mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2012. Ripoti itajumuisha mapendekezo ya Kamati kwa Serikali kuhusu hatua za kuchukua. Aidha, mapendekezo ya *Task Force* yamejumuishwa kwenye hadidu za rejea za Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(GNT)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji. Aidha, maoni ya Kamati ni kwamba, tunaishauri Serikali kusisitiza kwa wabia wake pale wanapoingia katika mikataba kuwa kinacholengwa ni mafanikio ya pande zote na siyo ujanja wa upande mmoja kuumiza upande mwingine pale vifungu vya mikataba vinapokuwa na utata. Kama tulivyoshauri awali, majadiliano ya kuleta ufumbuzi yaharakishwe, na Bunge lipewe taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 9, Kamati imegundua kuwa, kwa sasa masuala ya sekta ya gesi nchini yanasimamiwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta ya Mwaka 1980 *(The Petroleum Exploration and Production Act, 1980)* na mikataba ya uzalishaji na ugawanaji *(PSA)* ambayo inatoa mwanya kwa wawekezaji kujipatia faida kubwa kuliko anavyostahili. Kamati imebaini kwamba kutokuwepo kwa Sheria ya gesi kumefanya sekta ya gesi ikose mwongozo na usimamizi wa kutosha na hivyo wadau kutojua mwelekeo na imeathiri mahusiano ya wadau kwa jinsi yanavyopaswa kuwa. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa Sheria ya gesi ili kuhakikisha rasilimali hii muhimu inatumika kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri wa Bunge. Rasimu ya Sheria ya Gesi Asili imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kufanya maandalizi ya Muswada wa Sheria. Muswada huo utawasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge hili. Aidha, Rasimu ya Muswada umezingatia mabadiliko ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ya Kamati, Kamati imepokea maelezo ya Serikali. Kwa kuwa Sekta ya gesi imekuwa ikikua kwa kasi sana na hivyo kuhitaji uwepo wa sheria hii ili kuweza kuisimamia ipasavyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba Sheria ya Gesi Asili inawasilishwa na kupitishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge. Aidha, Kwa kuwa msingi wa sheria ni sera na kwa kuwa sera ya sasa ya nishati haikidhi mahitaji ya sekta ndogo ya gesi asili, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa upatikanaji wa sera ya gesi asili.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 10 - Utaratibu wa umiliki wa mitambo na mali nyingine baada ya muda wa Mkataba kwisha, umefafanuliwa vizuri katika kipengele cha 17 cha *PSA* ikiwemo mali zisizohamishika na zinazohamishika. Aidha, Kamati haikubaliani na kifungu cha 17.3 cha *PSA*. *TPDC* wana haki ya kununua chochote kilichoagizwa na *PAT* kutoka nje ya nchi na ambacho hakijalipiwa kodi kwa bei ya kibiashara, isipokuwa kwa vifaa vilivyoainishwa kwenye vipengele 17.1 (a) na 17.1 (b) vya *PSA*.

Kwa kawaida, katika *PSA* yoyote ile, mitambo na mashine zote (ikiwa ni pamoja na mitambo na mabomba ya gesi) zilizonunuliwa kwa ajili ya shughuli za kutafuta na kuendeleza gesi/mafuta chini ya *PSA*, zinatakiwa kuwa mali ya Serikali au Shirika la Mafuta, na kwa sababu hii ndiyo maana huwa hailipiwi kodi. Uhamishaji wa haki za umiliki wa mali hufanyika aidha baada ya Kampuni ya kimataifa kurejesha gharama zake za kununulia mitambo na kuifunga au mwisho wa uzalishaji. Kwa mantiki hii, Kamati haioni sababu ya kuwepo kwa kifungu hiki cha 17.3 cha *PSA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Lengo la kifungu cha 17.3 ni kutoa vigezo vya kufikia bei ya ununuzi ikizingatia uchakavu *(Depreciation),* kurudisha gharama *(cost recovery)* na misamaha ya kodi (*tax exemption*) kwenye vifaa hivyo kabla ya kufikia bei ya makubaliano. Katika kufikia bei ya kununua vifaa, ushauri wa Bunge utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kwamba, Kamati inakubaliana na tafsiri ya Serikali ya kifungu na. 17.3 cha *PSA*. Aidha, tunasisitiza kuwa taarifa hiyo iwe ndiyo tafsiri halisi panapojitokeza vifaa vilivyotumika katika shughuli za gesi vinauzwa kwa *TPDC*.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 11, msingi mkuu wa mkataba wa uzalishaji na ugawanaji *(PSA)* ni kwamba mwekezaji anaingia kwanza kuzalisha na baadaye kugawana na Serikali kulingana na mapato yaliyopatikana. Lakini mkataba huu mwekezaji amekuta uwekezaji umeshafanyika kwa maana ya visima tayari vimechimbwa na hivyo kukosekana uhalali wa mwekezaji kuwa mbia katika mikataba ya gesi. Pamoja na hoja za utetezi zinazoegemea mazingira ya wakati huo, Kamati inashauri kipengele hiki kiangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Bunge umepokelewa na hatua zimeanza kuchukuliwa. Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(GNT)* ambayo imeundwa itafanya pamoja na mambo mengine, kudurusu upya baadhi ya vipengele vya mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa maazimio mengine ambayo ufumbuzi wake unahusisha Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(Government Negotiating Team – GNT)* Kamati inahimiza uharakishaji wa upatikanaji wa ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 12, Mikataba ya Mradi wa Gesi iliyojadiliwa na kukubaliwa na kusainiwa na Serikali pamoja na *SONGAS* ilikuwa 18. Mikataba hii ina vipengele tata na vya makusudi vyenye maana zaidi ya moja ambavyo vingine vinatafsiriwa tofauti na wadau husika. Ipo haja kwa Serikali yetu kufanya tathmini ya kina *(Due Diligence)* kabla ya kuingia mkataba na wawekezaji. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeonyesha kutokuwa makini katika kupitia, kujadili na kusimamia mikataba kama hii inayoingia kwa niaba ya Serikali na hatimaye Serikali imekuwa ikiingia hasara kubwa katika sekta hii ya nishati, na wawekezaji wamekuwa wakineemeka kwa kunyonya rasilimali ya Watanzania ambao wengi wao ni maskini. Hali hii inaashiria kuwa imefika wakati kwa Serikali kuwachukulia hatua kali Watendaji wote wanaochangia hasara kubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Itakumbukwa kuwa, maandalizi ya mradi wa Songo Songo yalianza mwaka 1994 ambapo ilikuwa vigumu kupata mwekezaji. Hali hii ilisababisha kuwepo na mikataba mingi ambayo pamoja na mambo mengine mwekezaji kuwa na uhakika wa uwekezaji alioufanya. Tangu utekelezaji wa mradi ulipoanza, mazingira ya uwekezaji yamekuwa yakiimarika na hivyo kusababisha kufanyika durusu za mara kwa mara za mikataba pindi inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mikataba ya Songo Songo imedurusiwa mara tatu, yaani 2001, 2004, 2008 ambapo baadhi ya mikataba kama ya *ESCROW* imefutwa. Majadiliano yanaendelea kati ya wadau wote (Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *TPDC, TANESCO, SONGAS* na *PAT*) kupitia upya mikataba ya mradi na kufanya marekebisho yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepokea maelekezo ya Bunge na itaendelea kuisaidia Wizara na *TPDC* kwa kuchambua na kusimamia mikataba kati ya Serikali na Wawekezaji kwa maslahi ya Taifa. Aidha, pale ambapo Serikali itabaini utendaji mbovu au uzembe umesababisha hasara, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote waliohusika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa azimio hili. Aidha, Kamati inatarajia kupokea kutoka kwa Serikali taarifa ya matokeo ya majadiliano yanayoendelea juu ya azimio hili. Ni matumaini ya Kamati kuwa mikataba inayofuata itaboreshwa zaidi kwa maslahi ya Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 13, Kamati imejiridhisha ya kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumishi wenye utaalamu wa kisekta kuanzia ngazi ya Wizara, Taasisi zake na hata kwenye jamii na hakuna mfumo endelevu unaohakikisha nchi inakuwa na wataalamu wanaohitajika *(succession plan)* katika Sekta za nishati na gesi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama msimamizi wa kutoa vibali vya ajira nchini kupitia Ofisi yake ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kufanya utafiti na tathmini ya ajira zinazoombwa ambazo vibali vyake vinatakiwa kutoka haraka ili maslahi ya Taifa yalindwe, mathalan, wataalamu wa kijiolojia ya miamba. Kamati inaamini kuwa dola za kimarekani milioni 64 zilizoripotiwa kwenye ukaguzi wa *TPDC* zisingetokea kama kibali cha kuajiri Wakaguzi wa Ndani wa mahesabu wa *TPDC* kingetolewa mapema.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kwa kuzingatia kasi ya ukuaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Asili, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo pamoja na wadau wengine kama vile makampuni ya utafutaji mafuta inakamilisha majadiliano ya kutekeleza miradi ya kujenga uwezo *(Capacity building)* kwa Serikali na taasisi zake. Lengo la mkakati huu ni kuongeza uwezo wa kuendeleza na kusimamia sekta ndogo ya gesi asili. Kama ilivyoelezwa awali, Serikali imetoa kibali kwa *TPDC* kuajiri watumishi 51 kwa mwaka huu na kibali kimezingatia uharaka wa watumishi wanaohitajika. Kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 mpaka 2014/2015, *TPDC* wataajiri wafanyakazi 192 wanaohitajika kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *succession plan* kwa upande wa *TPDC*, Serikali imeiagiza *TPDC* kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba kuna mpango thabiti wa kuachiana madaraka pamoja na kuajiri watumishi wapya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni maoni ya Kamati. Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji. Kamati inasisitiza wafanyakazi 51 wanaotarajiwa kupatikana, Kitengo cha Ukaguzi kipewe kipaumbele. Aidha, kwa sekta hii na sekta nyinginezo Serikali ijenge utamaduni wa kutofautisha haja na umuhimu wa watumishi kati ya sekta moja na nyingine kabla ya kutoa maamuzi ya kusitisha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 14, Kamati imeridhika kuwa kuna uhusiano mbaya kati ya *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* ukizingatia kuwa mahusiano yao ni ya kimkataba na kila upande unao wajibu na haki ndani ya mkataba *(PSA)*. Mfano mzuri ni kuwa *Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* amekuwa akikiuka baadhi ya vipengele vya mkataba wa uzalishaji na ugawanaji *(PSA)*.

*Pan African Energy Tanzania Ltd. (PAT)* chini ya Ibara ya 24.4, anapaswa kufuata sheria zote za Tanzania, *Pan African Energy Tanzania (PAT)* amevunja Ibara ya 21.1 ya *PSA* kwa kitendo chake cha kutotunza taarifa au nyaraka za mahesabu yake ya uhasibu kwa mujibu wa taratibu za kihasibu zilizokubaliwa Tanzania. Aidha, *Pan African Energy Tanzania Ltd.* imekuwa haiishirikishi *TPDC* katika kufanya manunuzi kinyume na taratibu. Mifano hii michache inaashiria uwepo wa uhusiano mbaya unaofanywa na *Pan African energy Tanzania Ltd. (PAT)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Hata hivyo, Serikali inakiri kuwepo kwa mawasiliano yasiyoridhisha kati ya *PAT* na *TPDC*. Kwa kuzingatia hali hiyo, Wizara ya Nishati na Madini ilichukua hatua zifuatazo:-

- Kuwakutanisha wahusika na kujadili masuala yote yaliyoonekana kuwa na utata; na

- Kuandaa utaratibu wa manunuzi kwa kushirikiana *TPDC* na *PAT*, na utaratibu huu umeanza kutumika kuanzia mwaka 2011.

Aidha, mwaka 2010, Kampuni ya *PAT* ililazimika kubadilisha mfumo wa uongozi ikiwa ni pamoja na kumbadilisha Meneja Mkuu aliyekuwepo Tanzania wakati wa matatizo hayo. Kamati ya Serikali ya Majadiliano iliyoundwa itashughulikia vile vile kuimarisha uhusiano kati ya *TPDC* na *PAT*.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba baada ya kupata taarifa ya utekezaji ya Serikali, Kamati imepokea kauli ya Serikali juu ya hatua zilizochukuliwa. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa mahusiano ya wabia hawa ambao kwa pamoja wanafanya kazi muhimu na nyeti kwa maslahi ya Taifa yasiishie kwenye maandishi na mikataba bali yaende zaidi mpaka kwenye utendaji na mawasiliano ya siku kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 15, *TANESCO* amelalamika kuwa *Pan African energy Tanzania Ltd. (PAT)* amekuwa akikwepa adhabu pale inapotokea hitilafu kwenye visima vya gesi na mitambo ya kusafisha gesi na hivyo kutupiana mpira na *Songas* na hii inatokana na *Pan African energy Tanzania Ltd. (PAT)* kuwa mwendeshaji tu wa visima na mitambo hiyo na siyo mmiliki. Kamati imeridhika kuwa mahusiano ya mbia huyu siyo mazuri na hivyo Serikali iangalie Mkataba wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kwa kutambua kuwepo kwa hali hii, Serikali imewakutanisha *TANESCO* na *PAT* ambapo maofisa wa taasisi hizi walipitia kwa karibu mfumo mzima wa uzalishaji na usafirishaji wa gesi na kukubaliana njia bora ya kubadilishana taarifa ili kupunguza malalamiko. Kutokana na maagizo ya Bunge, Serikali imeagiza *PAT* kutoa taarifa za uzalishaji na usambazaji gesi kwa Wizara, *TPDC* na *TANESCO* kila siku, na agizo hili linatekelezwa. Tangu hatua hii ichukuliwe, uhusiano na utendaji kazi wa taasisi hizi mbili umeimarika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya Serikali ya utekelezaji, haya ni maoni ya Kamati. Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji wa azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 16 katika Sekta ya gesi, lipo tatizo kubwa la baadhi ya visima kuharibika (SS 5, 7 na 9). Hata hivyo, Kamati inashangazwa na uharaka wa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* kukimbilia kuchimba kisima kingine SSA badala ya kuokoa visima vya awali ambavyo tunahakika vina gesi nyingi. Zaidi ya hapo, zipo taarifa kuwa *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* wanalenga kuchimba kisima kipya SSA ambacho watatumia mtambo wa kuchimbia *(drill rig CARROL 6)* ambao umeaminika kuwa ni wa gharama kubwa na haufai kutumika kwa mazingira ya nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za ziada kuhakikisha visima vilivyoharibika vinaokolewa ili viendelee kuzalisha kama ilivyo kawaida. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa mitambo inayotumika katika kuchimba gesi na mafuta haitaingiza Taifa katika gharama kubwa na ambayo ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kazi ya kukarabati visima namba SS 5, SS 7 na SS 9 vilivyoathiriwa na kutu kali itafanyika baada ya kuchimba kisima namba SSA. Hatua hii imechukuliwa kwa vile kazi ya kukarabati visima hivyo vitatu inaweza kuchukua muda mrefu (visima hivi vilichimbwa mwaka 1974) na kusababisha kukosekana kwa gesi ambayo inahitajika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani. Uamuzi wa kuharakisha uchimbaji wa SSA badala ya kukarabati visima vyenye kutu unatokana na sababu zifuatazo:-

- Kitaalam, hali ya visima vyenye kutu kwa sasa haitabiriki. Inaweza kuchukua muda mrefu kufikia uamuzi wa kuvikarabati au ikashindikana kuvikarabati na kulazimika kuviziba hivyo kuathiri kiwango cha upatikanaji wa gesi kwa mitambo ya umeme; na

- Kuchimba visima vipya kwanza kabla ya ukarabati, kunatoa uhakika kuwa gesi asili ya kutosha inapatikana haraka kwa matumizi ya mitambo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kisima cha SSA kinachimbwa kisiwani Songo Songo ambacho kinakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha futi za ujazo milioni 60 kwa siku. Aidha, *PAT* pia itakarabati kisima SS 10 ambapo uwezo wake wa kuzalisha utaongezeka kutoka futi za ujazo milioni 50 kwa siku hadi kufikia milioni 60 kwa siku. Visima hivi pamoja na visima SS 3 na SS 4 kwa pamoja vitaweza kuzalisha gesi ya kutosha kwa mahitaji ya kuzalisha umeme na viwandani. Baada ya kuwa na gesi ya uhakika na ya kutosha ndipo ukarabati wa visima SS 5, SS 7 na SS 9 utafanyika.

Serikali inatambua umuhimu wa kuchimba kisima SS A kutumia mtambo unaoitwa *SAKSON PR5* ambao una uwezo mkubwa zaidi kuliko *CAROIL* 6 na ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni Maoni ya Kamati. Kwa maelezo ya Serikali kuwa utekelezaji wa azimio hili umezingatia mahitaji ya gesi na uchimbaji umezingatia ushauri wa kitaalam, tumeridhika na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 17, misingi ya hoja walizokuwa wanatoa *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* za kurudisha gharama walizotumia isivyo halali yafanyike kwenye gharama zilizobaki na ambazo zitadaiwa, na kurudishwa miaka inayofuata ni batili na ni sawa na kufanya marekebisho kwenye "*cost pool*". Hoja hii ikikubaliwa na Serikali itakiuka misingi ya *PSA* ya kuwa mwekezaji atumie fedha zake kwanza kabla ya kurudishiwa gharama zake. Kamati inasisitiza *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* izilipe fedha hizi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea maoni ya Bunge. Taratibu za mkataba zitafuatwa na *TPDC* imeagizwa kuhakikisha suala hili linafuatiliwa na litamalizika haraka iwezekanavyo. Suala hili pia litafanyiwa kazi na Kamati ya Serikali ya Majadiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni Maoni ya Kamati. Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji wa azimio hili. Aidha, tunaendelea kusisitiza kuwa vyombo vilivyopewa jukumu la kufuatilia fedha hizi vizingatie vipengele vya Mkataba na viwasilishe taarifa ya utekelezaji wake Bungeni ili maelekezo yapasayo yatolewe. Tunalenga kutoa maelekezo zaidi baada ya kupata taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 18, katika hali ya kusikitisha na kuvunja moyo, Kamati imejiridhisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa haitoi ushirikiano wa kutosha kwa *TPDC* na *EWURA* hasa katika kusimamia masuala ya sekta ya gesi nchini. Vitendo vya ukiukwaji wa taratibu, udanganyifu na uhalifu vinavyofanywa na *SONGAS* na *PAT* kwa lengo la kuibia nchi hii vinaendelea kulelewa na havijakemewa na Wizara ya Nishati na Madini ipasavyo.

Imedhihirika kuwa mara kwa mara Wizara imekuwa ikiwasaidia wawekezaji hawa katika mipango yao ya kufanya udanganyifu; mfano ni pale Wizara ilipofanya jitihada za makusudi kuilazimisha *EWURA* kupitisha maombi ya bei *(tarrif)* ya Songas ambayo hapo awali *EWURA* waliyakataa kwa kuwa yalikuwa na upungufu uliokinzana na maslahi ya nchi. Zaidi ya hilo, Wizara ya Nishati na Madini iliandikia *EWURA* barua ikielezea kuwa *EWURA* wamevunja sheria. Jambo la kusikitisha ni kwamba, Wizara ilitoa nakala ya barua hiyo kwa Songas ambao nao waliitumia barua hiyo kama kielelezo katika shauri lao walilofungua kwenye Baraza la Ushindani huru *(Fair Competition Tribunal)* dhidi ya *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa Wizara katika kusimamia Sekta ya gesi kama ilivyoelezwa awali, Kamati inashauri Serikali kupitia upya mfumo wa utendaji wa Wizara utakaohakikisha maslahi ya Taifa yanazingatiwa. Ni dhahiri uzoefu wa mgongano wa *EWURA* na Wizara unaonyesha hatari inayoikabili sekta ya gesi. Aidha, kutokana na udhaifu mkubwa wa kiutendaji ambayo yameelezwa hapo awali. Kamati inaishauri Serikali kuwawajibisha viongozi wakuu na watendaji waliohusika na uzembe huu na kuteua wengine wenye uwezo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Kukosekana kwa sera mahsusi, Sheria na Mpango Kabambe *(Gas Master Plan)* wa gesi asili kunatoa mwanya kwa baadhi ya wadau wa sekta wenye nia mbaya kugonganisha Serikali na Taasisi zake na mara nyingine kwa maslahi yao. Hivi karibuni tumeshuhudia jinsi Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ulivyopigwa vita na baadhi ya wadau wakidai kuwa mradi huo hauna manufaa ya kiuchumi. Wizara inajivunia kuwa na taasisi imara za *TPDC* na *EWURA* ambazo zimekuwa zikitoa ushauri Serikalini kuhusu hatua muhimu za kuchukua ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Gesi Asili inaimarika kwa maslahi ya wadau wote.

Pia, hali ya kutoshirikiana iliyokuwepo hapo nyuma kati ya Wizara na *EWURA* imerekebishwa ambapo ushirikiano kati ya Wizara na taasisi za *TPDC* na *EWURA* umezidi kuimarika katika kusimamia masuala ya uendelezaji wa gesi asili nchini ili kuhakikisha kwamba rasilimali hii ya gesi asili inaendelezwa na maslahi ya nchi yanalindwa. Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi zote husika ili kuhakikisha kuwa sekta hii inaendelezwa vizuri kwa maslahi ya nchi kwa kuzingatia matakwa na Sheria za Taasisi husika. Pia tunatarajia kwamba kuwepo kwa Sheria ya Gesi Asili kutachochea maendeleo katika sekta ya gesi asili kwa kuwa Sheria hiyo itaeleza kwa uwazi majukumu ya Wizara na Taasisi zinazosimamia sekta ya gesi asili. Sheria hiyo itawasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa ya Serikali ya utekelezaji, Maoni ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

Kamati pamoja na kuridhishwa na utekelezwaji wa azimio hili, inaipongeza Serikali kwa kuongeza kasi ya kusimamia sekta hii muhimu na nyeti kwa mustakabali wa Taifa letu. Naomba nirudie.

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na kuridhishwa na utekelezwaji wa azimio hili, inaipongeza Serikali kwa kuongeza kasi ya kusimamia sekta hii muhimu na nyeti kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 19; pamoja na jukumu la kufuatilia rasilimali za Taifa (dola milioni 64), Kamati imebaini kuwa ulikuwepo uzembe uliopelekea visima namba 5, 9, kuharibika *(Corrossion)*. Matatizo ya kuharibika kwa visima yangeweza kutambulika mapema na kurekebishwa kama *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* angezingatia maelekezo ya mkataba (*Gas Agreement* kifungu cha 7.6 (e))kitendo ambacho hakufanya.

Mbali ya hasara ya kupoteza visima hivyo, uendeshaji shughuli wa aina hii unaliweka Taifa katika hatari ya kukosa nishati hii muhimu katika kipindi ambacho gesi asili inategemewa katika kuzalisha umeme. Hivyo basi, Kamati inapendekeza:-

- Vipengele vya utunzaji wa visima vilivyopo kwenye mkataba vizingatiwe na Kampuni inayohusika kuharibika kwa visima hivyo, iwajibike kwa kuvikarabati visima hivyo kwa gharama zake.

- Serikali na wasimamizi wa sekta ya gesi wahakikishe kuwa utunzaji, ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ya visima yanafuatwa ili isije kutokea visima hivyo vinaharibika ghafla na kuhatarisha usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Baada ya kugundulika matatizo ya kuwepo kwa kutu katika visima vya gesi vya SS5, SS7 na SS9 mwishoni mwa mwaka 2010, Wizara ya Nishati na Madini iliiagiza *TPDC, PAT* pamoja na *Songas* kufanya tathmini ya uwezo wa visima hivyo pamoja na kuandaa mpango wa kuvikarabati.

Hatua za haraka zilizochukuliwa ili kuhakikisha kunakuwepo gesi ya kutosha ni kuchimba kisima cha SSA na kukarabati kisima cha SS10. Maelezo kuhusu mpango huu, yapo kwenye jibu la Azimio Na. 16.

Kuhusu nani awajibike na uharibifu wa visima SS 5, SS 7 na SS 9, Serikali imeliweka kama mojawapo ya hadidu za rejea za Kamati ya Serikali ya Majadiliano ili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na kuafiki haja ya kutumia kwanza Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(Government Negotiating Team - GNT)* katika kupata ufumbuzi, tunashauri tena masuala ambayo yako bayana katika mikataba yawekwe wazi katika hadidu za rejea *(Terms of Reference)*. Mfano, asasi iliyokabidhiwa kulinda na kutunza visima haijulikani? *PSA* inatoa maelekezo gani katika utunzaji wa visima? Je, maelekezo hayo yalifuatwa?

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 20, Kamati imeona kuwa uwepo wa Kampuni moja ya *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* ya usambazaji wa gesi kutoka maeneo ya uzalishaji kunawanyima fursa wawekezaji wengine na hivyo kusababisha migongano ya kibiashara pamoja na bei ya gesi kutokuwa na uwiano sahihi kwa watumiaji. Kamati imepata malalamiko kutoka wadau wa matumizi ya gesi kuwa hali hii inazuia ushindani wa kibiashara na kunyima fursa kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali vinavyotumia nishati ya gesi kukua na kutanuka na pia kudumaza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kuwa, sasa umefikia wakati kwa wadau wa sekta ya gesi kupewa fursa iliyo wazi katika kutafuta, kuzalisha, kusafirisha na kusambaza gesi. Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwa, katika Sheria ya gesi itakayotungwa ni lazima iainishe ugatuaji *(Unbundling)* kwa upande wa utafutaji, usafirishaji na usambazaji. Hii itasaidia kukuza sekta ya gesi nchini kwa kuwa kampuni nyingi za gesi zitahusika kikamilifu na gharama kwa watumiaji kupungua kutokana na ushindani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeupokea ushauri wa Bunge. Katika rasimu ya sheria mpya ya gesi asili iliyoandaliwa, ambayo itawasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge, suala la kutenganisha utafutaji,

uzalishaji na usambazaji ni miongoni mwa masuala yaliyozingatiwa kama ilivyoelezwa katika taarifa hii hapo awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni Maoni ya Kamati. Kamati imepokea hatua za utekelezaji wa azimio hili. Aidha, kwa mara nyingine tena tunaitaka Serikali iharakishe Muswada wa Sheria ya gesi na uje kwa kuzingatia matakwa ya wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 21, *TDPC* akiwa ndiye msimamizi wa sekta ya gesi kwa niaba ya Serikali Kamati inashauri shughuli zote za uwekezaji katika Sekta ya Gesi zisifanyike bila ya kuihusisha *TPDC*. Aidha, *TPDC* ihakakishe gharama zinazoingiwa kwenye mradi wanazihakiki ipasavyo. Pamoja na hayo, Kamati inasisitiza shughuli zozote za uchimbaji zisiendelee bila ya kurekebisha visima ambavyo vimeharibika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeupokea ushauri wa Bunge. Kwa mujibu wa Sheria ya Utafutaji wa Mafuta ya mwaka 1980, Wizara hutoa leseni ya utafutaji na uendelezaji kwa *TPDC*. Aidha, *TPDC* ni mbia katika mikataba yote ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi *(PSA)* hapa nchini. Katika mikataba hiyo ya utafutaji, wawekezaji, yaani kampuni za kutafuta mafuta hushiriki kama wakandarasi wa *TPDC*. Kuhusu uchimbaji wa visima vipya Songo Songo, maelezo ya kina yametolewa katika majibu ya Azimio Na. 16.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji toka Serikalini, haya ni maoni ya Kamati. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali iliyoyatoa awali juu ya kushughulikia visima vilivyoharibika. Aidha, mbali na sheria au taratibu kuonyesha ushiriki wa *TPDC* na Idara nyingine za Serikali katika uendeshaji wa Sekta ya gesi, Kamati inataka zaidi ya maandiko, ionekane wazi kwamba Serikali na asasi zake ndiyo zinamiliki na kuendesha sekta ya gesi.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 22, Kamati imebaini kuwa fedha zinazotolewa na wabia wa *TPDC* katika utafutaji wa mafuta na gesi kwa lengo la kutoa mafunzo ya wataalamu mbalimbali katika Sekta ya gesi hazitumiki kwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati imebaini kuwa fedha zinazofikia dola za kimarekani milioni 1.75 kwa mwaka zinazotolewa na wabia hao hazitumiki kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, Kamati imebaini kuwa sehemu kubwa ya fedha hizi zimekuwa zikitumika kulipia safari zisizo za mafunzo kwa Viongozi na Maafisa Waandamizi wa Wizara. Kamati inaona kuwa kitendo hiki ni ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma na hivyo uchunguzi ufanywe kwa ajili ya hatua zaidi kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa, suala hili halirudiwi tena. Aidha, Serikali inaendelea na uchunguzi kuhusu matumizi ya fedha hizi na hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale wote waliohusika.

Serikali imebaini utata uliopo kati ya madhumuni na jina la kifungu kinachohusu mafunzo, hivyo Serikali itarekebisha kifungu hiki ili kupanua wigo wa madhumuni ya kifungu kitumike kwa ajili ya kujenga uwezo *(Capacity Building)* kwenye sekta ya Nishati badala ya mafunzo *(Training and Technology Transfer)* tu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni maoni ya Kamati. Kamati inaitaka Serikali kwa maeneo ambayo imeainisha kuwa yanafanyiwa uchunguzi kutokana na fedha zake kutumika kinyume na malengo, basi haraka taarifa zake ziletwe mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 23; kufuatia kitendo cha Serikali kutumia fedha zilizokuwa zimepangwa kuondoa utofauti wa bei *(National Tarrif Equlization Fund)* kinyume na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, Kamati inaishauri Serikali kuanzia sasa kutumia fedha kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, inapoonekana kuna ulazima wa kubadili matumizi ya fedha hizo zilizoizinishwa na Bunge, ni vizuri taratibu zinazotawala sheria za fedha zikazingatiwa na bila kuathiri Mamlaka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Aidha, Serikali inakubali kuwa ni muhimu na ni vizuri kuwa taratibu za fedha zifuatwe. Wizara ya Nishati na Madini itaendelea kuzingatia sheria na

bila kuathiri Mamlaka ya Bunge katika utekelezaji wa Bajeti, na kifungu husika kitarekebishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kuondoa tofauti zilizojitokeza katika matumizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji iliyotolewa na Serikali, haya ni Maoni ya Kamati. Kamati imeridhika na inategemea katika Bajeti ijayo kifungu hiki kitarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio Na. 24, Kamati imejiridhisha kuwa hakuna mpango mahsusi wenye kuonyesha kalenda ya ulipaji wa mkopo wa dola za kimarekani milioni 216 na kwamba kiasi gani kitalipwa na lini? Ni mapendekezo ya Kamati kuwa pamoja na manufaa ya mradi huu, mamlaka zinazohusika zinapaswa kujiandaa kwa kupanga ni lini na kwa namna gani watalipa deni hilo pamoja na riba yake kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Aidha, Serikali imeielekeza Wizara ya Fedha kuandaa mpango wa kulipa deni hilo ili uweze kutekelezwa. Serikali ilisaini mikataba 21 ya Mradi wa Uendelezaji Gesi ya Asili ya Songo Songo tarehe 11 Oktoba 2001 pamoja na *TPDC, TANESCO, Songas (CDC Globeleg), PanAfrican Energy (T), FMO, EIB, IDA* na *TDFL.* Miongoni mwa mikataba iliyosainiwa ni mkataba wa *Power Purchase Agreement (PPA).* Mkataba huu ulisainiwa kati ya kampuni ya Songas na *TANESCO*. Mradi wa Songas ulianza kuzalisha umeme kutumia gesi asili kuanzia mwezi Julai, 2004.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa mikopo na mitaji umeainishwa kwenye Kiambatisho Na. F cha mkataba wa *PPA*. Mpangalio wa kimkataba ni kuwa mikopo ya Serikali toka Mashirika ya Fedha, Benki ya Dunia, Benki ya Raslimali ya Ulaya na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden - Sida inahitajika kulipwa na Serikali baada ya kupokea malipo kutoka kampuni ya Songas.

Aidha, *TANESCO* wanawajibika kimkataba kumlipa Songas malipo yaliyoainishwa kwenye mkataba ikiwa ni *Capacity Charge* na *Energy Charge*. Serikali ilikopa Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya na Sida jumla ya Dola za Marekani 209,582,499 ambapo deni hili linatakiwa kulipwa pamoja na riba ya Dola za Marekani 138,031,674 kwa kipindi cha miaka 12 hadi 16.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Mkataba *(PPA)* kati ya *TANESCO* na *Songas; Songas* wanawajibika kuingiza sehemu ya malipo ya mkopo *(principal)* na riba (*interest*) kwenye gharama za *Capacity Charges* katika Ankara ya kila mwezi kwa *TANESCO. TANESCO* wanawajibika kulipa kiasi hicho kwa Songas, kisha Songas wanawajibika kuyapeleka malipo hayo Serikalini (Hazina). Rejea kifungu 4.2(d) *"IDA Subsidiary Loan Agreement", 2.6(d) "EIB On-Lending Agreement"* na *2.5(d) "Loan Assumption Agreement."*

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni Maoni ya Kamati: Kamati imepokea hatua za utekelezaji na inasisitiza katika Mikutano ya Bunge inayofuatia Serikali ilete taarifa ya utekelezaji wa ulipaji wa Mkopo huu.

Mheshimiwa Spika, Katika Azimio Na. 25, Kamati imebaini kuwepo kwa kasoro katika ulipaji wa kodi miongoni mwa Makampuni. Kamati inashauri Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* iongeze udhibiti katika ukusanyaji wa kodi katika sekta ndogo ya gesi kwa kushirikiana na mamlaka na taasisi nyingine za kiserikali na sekta husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imeanza kufanya ukaguzi maalumu wa *PSA* husika kuanzia Januari, 2012. Ukaguzi huu utawezesha kuondoa kasoro zote zitakazoonekana wakati wa ukaguzi. Mamlaka ya Mapato itaongeza udhibiti katika ukusanyaji wa kodi katika maeneo yote yatakayoonekana yana udhaifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Serikali, haya ni Maoni ya Kamati: Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji. Aidha, kwa yale maeneo mahsusi ambayo taarifa za ukaguzi zinaonyesha kuwa kuna ukwepaji wa kodi, tunataka maelezo jinsi *TRA* ilivyofuatilia maeneo hayo moja baada ya lingine. Kwa sehemu ambazo zitabainika kuwepo ukwepaji wa kodi, yasiwepo majadiliano bali hatua za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 26; ili kulinda misitu na kupunguza gharama kwa wananchi, Kamati inashauri *TPDC* iwezeshwe ili kuweza kutekeleza miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Bunge. Aidha, Serikali imeona umuhimu wa ushauri huu na tangu mwaka 2010/2011 ilianza kuiwezesha *TPDC* kwa kuiruhusu kubakiza asilimia hamsini *(50% retention)* ya mapato yatokanayo na mauzo ya gesi asili ili iwekeze katika miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari. Kwa kutambua umuhimu wa azma hii, Serikali imeiruhusu *TPDC*, kwa kuanzia, kukopa fedha kwa riba nafuu Dola za Marekani milioni 55 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji gesi asili Dar es Salaam kwa nia ya kuokoa matumizi ya mkaa ambayo yanakadiriwa kuwa magunia 40,000 kwa siku.

Baada ya kupata taarifa ya Serikali ya utekelezaji, haya ni maoni ya Kamati. Kamati imeridhishwa na Utekelezaji wa Azimio hili. Aidha, pamoja na ruhusa ya *TPDC* kwenda kukopa kwenye taasisi zenye riba nafuu, tunaendelea kushauri waachiwe mapato yao ya gesi kwa asilimia mia moja ili kuendelea kuwekeza katika sekta ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipitia taarifa ya Serikali utaona dhahiri kuwa majibu ya maazimio mengi ni ahadi, tunatumia fursa hii kuishauri Serikali kuwa ahadi hizi zitekelezwe kama zilivyoainishwa kwenye taarifa hii. Aidha, ili kuipunguzia Serikali mzigo, tunaagiza mpango wa utekelezaji wa maazimio haya uendane na kutoa taarifa mara kwa mara kwenye Kamati na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Adama Malima, Katibu Mkuu Ndugu Eliakim Maswi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kushirikiana na Kamati katika kujadili suala hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa michango yao mizuri ambayo imewezesha kutoa taarifa katika muda mfupi. Napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa January Y. Makamba ni Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mhehsimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Khalfan Hilary Aeshi, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Yussuf A. Nassir, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Shafin Amedal Sumar, Mheshimiwa Seleman J. Zedi, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Josephine T. Chagulla, Mheshimiwa Mwanamrisho T. Abama, David E. Silinde, Mheshimiwa Suleiman M. Nchambi, Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri, Mheshimiwa Ali Mbarouk Salim, Mheshimiwa Sarah Msafiri, Mheshimiwa Munde A. Tambwe, Mheshimiwa Vick P. Kamata, Mheshimiwa John J. Mnyika na mimi mwenyewe Charles J. Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vile vile namshukuru Katibu wa Kamati - Ndugu Pamela Pallangyo kwa kuihudumia Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Umewasilisha vizuri na kwa ufasaha sana.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, hatujadili hoja ya Kamati ndogo, tunajadili utekelezaji uliofanywa na Serikali kuhusiana na hoja ya Kamati ile ndogo ambayo utekelezaji wake tumeshapewa majibu na bahati nzuri Kamati imepitia hoja baada ya hoja. Wasiwasi wangu ni kwamba, hawa wote wanaoomba sijui wanataka kusema nini, maana hamtaanza mjadala wa gesi muelewe hivyo. Kwa sababu, sasa hatuwezi kuwa tunajadili hoja isiyokwisha.

Kwa hiyo, namwita msemaji wetu wa kwanza ambaye atakuwa ni Mheshimiwa Januari Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa John Mnyika atafuatia na wengine nitawaita baadaye.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kwanza ya kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru tena kwa kuturuhusu kuunda Kamati Ndogo ya kupitia jambo hili, kuwasilisha taarifa yetu Bungeni, Serikali kutoa ripoti kuhusu utekelezaji na leo Kamati kutoa ripoti tena kuhusu taarifa ya utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama ripoti yetu ilivyosema ni kwamba taarifa ya Serikali ni taarifa ya ahadi. Kwa hiyo, leo ndiyo tunaanza safari ya utekelezaji wa maoni ya Kamati Ndogo. Tunaamini kwamba *spirit* iliyoonyeshwa ndani ya Kamati, kati ya Serikali na Kamati kwa maana ya kushirikiana ili kuhakikisha haya mambo tuliyoyapendekeza na ambayo tumeyaainisha yasaidie nchi yetu kunufaika na sekta hii ndogo yatatimizwa kwa haraka na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wanasema: "Ukitaka kuliua jambo, unaliundia Kamati." Waingereza wanasema ukitaka kuua jambo, unaliundia *commission*, sasa Serikali imeunda Kamati inaitwa *Government Negotiating Team(GNT)* ili iweze kufanya kazi, Serikali na taasisi nyingine kuhusu mambo yanayohusiana na *Pan African Energy*, nia yetu na imani yetu kwenye Kamati ni kwamba ile timu ya Serikali imeundwa kuhakikisha haya mambo tunayamaliza na tunayamaliza mapema, shaka ni kuliendeleza hili jambo kwa muda mrefu na likakosa kuwa na mwisho kama lile jambo lingine kwenye Bunge lililopita ambalo limeendelea na kuendelea. Tunataka tufikie mwisho kwenye hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwenye baadhi ya mambo ambayo tuliyaainisha sisi kwenye ripoti yetu, kwa kweli hayahitaji mjadala, yanahitaji utekelezaji tu, na hasa lile suala la malipo ya dola milioni 20 ambazo hata ile Kampuni imekiri kwamba kulitokea udanganyifu na pesa zile walizirudishia isivyo halali na ukaguzi unaonesha hivyo. Hilo suala halihitaji *negotiation,* lile suala linahitaji utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, imepita miezi kadhaa maana yake ile ripoti ilikuwa mwezi wa Nane leo ni mwezi wa Pili. Tungekuwa tumeshajua kama *invoice* imekwenda na kiasi fulani kimeanza kulipwa. Lakini vile vile tunatambua na kwenye Kamati tumeelewa dhana ya Serikali kwamba ni lazima uchukue hatua ambazo hazitakuingiza kwenye mgogoro wa kisheria na hatutaingia kwenye kushtakiana, lakini sisi kwenye Kamati tunaamini kabisa haki ipo upande wa Serikali na wenyewe wakijitahidi watapata hizo pesa kwa ajili ya manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *GNT* kama nilivyoelezea, lakini tunafurahi kwamba sasa *CAG* ameshirikishwa katika kukagua zaidi kwa sababu bado kuna uwezekano kwamba fedha nyingi zaidi zimepunjwa, na sisi kwenye Kamati tunaamini kwamba fedha nyingi zaidi bado zimepunjwa kilibaki kiasi cha dola kama milioni 35 hazijafanyiwa ukaguzi. Tunashukuru kwamba ameingia *CAG*, imani yetu ni kwamba *CAG* atamaliza hiyo kazi mapema na ripoti yake itawekwa wazi na pale itakapoonesha kwamba tumepunjwa, basi tusicheleweshwe kulipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile wakati tunafanya hii kazi ya Kamati ndogo tuliwaita *TRA* tuzungumze nao na tuwaeleze kwamba hapa kuna matatizo ya kikodi, na bahati nzuri *TRA* wakaona kwamba kweli kuna hitilafu mahali fulani, na tunashukuru kwamba *TRA* wameanza uchunguzi toka mwezi uliopita wa Kwanza kuhusu uwezekano wa kwamba kodi ya Serikali imekwepwa, yuko *CAG* na *TRA*. Lakini kuna mtu mwingine tunataka aingie na mwenyewe ni *DCI,* kwa sababu hapa kuna tatizo la kijinai ambalo inawezekana limetokea na Kamati yetu ilipendekeza kwamba ni lazima hatua za kijinai zichukuliwe na ripoti yetu ya utekelezaji imesema hivyo na tungependa jambo hilo lianze kesho, kwa sababu yapo mambo yamefanyika ambayo ni dhahiri kabisa ni udanganyifu. Ni dhahiri kabisa ni kinyume kabisa na sheria za nchi hii na sisi tunataka sasa ifike mahali tusishikwe rehani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tulichojifunza katika mchakato huu ni kwamba Taifa linaweza kuwekwa rehani na Mwekezaji, na tulichoona hapa kilichotokea ni kwamba maelezo yanatolewa kwamba mmeona kabisa dhahiri tumedhulumiwa, tumepunjwa, jinai imefanyika, lakini maelezo ni kwamba unajua tukivunja mkataba hapa tunaweza tukapata matatizo kama nyuma tukashtakiwa, au unajua tukivunja mkataba hapa au tukichukua hatua za kimkataba tutachelewesha miradi ndiyo maelezo. Kwa hiyo, afadhali tuendelee na unyonge huu huu ili tusiwachokoze hawa jamaa wakachelewesha miradi yetu. Maelezo mengine ni kwamba unajua tukiwa-*harass* hawa watu tutaharibu mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa ni lazima tuwe tayari kutetea rasilimali zetu na ni lazima tuwe tayari kuchukua hatua madhubuti pale tunapoona dhahiri tunadhulumiwa, hatuwezi kuwa wanyonge, tunasema tunaogopa kuharibu mazingira ya uwekezaji, kwamba Tanzania tutakwenda chini kwenye *ranking* ya uwekezaji kwa sababu tu tumechukua hatua za kimkataba za kupata haki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niishie hapa ili kutoa fursa ya wengine kuzungumza kwa sababu muda ni mfupi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa John Mnyika ajiandaye na baadaye Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa kucheza ngoma ya Kisukuma ulivyokuwa unasheherekea miaka 35 ya Chama cha Mapinduzi.

**SPIKA:** Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nikiwa kama mmojawapo wa Wenyeviti wako, nataka kusema kwamba ripoti hii ndiyo chanzo cha kuonyesha jinsi gani Bunge lako linaweza kusaidia Serikali kukokotoa mapato ambayo tunapoteza, ni ripoti nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia ningeshauri wasiishie hapa. Ninaona inafaa tena watengeneze Kamati ndogo waangalie mikataba upya tena ya madini. Kila wakati tunaona magazeti yanazungumza kwamba watu wanataka kuibiwa Shilingi bilioni 40, kumbe ni Shilingi bilioni 135. Huu ni udanganyifu! Vitu kama hivi vinaweza vikapatikana tu kama Kamati zako zitafanya kazi ya uchunguzi kuleta mapendekezo hapa, tukatoa maazimio na maazimio hayo tukayafuatilia mpaka yametekelezwa. Hii ni ishara nzuri sana na mimi ninawapongeza sana Wajumbe wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumza ni kwamba, katika Kamati ya *PAC (Public Accounts Committee)* tulipokuwa tunazungumza na Afisa Mhasibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tulimwuliza, hivi ni vipi kila mkataba haufai, mbovu, mkataba wa gesi mbovu, mkataba wa madini mbovu, mkataba hata wa kuuza mahindi mbovu, *what is wrong*! Hivi kuna kitu gani ninyi Wanasheria ambao tunao hapa, mnakwenda shule gani tofauti na wanasheria wengine wa dunia hii ambao wenyewe wanaweza wakatengeneza mikataba ambayo inawasaidia wawekezaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumegundua Serikali kwa maksudi imefanya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iwe haina kazi kabisa kwa kuweka kitu kinachoitwa *GNT (Government Negotiating Team)* na Mwanasheria ni mmojawao wa hii *GNT*.

Mheshimiwa Spika, hebu niambie, hapa tumezungumza juu ya *GNT,* kama ukitaka kweli mtu tumwajibishe, tutamwajibisha nani? Huyo mtu anayeitwa *GNT* utampata wapi? Anachaguliwa kwa misingi gani? Hata Waziri, tumekuwa na matatizo makubwa mengine *Richmond* na kadhalika yote hayo mwisho wake ilikuwa ni *GNT*, na tukashindwa. Ni nani huyu *GNT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningefikiria Serikali bado iangalie hili jambo. Zaidi, wakati huu tunapokuwa na mikataba hii ambayo inahusu pesa, ndugu zangu niwaambie kwamba, sasa wakati umefika tutumie tulivyopewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mapato ya Serikali, na mapato hayo ndiyo yatumike katika kuendesha bajeti yetu ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka yote ambayo mimi nimekuwa Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee (PAC)* kama kuna bajeti ambayo haifanyi kazi ni bajeti ya Maendeleo, na kila wakati ndiyo hiyo inanyimwa pesa. Pesa hizi zinatoka kwa Wafadhili. Wafadhili wa siku hizi na wenyewe wanakopa, hawana hela. Wenyewe hawana madini, wamebakiza lugha tu nzuri, lakini hawana kabisa *natural resources*, ni sisi tu Afrika, ni sisi tu Tanzania tuliobakia, kila ukigusa una mali uliyopewa na Mwenyezi Mungu bure.

Mheshimiwa Spika, ukienda Singida, kuna madini; ukienda Kusini, kuna gesi; ukienda hata Mkuranga pale, kuna gesi; kila mahali. Lakini mikataba hii ndiyo inatumaliza kwa sababu ya *Government Negotiating Team* ambayo haijulikani ni nani. Hujui utamkamata mtu gani, na sheria ya Mwanasheria Mkuu

imesema wazi kwamba *the final council to the Government will be the Attorney General.* Yeye akisema, hakuna mwingine wa kugeuza maneno yake isipokuwa *a Court of Law.* Lakini hizo *power* sasa hana, *Power* hizo sasa zimewekwa kwa *GNT*.

Mheshimiwa Spika, ninachoishauri Serikali, hebu mkaliangalie hili jibu upya, hata kama umeweka *Government Negotiating Team,* bado tunataka kujua kwamba tutakayemkamata kwa mkataba mbaya ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kama yeye akiweka ndiyo maana yake amekubali yale yote yaliyomo mle atayabeba, lakini sasa hivi tutamwonea huyu Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na kijana mmoja juzi alikuwa anasikitika hapa, alikuwa hana mamlaka. Huo ndiyo ushauri wangu. Ili tupone, tutumie tulivyopewa na Mwenyezi Mungu kuifanya Tanzania namba moja katika Afrika na hakuna mtu anaitwa maskini. Hakuna sababu kuitwa maskini na wewe ni mtu wa tatu kupata dhahabu katika Afrika. Haiendi pamoja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, yote haya ambayo tumesema ni matatizo ya kunyang'anywa pesa na imenifanya nimeona ni vizuri sana kwamba kila wakati tunasema *CAG* wetu nenda ukaangalie hili, huu ni utaratibu mzuri. Lakini zile ripoti za *CAG* ambazo zinafanyiwa hizi *special report,* mbona haziji hapa Bungeni? Zinabakia kule kule! Kwa hili ni rahisi sana kumtumia *CAG* wetu kusafisha uchafu wa watu. Hatutaki kumtumia *CAG* kusafisha uchafu wa watu wanaoharibu.

Mheshimiwa Spika, kama vile sheria inavyosema, Ibara ya 11 ya *Audit Act,* inaeleza wazi sana kwamba baada ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi ataleta ripoti hizo. Siyo ripoti moja tu, ni ripoti zote kwenye Bunge kwa utaratibu ambao umewekwa na Katiba, *Article* 143(4) huo ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Spika, sasa wanapomtumia *CAG,* anasafisha huko, halafu baadaye mnaleta hapa, ooh, ooh! Ooh ooh nini? *CAG* ni mtu ambaye anafanyakazi kwa niaba ya Bunge hili, *is the Officer of the Parliament* na sisi wote pia ndiyo tunaomtegemea kwamba sisi Wabunge hatuwezi kwenda kuangalia kila akaunti, lakini tunaye Afisa wetu *CAG* ambaye ni lazima alindwe na Bunge hili kwa sababu ni Afisa wa Bunge hili. Kwa hiyo, tunataka kazi zake zote mnazomwomba na anazoafiki kuzifanya, ziletwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwe pia marufuku baadhi ya viongozi kila siku akisimama pale nimemwagiza *CAG* afanye (a), (b), (c), (d).

Mheshimiwa Spika, *CAG* wa Tanzania na kokote duniani haagizwi na mtu yeyote, yeye anachunguza kufuatana na utalaam ambao ameuona unaweza ukamwomba, *PAC*, wanaweza kumwomba, *POAC* wanaweza wakamwomba, lakini iwe yeye ndiyo atoe maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri tukifanya baadhi ya mambo ambayo nimesema, Kamati zako kweli itaisaidia Serikali kuweza kupata mapato mengi ambayo tunayahitaji kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni pamba. Leo asubuhi Waziri ametueleza anataka kuleta pamba inayoitwa *GMO (Genetic Modifying Cotton),* sisi hatutaki *GMO. Genetic Modified Cotton* haina soko, usituulie pamba yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwanza hilo la mwisho halifanani na gesi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na Waziri Kivuli wa Nishati na Madini. Naomba nielekeze mchango wangu kwenye taarifa ya Serikali kama ilivyowasilishwa nikianzia na ukurasa wa tatu kuhusiana na azimio la pili.

La kwanza, hii taarifa ilitokana na maazimio ya tarehe 18 Novemba. Leo ni tarehe 7 Februari, 2012. Kwa hiyo, ni miezi michache iliyopita toka Bunge lifanye maazimio. Kwa hiyo, kwa kuangalia kiwango cha muda kutoka Maazimio yafanyike mpaka sasa mwezi Februari, angalau taarifa hii ya Serikali imeonyesha

hatua. Lakini hatua hizi bado ni ahadi. Kwa kweli ahadi ni deni na hazijafikia hatua ya kuweza kwa pamoja kusema kwamba sasa utekelezaji umetimia.

Kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali kwa ujumla ni kwamba ni muhimu sana ifikapo Mkutano ujao wa Bunge mwezi Aprili, tukaletewa taarifa isiyokuwa na ahadi nyingi, taarifa yenye vitendo vingi ambayo itaonyesha kweli kwamba hili jambo sasa linamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mwezi Februari, 2008 Bunge lilipopitisha Maazimio kuhusiana na *Richmond* mwezi *August*, 2008 miezi michache baadaye wakati ule taarifa ya Serikali ya wakati ule ilitilia matumaini sana. Lakini miaka minne baadaye bado Taifa linaendelea kuzungumza masuala ambayo ni ya kutoka mwaka 2008. Sasa isije ikawa katika jambo hili la gesi asilia Maazimio ya mwaka 2011 tukaendelea mpaka 2012, 2013, 2014, 2015, 2016 tukaendelea tu kuyajadili mambo ambayo yanapaswa kumalizika. Sasa na hapa tunakwenda kwenye azimio la pili ambalo kuna mambo ambayo ni vizuri Serikali ikaharakisha utekezaji.

La kwanza maamuzi ya kuunda *Government Negotiation Team* ni maamuzi ambayo yanapaswa kupokelewa kwa tahadhari. Ningeshauri Serikali wakati *Government Negotiation Team* inakwenda kufanya kazi, hiyo timu ya Serikali ikapitia azimio namba 5, 7, 9 na 14 ya wakati ule ya *Richmond* ambayo yalizungumzwa kuhusu masuala ya *Government Negotiation Team*. Kama hayo, yasipozingatiwa, hili suala la kuundwa kwa *Government Negotiation Team* linaweza likawa tena mgogoro mwingine. Tunahitaji tena kuunda Kamati nyingine ya kuichunguza *Government Negotiation Team* kwenye masuala ambayo Bunge liliazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya ya moja kwa moja kama ya udanganyifu wa dola milioni 20.1 haya kweli yanahitaji hatua za kisheria. Lakini ningependa kuweka vile vile tahadhari kuhusiana na hizi dola milioni 35. Hizi milioni 20 ni takribani bilioni 30 na hizi nyingine ni zaidi ya bilioni 40, fedha nyingi sana zaidi ya bilioni 50. Wakati *CAG* anakwenda kufanya uchunguzi na ukaguzi ni vizuri hili jambo likaharakishwa sana. Mimi ni Mbunge wa Dar es Salaam, sisi tunalalamika kule kuhusiana na uchunguzi wa kashfa ya *UDA* ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa rai kwa *CAG* kufanya uchunguzi. Sasa mpaka sasa uchunguzi unaendelea tu. Lakini wakati uchunguzi unaendelea, Kampuni ya *Simon Group* inaendelea kuendesha Shirika la *UDA* na matokea yanaendelea kuwa mabaya zaidi.

Sasa hii inahusu dola milioni 35 ambavyo vielelezo vyake vinapaswa kuchunguzwa. Ni vizuri wakati *CAG* anachunguza, moja achunguze kwa haraka, lakini pili, uchunguzi wake uhakikishe kwamba vielelezo haviharibiwi ili baadaye haya madai ya dola milioni 35 yasibadilike na kuwa madai tofauti. Kwa hiyo, ni kuhusu azimio la pili.

Kuhusu Azimio la 12 ukurasa wa 12, kuna Azimio hapa kuhusiana na majadiliano na *Songas* ambayo na yenyewe yameundiwa yanakwenda kufanywa na *Government Negotiation Team.* Ningependa na yenyewe kutoa tahadhari.

Mheshimiwa Spika, hili azimio la 12 la Kamati la Bunge la mwezi Novemba, 18 kimsingi ilikuwa ni marudio ya Azimio ambalo Bunge liliazimia mwaka 2008, azimio la tatu la Kamati ya *Richmond* lilisema mikataba, likataja mikataba ikiwemo Mikataba ya *Songas* ipitiwe upya. Kwa hiyo, leo mwaka 2012 tunapokea tena taarifa ya utekelezaji ya Serikali ikionyesha kwamba majadiliano ya kimikataba na Kampuni ya *Songas* ambayo majadiliano yalipaswa yakamilike kutoka mwaka 2008 bado hayajakamilika mpaka hivi leo.

Kwa vyovyote vile Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, taarifa ya Serikali isipoonyesha majadiliano na kampuni ya *Songas* ambayo kimsingi yanachangia vile vile kwenye bei ya umeme kwamba yatakuwa hayajakamilika kwenye nyongeza ya gharama ya bei ya umeme, kimsingi Bunge lako Tukufu lichukue hatua nzito sana kwa mujibu wa ibara ya 63 ya Katiba ya kuisimamia Serikali kwa sababu hili ni jambo la muda mrefu sana kutoka mwaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 16 kuhusiana na Azimio la 18, hili nilizungumza kwa kirefu tarehe 18 nilipopewa nafasi ya kuchangia nikitaka maelezo ya kina zaidi ya Serikali. Kuna mstari wa Azimio la Bunge ambao naomba niurudie kuunukuu kwa faida ya rejea ambao uko ukurasa wa 17. Kamati inaishauri Serikali kuwawajibisha Viongozi Wakuu na Watendaji waliohusika na uzembe huu na kuteua wengine

wenye uwezo haraka iwezekanavyo. Ushauri huu wa Kamati ulitokana na Kamati kubaini kwenye azimio la 18 kwamba, katika hali hiyo ya kusikitisha na kuvunjwa moyo, Kamati imejiridhisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa haitoi ushirikiano wa kutosha kwa *TPDC, EWURA* hasa katika kusimamia masuala ya sekta ya gesi nchini.

Kwa hiyo, baada ya kuona hali hiyo, Kamati ikaishauri Serikali kuwawajibisha Viongozi Wakuu na Watendaji waliohusika na uzembe huu na kuteua wengine wenye uwezo haraka iwezekanavyo. Kwenye maelezo ya Serikali kama tulivyogawiwa, hakuna maelezo yoyote ya namna ambavyo Serikali imewajibisha Viongozi Wakuu na Watendaji waliohusika na uzembe na kuteua wengine haraka iwezekanavyo. Hakuna maelezo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafahamu kwamba kule Wizara ya Nishati na Madini, Katibu aliyekuwa amesimamishwa akachunguzwe aliondoka bila kufukuzwa, aliondoka bila kuwajibishwa, uteuzi tu ulibadilishwa. Kwa hiyo, kwa maana ya hatua kwa Bwana Jairo, hatua hasa hasa hazichukuliwa. Sasa mimi ningependa sana Serikali katika hili itoe maelezo, ni hatua gani imechukua katika kutekeleza hili azimio la Serikali kuwawajibisha Viongozi Wakuu kwa Azimio la Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende ukurasa wa 22 kwenye Azimio la 26. Nashukuru kwamba Serikali imekubali kuongeza fedha kwa *TPDC* na kuwezesha *TPDC* kukopa dola milioni 55. Lakini naunga mkono wote waliotaka *TPDC* ipewe *retention* ya asilimia 100 badala ya asilimia 50. Lakini *TPDC* iwezeshwe kukopa zaidi kwa sababu kama kuna sehemu ambayo tunaweza kusaidia Taifa, hivi sasa gharama za maisha zinapanda. Ni mzigo mkubwa kwa sababu ya kiwango kikubwa cha mafuta ambacho tunaagiza kutoka nje ya nchi, tunatumia mafuta, *petrol, diesel* kwa kiwango kikubwa sana wakati nchi yetu ina gesi, tungeweza kutumia gesi viwandani, kwenye majumba, kwenye magari, kwenye matumizi mengine.

Sasa ni lazima kama Taifa tuamue kwamba hiki ni kipaumbele cha dharura cha haraka sana. Kiwango cha fedha hiki kilichopo hapa bado hakionyeshi huo udharura. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba fedha hizi ziongezwe, na katika kuongezwa huko, miradi ile ya kupeleka gesi asili pale Kituo cha Magari cha Ubungo, miradi ya kupeleka gesi asili Mikocheni, ihusishe vile vile kupeleka gesi asili Sinza na miradi ya viwanda pale Dar es Salaam, ihusishe vile vile *Ubungo Industrial Area*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho liko kwenye azimio la 25 kuhusiana na hatua za *TRA* juu ya makampuni kukwepa kodi. Pamoja na maelezo ya Serikali, ningependa maelezo ya ziada kwa sababu nilipochangia mjadala huu tarehe 18 Novemba siku ya kuwasilishwa kwa taarifa nilitoa rai kwa Serikali kwamba itakapofuatilia huu ukwepaji kodi ifuatilie vile vile tuhuma zilizoko kwenye ripoti ya *Action Aid* ya Sweden ya Kampuni ya *Pan Africa* ukiondoa tuhuma zilizopo kwenye taarifa ya kukwepa kodi kiwango cha dola milioni 65 ambayo ni takribani bilioni 90 kwa kutumia *off show companies.*

Sasa kwenye maelezo ya Serikali imeelezwa tu kwa ujumla kwamba *TRA* imeanza kufanya ukaguzi kuanzia Januari. Ningependa maelezo mahsusi kuhusu hii tuhuma iliyopo kimataifa ya *action aid* ya dola milioni 65 ambayo ni sawasawa na bilioni 90, na ni hatua gani *TRA* na Serikali na Wizara ya Nishati na Madini zinachukua kuhakikisha kwamba mianya yote ya ukwepaji kodi kwa kutumia matumizi *off show*, kwa kutumia njia nyingine kwa makampuni haya makubwa kwenye sekta ya gesi na sekta nyingine ambazo zingeweza kusaidia kwa Pato la Taifa inazibwa ili Watanzania tuweze kunufaika na rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo ni ya msingi sana kwenye kuzingatiwa. Tusipokuwa makini na hatua za haraka kuchukua kwenye sekta ya gesi, nchi hii itakwama. Sasa hivi mpango wa dharura wa umeme unatekelezwa. Kampuni moja *Symbion in total* kwa sasa ukiondoa…. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ya mwisho ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kwa haya niliyoomba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kigumu sana kama kutekeleza jambo. Ni kitu kigumu sana. Kwa sababu utekelezaji wa mambo unahitaji maamuzi magumu. Lakini kuandika taarifa kusema kwamba tutafanya hivi ni kitu ambacho kinawezekana tu na mtu yeyote yule anaweza akafanya. Lakini kuchukua maamuzi magumu ya kuvunja mikataba ni kitu kigumu sana ambacho kinahitaji maamuzi magumu sana ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa ya Kamati imeeleza vizuri sana, lakini mwishoni imekiri kabisa kwamba mengi ni ahadi za kutekeleza. Wazungumzaji waliotangulia wamezungumza akiwemo Mheshimiwa Mnyika. Kuna maazimio mengi sana ya *Richmond* ambayo kama yangetekelezwa inawezekana hata hii Kamati Ndogo, isingeundwa yakiwemo Maazimio ya Songas. Lakini kuchukua maamuzi magumu imekuwa ni kitu ambacho hakifanyiki.

Serikali inaogopa, ndio maana katika utekelezaji wake inasema haya sijui nini, tumeunda *Negotiation Team* lakini kuna mambo ambayo ya kimikataba na yako kisheria. Kampuni inapovunja mkataba, inapokwenda kinyume na *terms* za mkataba, mkataba ule unavunjwa. Ndio taratibu za kisheria. Mimi siamini kwamba hii *Government Negotiating Team* itakwenda kuibua kitu kingine tofauti na kuvunja mikataba kwa sababu ni jambo ambalo tulishaamua kama Bunge kwamba hii mikataba ivunjwe kwa sababu haitunufaishi. Mtu anapokiuka *terms* za *contract* ni ku-*discharge contract*, tuna *negotiate* kuendelea naye mtu ambaye ameshaonyesha nia mbaya, tuna-*negotiate* naye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Watanzania wanachohitaji, kuna fedha zimepotea zaidi ya dola milioni 20. Watanzania wanachohitaji ni kurudishiwa hizi fedha. Watanzania tunataka fedha zetu zirudi, ndio tunachotaka. Kuna mkopo huu wa zaidi ya dola milioni 216. Tunachotaka ni kalenda ya fedha zetu kurudi, ndio tunachohitaji sisi Watanzania. Lakini tukiendelea hivi, kwanza Bunge letu litakuwa linapoteza heshima yake na hadhi yake kwa sababu tunapotoa maagizo na naomba hili lizingatiwe kwamba tufikie sehemu Bunge tuwe tunatoa maagizo na muda wa kutekeleza maagizo hayo. Tunatoa Azimio na muda wa kutekeleza hilo azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa tuna maazimio, halafu tunaacha tu Serikali ikafanye vile inavyoona inataka au vile inavyoona inafaa, tutakuwa tunatoa maazimio kama yaliyofanyika mwaka 2007/2008 kwenye *Richmond* lakini mpaka leo maazimio yale hayatekelezwi. Tutaunda Kamati nyingi, matokeo yake Watanzania wataendelea kuumia na Mikataba hii mibovu itaendelea kusainiwa na bila hatua zozote zile kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuchukuliana hatua kuwajibika. Kama tunafikia maamuzi na hakuna mtu yeyote yule anayewajibika, maamuzi yale yatakuwa hayana nguvu yoyote na watu wengine hawataogopa kufanya vile. Kwa mfano, Wanasheria ambao waliingia Mikataba hii mibovu ambayo haina maslahi kwa Taifa hawajachukuliwa hatua yoyote. Jambo hili wala hakuna aliyewajibika wala haijulikani aliyekosea ni nani wakati wa kuingia mikataba hii?

Mheshimiwa Spika, kama watu hawawajibiki, kama watu wanasaini mikataba na tunawaacha tu tunatoa Maazimio, Serikali inakaa, itakaa mpaka itakapojisikia hata miaka 10 itatoka awamu hii itaingia awamu nyingine, hakuna ambacho kimetekelezeka, tutakuwa hatutekelezi wajibu wetu wa kuisimamia Serikali. Tutakuwa kinyume na Katiba yetu, tutakuwa hatuzingatii ushauri. Kuna Spika mmoja aliwahi kuandika kitabu kinaitwa. “Bunge lenye meno.” Tutakuwa siyo Bunge lenye meno kama maagizo ya Bunge yanakuwa hayatekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima watu ambao waliingia Mikataba hii haiwezekani kwamba wanasheria alioingia mikataba hii wao walikuwa hawafahamu sio kitu kinachowezakana wala hawakudanganywa na wanasheria wa upande mwingine. Walikuwa wanafahamu sasa ni hatua zipi zimechukuliwa mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, naomba sana jambo hili la kuwachukulia hatua watu ambao wanasababisha uzembe lifanyike na litekelezwe.

Tumekuwa tunaomba hapa na wamesema Serikali kwamba wataleta Muswada kwa ajili ya Sheria na Sera ya gesi ni jambo ambalo linahitaji utekelezaji wa haraka, tusije tukafika hapa mwezi wa Nne, bado jambo hili halijatekelezwa. Itakuwa kama kwenye Sekta ya Madini, tumekuwa tunasema kila siku kwamba

utaratibu huu wa kutoa *prospecting licence*, watu wanakwenda kufanya utafiti wa madini, wanachimba tu madini kwamba wako wanafanya utafiti kumbe wanachimba. Tuwe na chombo chetu ambacho kitakuwa kinafanya *survey*, tujue kiasi cha madini na hili suala la gesi tunapaswa kutunga Sheria haraka, tunapaswa kuwa na Sera ambayo itatetea na kulinda rasilimali zetu mambo haya, tunaomba yasije tena kwa ahadi. Yakija kwa ahadi ni kwamba litakuwa ni Bunge la kutoa maagizo na Serikali ya kuahidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nitatumia dakika zangu chache katika muda huu, lakini kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiye aliyenipa afya na uzima nikaweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, yangu yatakuwa machache katika suala zima la mjadala huu wa leo kwa sababu kama ulivyosema, Kamati ilitoa maagizo. Serikali imekwenda kufanya mchakato mzima wa utekelezaji. Kamati yetu ya Bunge leo imekuja katika kutoa maoni mbalimbali na sisi tuweze kuchangia jinsi gani katika suala zima la sekta ndogo ya gesi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukipitia maazimio yote yaliyopendekezwa na Kamati na sehemu ya utekelezaji jinsi gani Serikali imejipanga, napenda kuzipongeza sehemu zote mbili kwa sababu Kamati yetu imetusaidia sana kuhakikisha kwamba inaielekeza Serikali nini cha kufanya. Lakini kama nilivyosema, yangu ni machache sana mchana huu wa leo. Tatizo kubwa ni kwamba tuna watu ambao hawako *committed* kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu ya Tanzania. *That is the problem. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa hapa, ni kwamba katika Wizara zetu, hasa baadhi ya Watendaji wa chini ambao wengine wamepewa dhamana, hawafanyi kazi kwa ajili ya masilahi ya Watanzania. Hata hili suala zima tunasema kwamba inawezekana Serikali inavishwa *word*, ni kweli kuna baadhi ya watu ambao wako maofisini, niwaambieni wana CCM wenzangu wengine sisi hawatupendi na wanafanya uharibifu wa hali ya juu na hili tusilikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mchakato mzima ukiuangalia, naiomba sana Serikali na kwa sababu ni Serikali sikivu na kwa sababu tumejipanga katika hili kuhakikisha tunabaini baadhi ya watu ambao wanafanya ubadhilifu mkubwa unaoendelea na kwa sababu sekta ya gesi kwa mfano tulivyojipanga katika utekelezaji na nina imani kama tutakwenda na *time frame* katika kila Azimio, tukifika Bunge la kikao kijacho, tutakuja na majibu muafaka kwa ajili ya kumnasua Mtanzania wetu huyu ambaye yuko katika hali ngumu sana.

Sasa hivi ukifikiria suala la umeme ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Hii hali haikubaliki hata kidogo! Lakini ukija kuangalia jinsi gani baadhi ya watu katika suala zima la mikataba, mimi nasema hapo ndiyo tatizo la msingi lilipo au haiwezekani kwamba hawa *Pan African Limited* karibu ya dola bilioni 20.1 watu wanaonekana ni kweli wameiba, taratibu hazijafuatwa, lakini mpaka leo hii bado kuna kigugumizi cha kurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ni wazi kabisa kuna baadhi ya watu wanawasaidia mpaka hawa watu wasirejeshe hizi pesa Serikalini. Hili kweli ni tatizo la msingi lazima tuweze kulibaini, kwa sababu haiwezekani watu tathmini yote iliyofanyika, nguvu zetu zimetolewa, imeonekana kweli *Pan African Limited* wanatakiwa warejeshe hizo pesa, lakini mpaka leo hii bado kuna kigugumizi. Hii *negotiation team* inawezakana hata kama tutaunda *team* ambayo baadaye inakwenda kupatana jinsi gani utaratibu utakuwa, lakini siyo kurejesha hizi pesa. Tuangalie mzigo wa Watanzania sasa hivi. Mimi naamini gesi ndiyo ufumbuzi pekee kwa ajili ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa sababu ukifikiria sasa hivi hata gharama za umeme zilizopanda, nimezungumza juzi hapa, suala zima hata tukiangalia tumeingia katika wakati mgumu, umeme tunaununua kutoka *Symbion Power*, kununua kutoka *Agreko* jinsi gani saa nyingine unaigharimu nchi yetu ya Tanzania.

Kwa hiyo, maana yake tatizo la kutatua changamoto hii ni lazima kuhakikisha kwamba sekta ya gesi inasimama vizuri katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini siyo kusimama pekee yake, ni lazima tuhakikishe kwamba inasaidiwa vya kutosha. Kwa mfano tumesema *TPDC* iweze kupewa nguvu, iweze kusimamia sekta ya gesi nchini kwa kadri iwezekanavyo. Lakini kuna suala zima la Sheria ya Gesi, mimi naiomba sana

Serikali katika Bunge lijalo Sheria hii iweze kuja. Inawezekana upotevu wote unatokana ni kwa sababu hatuna sheria maalum inayosimamia sekta ya gesi na watu wanatumia mwanya huo huo, jinsi gani ya kuikandamaiza Serikali.

Naiomba sana Serikali kwamba katika Bunge lijalo, kikao kijacho, sheria hii iweze kufika hapa tuweze kuifanyia mjadala mpana. Lakini kupitia changamoto mbalimbali, hata hawa watu wa *Pan African* nimepata *report* kutoka kule Kilwa kwa ndugu yangu Mangungu kwamba hata ulipaji wa *commodity tax* katika Halmashauri pale ni tatizo. Halmashauri imebaki kuwa hoi japokuwa rasilimali ile inatoka katika maeneo yao. *Service levy* hailipwi kule Kilwa, jinsi gani tutaendesha Halmashauri zetu wakati rasilimali inatoka katika maeneo ya wakazi husika? *(Makofi)*

Ndugu zangu *impact* tunayopata katika uchumi kutokana na suala zima la umeme Tanzania ni kubwa sana. Mimi nikichukulia mfano mmoja pale Kisarawe kwetu, kuna benki yetu ya *NMB,* kila siku wana-*run generator.* Sasa jinsi gani wanafunzi wengi Tanzania wanakosa kusoma kwa ajili ya tatizo la umeme kwa sababu umeme wenyewe ni wa mashaka?

Vyuo vyetu, mafundi vinyozi, mama ntilie wauza maji baridi, kote wanapata matatizo katika suala zima la uchumi kutokana na suala zima umeme kwamba haujakuwa *stabilised* na ufumbuzi huu utapatikana na suala zima na sekta ya gesi ikiweza kuwa imara katika nchi yetu, kwa sababu tunajua umeme wa gesi ndiyo umeme tunaoupata kwa bei nafuu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nadhani maazimio yametoa kwamba *CAG, TRA* waweze kuangalia jinsi gani Serikali inapata mapato. Ndugu zangu nchi bila mapato hatuwezi kwenda na ningeliomba sana Serikali, mchakato huu uende kwa haraka na watu waliopewa dhamana, waangali jinsi gani waweze kufanya kazi kwa umakini wa hali ya juu. Lakini nimuombe Mwanasheria wetu wa Serikali, nimesikia kwamba kutakuwa na *negotiation team*, mimi sijajua jinsi gani timu hii itaweza kufanya kazi vizuri zaidi na ikakoswa kubanwa vizuri zaidi.

Ingewezekana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali moja kwa moja ingewajibika katika hili, ingetusaidia sana. Kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndiye mwenye dhamana kubwa sana, angeweza kutusaidia ilimradi kwamba Taifa letu tuone rasilimali za nchi yetu na wale wote kama kuna mikataba mibovu ambayo haijakwenda vizuri iweze kwenda sawa. Lakini suala zima ni la uwajibikaji.

Kwa mujibu wa taratibu ilivyoonyesha katika mchakato mzima ni kwamba kuna watu kabisa wana makosa ya jinai. Mimi naomba kama nchi yetu na kama Bunge, watu hawa watakaobainika kabisa wapelekwe Mhakamani. Hii itasaidia sana katika suala zima la kukuza nidhamu ya utendaji wa Watendaji wetu. Hili kwa kiwango kikubwa ni kwamba tutaweza kumfikia Mtanzania mnyonge kabisa aliyekuwa chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ningelipenda kukupongeza kwa kunipa fursa mchana huu wa leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lugola.

**MHE.ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ninaomba mwongozo wako. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anawasilisha taarifa ya utekelezaji wa ripoti hii ya Kamati yetu, kwenye lile Azimio Na. 4 linalohusu kusitishwa kwa mkataba amezungumzia kuundwa kwa *Government Negotiating Team*, lakini kwenye Azimio Na. 18 naomba nimnukuu. Anasema: kukosekana kwa Sera mahsusi, sheria na mpango kabambe (*Gas Master Plan*) wa gesi asili ninaomba mwongozo wako kama Serikali inaweza ikaunda *government negotiating team* bila kuwepo Sheria au Sera ambapo wao wana-*base* katika kwenda ku-*negotiate.* Nilikuwa naomba mwongozo wako kama inawezekana kufanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wewe Mheshimiwa Lugola, mbona jioni unachangia? Sasa jioni utachangia nini? Kwa hiyo, utachangia wakati utakapoitwa jioni. Kwa hiyo, kwa sasa hivi nasitisha shughuli za Bunge kwa sababu dakika zenyewe hazitoshi kwa wengine, tukirudi hapa saa 11.00 Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu atakuwepo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa

Kabwe Zitto, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Lakini nitaanza na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola ili aeleze hayo anayoeleza, maana yake huko ndiko kujadili kwenyewe sasa. Ukiniuliza tena kujadili kwenyewe, nijibu nini sasa? Huko ndiyo kujadili kwenyewe. Nashukuru sana.

Waliojadili asubuhi wamejielekeza sana kwenye taarifa ya Serikali na maoni ya Kamati, naomba iwe hivyo. Tusifumue habari nyingine zozote nje ya ile kwa sababu *otherwise* tutakuwa tunajadili mara ya pili. Lakini nawashukuru hawa walioanzisha asubuhi, wamefanya vizuri. Kwa hiyo, na nyie niliyowataja mjiandae kwa mtindo huo.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge asubuhi nilikuwa nimewataja watu ambao watachangia. Nitaanza na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola na aeleze vizuri hoja yake ile halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Felix alikwishaongea na Mheshimiwa Mariam Kisangi. Mheshimiwa Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nikiwa mtu wa kwanza kabisa kutoa mchango wangu kwenye Taarifa hii ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwenye hii sekta ndogo ya gesi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Kamati yetu ya Nishati na Madini kwa kuibua haya mambo ambayo kwa kweli kama yatafanyiwa kazi kwa dhamira ya Serikali yetu basi sekta ndogo hii ya gesi itaweza kutuletea uchumi mzuri na hivyo kutatua matatizo mengi yanayowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu pia kwamba naishukuru Serikali inayowasilisha taarifa yake juu ya Maazimio haya na kama Serikali isingeleta taarifa hii nadhani sisi Wabunge nikiwemo na mimi tusingekuwa na jambo la kusema. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa sababu imetupa mahali pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kuungana na wenzangu ambao kwa kweli wana *concern* ya namna gani ambavyo Serikali yetu imekuwa *slow* katika kutekeleza Maazimio ya Bunge lako Tukufu nikianzia kwenye lile Bunge la baada ya uhuru lililokuwa likijulikana kama Baraza la Kutunga Sheria *(LEGICO)* na baadaye tukapata Bunge letu la Tanzania na leo ni Bunge la Kumi. Yako Maazimio mengi sana ambayo yamekuwa yakitolewa na Bunge lakini utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua, Serikali imekuwa haionyeshi dhamira ya dhati ya kutekeleza Maazimio haya.

Mheshimiwa Spika, mimi katika eneo hili la utekelezaji wa Maazimio ya Bunge naamini ndiyo njia pekee itakayoleta ufanisi Serikalini, ndiyo njia pekee ya Bunge kuisimamia Serikali yake lakini kama Maazimio hayatekelezwi kwa namna ambayo Wabunge tunashauri, naamini mambo yataendelea kuwa yaleyale ya kuifanya nchi hii kwa upande wa rasilimali zake kuwa Shamba la Bibi. Katika hili ninakusudia na nitaomba Idara yetu ya *Hansard* pamoja na *Research* wanitafutie Maazimio yote ya Bunge ambayo yalitolewa toka tumepata uhuru kwenye *LEGICO* mpaka Bunge hili la Kumi ili niweze kuona ni Maazimio yapi ambayo Serikali yetu hii haijawahi kuyatekeleza ili tuiulize ni kwa nini haijatekeleza Maazimio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, moja kwa moja niende kwenye Azimio Na.12. Mimi nimeshindwa kuelewa na sikubaliani na sababu ambazo Serikali imezitoa hapa kwenye Jedwali la Utekelezaji kuhusiana na hawa *Pa-African Energy* ambao wamekwapua hizi dola 28.1 fedha ambazo ni za Serikali na ni za Watanzania. Kwa nini nasema sikubaliani na utekelezaji wa namna hii?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mtu ambaye amekiri kabisa kwamba hizi dola 28.1 amezichukua, amezikwapua, tena kwa mtindo ule wa ubadhirifu kwa maana ya *fraud* lakini leo Serikali inasema wataunda *Government Negotiating Team.* Labda kama ni Tanzania, duniani utatembea utamaliza nchi zote huwezi ukaenda ku-*negotiate* na mwizi. Unaenda ku-*negotiate* naye kitu gani?

Mheshimiwa Spika, hivi kweli umesikia kuku analia kwenye banda kule 'kruu, kruu', unakwenda unamkuta mtu ametembea hatua tano akiwa ameshikilia kuku. Akakiri kwamba huyu kuku nimekuibia, halafu ukamruhusu aende naye baadaye ukaunda timu ya familia yako kwenda ku-*negotiate* na yule mwizi. Mimi sijawahi kuona. Huu ni wizi wa dhahiri, lazima watu hao wachukuliwe hatua kuanzia leo, kuanzia sasa. *Government Negotiating Team*, inaenda ku-*negotiate* nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nirudi kwenye hiyo *Negotiating Team.* Kama nilivyosema mchana, ukiangalia lile Azimio la 18 ambalo limekuwa na mambo mengi ambayo Kamati yetu imetuambia pale mwishoni kwamba Kamati inaishauri Serikali kuwawajibisha Viongozi Wakuu na Watendaji waliohusika na uzembe huu na kuteua wengine wenye uwezo haraka iwezekanavyo. Suala kama hili na lenyewe huku limeambiwa kwamba linaenda kwenye *Government Negotiating Team* kwa sababu wamesema yote haya yanaenda kwenye Hadidu za Rejea.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo nataka Serikali inipe maelezo. Leo hii ningeweza kusema hapa, 'kitendawili, tega' na nikauliza ni nchi gani duniani hapa katika kitendawili, ambayo ina uwezo wa kwenda kuwekeza kama Kampuni lakini hiyo sekta unayotaka kuwekeza haina Sheria, haina *Master Plan,* haina Sera mahsusi juu ya jambo hilo? Suala la 'Kitendawili, tega' lingeruhusiwa hapa, Wabunge wangesema ni Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hii inatia uchungu sana. Ninaamini kabisa katika *stage* ya kuingia mkataba na Kampuni ya Uwekezaji hasa kwenye hii sekta ya gesi lazima nako kulikuwa na *Government Negoting Team* ya kwenda ku-*negotiate* kwenye mkataba huu. Sasa hawa walikuwa wanakwenda ku-*negotiate* wakiwa na vitendea kazi gani? Wana-*negotiate,* wakiwa wana-*base* wapi? Hawana Sheria, hawana *master plan* wala Sera ya nchi hii haipo. Kwa hiyo, hainiingii akilini kama leo Serikali inaleta Taarifa ya Utekelezaji, wanatuambia tena kuna *Government Negotiating Team*. Wanaenda ku-*negotiate* wakiwa wana-*base* wapi kuhusiana na mambo haya ya gesi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi sikubaliani kabisa na maelezo haya na namna ambavyo Serikali imeleta Taarifa yake ya Utekelezaji na wakati huohuo pia mwezi wa nne ndipo hawa wa *Government Negotiating Team* tumeambiwa kwamba wataleta ripoti yao Bungeni na wakati huohuo pia ndipo ambapo Sheria hii ya mambo ya gesi tunarajia pia ije Bungeni. Sasa nashindwa kuelewa vita-*tally* vipi kuhusiana na mambo haya.

Mheshimiwa Spika, niende Azimio la 4. Azimio la 4, utekelezaji wake mimi umenishtua sana. Kwanza Kamati yetu katika Azimio lake ilisema *PanAfrican Energy* walikosa sifa za uaminifu. Sasa kampuni ambayo siyo waaminifu, tunachekacheka nayo ya nini? Kampuni ambayo siyo waaminifu, hata sisi katika hali ya kawaida, nyumbani kwako kama mtoto wako hana uaminifu, unapomtuma sokoni au dukani harudishi chenji hutamtuma tena. Sasa mimi nashindwa kuelewa Serikali inapotumia maneno itazingatia taratibu, itatafakari, kwa umakini, inatafakari vitu gani ambavyo Kamati imeshasema kampuni hii si waaminifu? Wanataka vitu gani waambiwe ili waone kwamba Kampuni hii ni kampuni ambayo inaiba fedha za Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kama kampuni hii ingekuwa ni ya Wazungu, taarifa nilizonazo ni kwamba ni ya Wazungu, mimi siamini. Wazungu gani hawa ambao mpaka leo hawataki kutupa fedha zetu dola za Kimarekani 28.1? Wazungu gani hawa? Halafu ni Wazungu gani hawa ambao mpaka leo hawataki na wamekaidi kutoa maelezo ya dola za Kimarekani milioni 36, Wazungu gani hawa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Wewe shida yako Wazungu wawekezaji? *(Kicheko)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, hata mtu mweusi anaweza akawa mwekezaji lakini sasa mimi naamini hawa siyo Wazungu hawa tunaowafahamu. Kampuni hii tuiangalie vizuri. Maelezo yote yaliyozunguka katika utekelezaji juu ya kampuni hii na suala hili ni la kusitisha mara moja, mkataba ambao umegubikwa na matatizo na matatizo mengi ni yale yaliyofanywa na kampuni yenyewe ile ya *PanAfrican Energy,* wametuibia hela mpaka sasa hawajatoa maelezo ya dola za Kimarekani milioni 36 lakini bado tunasema sisi tupeleke *Government Negotiating Team*, tunaenda ku-*negotiate* na watu waliotuibia, tuna-*negotiate* nini?

Mheshimiwa Spika, nimalizie pale kwenye Azimio Na.22. Azimio Na.22 linahusu fedha ambazo wabia wa *TPDC* wana-*contribute* na inasemekana kwa mwaka mmoja ni shilingi bilioni tatu za Kitanzania kwa ajili ya mafunzo ili tuweze kupata Watanzania ambao wana ujuzi, wana *skills* juu ya mambo ya gesi. Cha ajabu kwenye Azimio hili, asilimia 50 ya bilioni tatu za Kitanzania zinachukuliwa na Wizara ya Nishati na Madini, wanazichukua wanazipeleka wapi? Fedha hizi ni kwa ajili ya ku-*train* Watanzania, *TPDC* kwa ajili ya *skills* lakini bado hatujapata maelezo ya kutosha ambayo yametolewa na Serikali licha ya maelezo ambayo mimi nimeshindwa kuyaelewa. Naomba niyasome kwa ruhusa yako.

*"Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa suala hili halirudiwi tena".*

Mheshimiwa Spika, hizo ni hatua hizo? Hizo ni hatua gani hizo? Naomba nirudie.

*"Serikali imechukua hatua za makusudi ili kuhakikisha kuwa suala hili halirudiwi tena".*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lilitaka kujua juu ya jambo hili, Serikali imechukua hatua gani? Hatua hizo ambazo wamezichukua wazilete hapa tuweze kuziona na kuzijadili. Sasa wao wanasema tu hatua za makusudi, ni hatua gani hizo za makusudi? Labda niseme tu kwamba nchi yetu sasa tufike mahali, tumechoka kufanywa Shamba la Bibi. Kwa kweli Serikali isipokubali ushauri unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge, tena Wabunge wanatoa ushauri huu kwa nia njema kwa sababu ni masuala yanayohusu wananchi wa Tanzania lakini leo Serikali imebaki kupikuana na Bunge, hatutafika. Mimi ninasema kama Bunge hili tutaendelea kukubali taarifa za namna hii ambazo zinatuchezea tu akili, wanatutwistitwisti. Nawaambieni Waheshimiwa Wabunge wenzangu Serikali hii, Watanzania hawa na nchi hii ambayo ina rasilimali nyingi ikiwemo hii gesi, nawaambieni Shule ya Msingi Mranda (A) pale Mwibara, itaendelea kuwa na Walimu wawili kama waliopo kwa sababu uchumi hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule zetu zitaendelea kutokuwa na madawati kwa sababu fedha hizi ambazo hata zingine mwizi tumemwona, mpaka leo Serikali haitaki kumkamata na zile fedha hawazirudishi, kuna nini? Ninawaomba Wabunge wenzangu, chondechonde, nchi hii Watanzania wana hali mbaya sana ya kiuchumi, wana matatizo lukuki, yakiwemo hata hayo mengine tunayoendelea nayo huko, sijui Madaktari wanaomba, hawa wezi wangekuwa wameambiwa hizi pesa warudishe, si tungekuwa kifua mbele katika kujadili kwa sababu tunajua chenji iko. Kama Serikali itaendelea kutuletea Taarifa ya Utekelezaji ya namna hii, hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa mwisho kwa Serikali yangu ya CCM, Serikali ninayoipenda sana, yale yote ambayo Bunge hili, tuanze leo sasa, Maazimio haya ambayo yanawahusu watu ambao wametuingiza mkenge, wametufikisha hapa kwenye Wizara ya Nishati na Madini, Wabunge tusikie watu hawa wamechukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani na namna walivyotekeleza taarifa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest,* mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. Nchi ilikuwa gizani lakini sasa ina ahueni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ngeleja umefanya kazi nzuri, matatizo umeyakabili, naomba ugandamize zaidi na kanyaga moto twende.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita zaidi kwenye Azimio la mwisho, namba 26 ambalo nitalisoma kwa ruhusa yako. Azimio linasema:-

"*Ili kulinda misitu na kupunguza gharama kwa wananchi, Kamati inashauri TPDC iwezeshwe ili kuweza kutekeleza miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye maghala".*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi na kwa mara nyingine tena sasa tuna gesi, baada ya kuwa na madini mengi yakiwemo madini ya *uranium* ambayo na yenyewe bado yanatusubiri

kuyachimba na kufaidisha taifa letu.  Sasa ni miaka tisa takribani kumi hivi toka tuanze kuzalisha gesi mwaka 2004 lakini tunazalisha, tunatumia asilimia tano (5%) pekee ya gesi yetu. Asilimia tano peke yake kwa miaka tisa.  Tanzania ni nchi pekee katika Afrika Mashariki yenye gesi lakini Msumbiji ambao ni majirani zetu nao wana gesi.

Mheshimiwa Spika, kusuasua huku kuwekeza katika gesi, gesi ambayo faida zake ni bayana, faida ya matumizi ya gesi katika uchumi na maisha ya Watanzania na siyo Watanzania, ni duniani kote, faida zake ni bayana.  Kutokana na faida hizo sioni kigugumizi cha Serikali kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika sekta hii.  Kitendo cha Serikali cha kuiruhusu *TPDC* iweze kubakiwa na asilimia 50 ya mapato yanayotokana na mauzo ya gesiasili ili iweze kuwekeza katika miradi ya gesi kwa matumizi, kwa kuanzia wamekopa dola milioni 55 lakini hii ni kwa kusambaza gesi Dar es Salaam peke yake, ambayo tunaambiwa inatumia magunia ya mkaa 40,000 kwa siku.  Mkaa unaotumika nchi nzima hushangai kwa nini nchi yetu sasa ina matatizo ya kimazingira kwa maana ya kukatwa miti hovyo, kwa sababu wananchi inabidi wakate miti kujipatia mahitaji ya kiuchumi na kadhalika. Gesi tuliyo nayo hii, Mungu ametupa ili tunusuru mazingira yetu, tuboreshe maisha yetu kama ambavyo nchi zingine zenye gesi zinavyonufaika na gesi katika nchi yao.  Nchi ya Qatar uchumi wake unategemea gesi peke yake.

Mheshimiwa Spika, nilisoma *internet* jana nikakuta kuna mazungumzo yameanza ya kupeleka gesi Kenya, gesi ya Tanzania kupitia Tanga, yaani Dar es Salaam tunatumia magunia 40,000 ya mkaa kila siku, sisi tunaanza mipango ya kupeleka gesi Kenya, hii haiingii akilini.  Tunataka Serikali iwekeze kiasi kikubwa siyo hiki ambacho wamewapa *TPDC* dola milioni 55, ni hela kidogo sana, waongeze kiasi hiki kwa mara 10 zaidi na hiyo iwe ndani ya muda mfupi. Mwanza, Magu tunataka gesi itumike, sasa hivi wananchi wanapikia miti ya pamba kitu ambacho hakikuwepo zamani, kwa sababu hakuna nishati ya kupikia. Kwa hiyo, nishati hii inabidi tuitumie na tupange mipango yetu ili kuwezesha gesi kunufaisha nchi. Hivi sasa ndio tunaandaa *Gas Master Plan,* miaka 10 baada ya kuanza kuizalisha! Bado Sera na Sheria hatuna.

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza kwamba, pamoja na hizi zote kuandaliwa, *Master Plan,* Sera, Sheria, inabidi pia tuwe na Sheria ya kusimamia mapato na matumizi ya fedha zitakazotokana na gesi asili; yaani *Gas Revenue Management Bill.* Hili nitakuja kupendekeza pia kwenye *Uranium.* Nchi nyingine zenye madini asilia, zenye *extractive industries* zina *Bills* hizi na zinadhibiti matumizi na mapato kwa ajili ya manufaa ya nchi. Hili nitakujanalo baadaye, sio mahali pake, lakini nitakuja kupendekeza tuwe na *Gas Revenue Management Bill.*

Mheshimiwa Spika, naomba tuangalie upya mipango yetu ya kiuchumi ili tutoe kipaumbele zaidi kwenye gesi. Faida za gesi ni nyingi, nitataja chache tu; kufua umeme, kuendesha magari, nishati viwandani na matumizi haya yote matatu yanapunguza matumizi ya mafuta ya petroli na hivyo kuimarisha shilingi ya Tanzania kwa sababu, *import* ya mafuta ni kubwa sana. Hatuta-*import* mafuta kutokana na kufua umeme kwa gesi, kuendesha magari kwa gesi na nishati viwandani.

**SPIKA:** Na mbolea bwana inatengenezwa.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, na mbolea!

**SPIKA:** Eeh na mbolea pia inatengenezwa na gesi.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, na viwandani kama malighafi kutengeneza mbolea. Pia itachangia sana kuongeza mapato ya Serikali ya ndani pamoja na fedha za kigeni kupitia mirabaha, kodi, tozo mbalimbali na uuzaji gesi nchi za nje baadaye tukishaanza kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, mipango inayofanywa hivi sasa na Serikali ambayo imependekezwa katika utekelezaji kwenye Azimio Namba 26, ya kuanzia Dar-es-Salaam peke yake, mimi napingana nalo. Huu ungekuwa ni mpango wa mwaka mmoja ili mwaka kesho tuone zoezi hili linasambaa katika miji mingine. Tuone zoezi hili linasambaa katika miji mingine, la kuongeza matumizi ya gesi kwa matumizi ya majumbani, viwandani na kwenye magari. Mpaka sasa ni magari 31 tu ndiyo yanatumia gesi! Kuna kikwazo gani kuwekeza fedha ili magari yetu mengi yatumie gesi ambayo tunayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu alitazame upya. Pamoja na kwamba *TPDC* uwezo wao wa *Manpower* ulikuwa umepungua na sasa wanaajiri na wana mpango wa

kuajiri watumishi 190 na hilo lifanyike haraka na iongezewe uwezo. *TPDC* ifanye mambo makubwa katika muda mfupi iwezekanavyo kuinusuru nchi yetu na umaskini, kuokoa mazingira ya nchi yetu pamoja na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka nichangie kwenye Azimio hili. Niko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Waziri na Wizara na Katibu Mkuu ambaye nampongeza kuteuliwa na Rais; ni Mtendaji shupavu namfahamu, naamini kwamba, sekta itaenda mbele kwa kuwa, yeye ndiye usukani katika mambo ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi mchango wangu ulikuwa huo. Naomba Mheshimiwa Waziri, kama ni *concentration* pamoja na mambo mengine, sukuma nguvu zako kwenye gesi ili nchi yetu inufaike ili ndani ya miaka mitano hii, tuone hatua kubwa unazozipiga. Nchi kama Bangladesh imenufaika, mimi nimesoma Bangladesh mwaka mmoja, ukiingia kwenye nyumba unafungua gesi kama unavyofungua maji! Hawana matatizo ya kuni za kupikia, sijui mkaa!

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nisigongewe kengele, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu utekelezaji uliowasilishwa na Serikali juu ya sekta ndogo ya gesi asili ambayo Maazimio yake yalitolewa na Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mawazo yangu, napenda na mimi ku-*declare interest* kwamba, ni Mjumbe wa Kamati hii ya Nishati na Madini na vilevile ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo na pia mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ambayo ilikuwa inachunguza sekta hii ya gesi asili kwa kipindi cha miezi miwili huko Dar-es-Salaam. Kwa bahati mbaya sana hata juzi walipoleta Taarifa, wenzetu wa Wizara, mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti kwa sababu Mwenyekiti wangu alikuwa Kigoma kwa shughuli za Chama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nianze na pongezi. Kwanza nalipongeza Bunge hili kwa jinsi ambavyo waliipokea Taarifa hii na wakaijadili kwa kina na mpaka ikaleta matunda mpaka hapa tulipofikia. Vilevile niipongeze Serikali, kupitia Mheshimiwa Lukuvi, wakati tunawasilisha Taarifa hii alikiri ndani ya Bunge kwamba, Taarifa hii iko vizuri na wameipokea na wanaenda kuifanyia kazi. Haya mambo, yaliitia faraja sana Kamati yangu kwa sababu walifanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niipongeze Wizara kwa jinsi ambavyo walipokea Maazimio yetu 26, Maazimio yote mazito ambayo yalihitaji majibu ya kina ndani ya Bunge hili. Kwa jinsi walivyowasilisha, kwa kweli mimi kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, nimeona wamejitahidi kwa kiasi kikubwa sana kulingana na tulikotoka! Mambo yalikuwa mengi, ubadhirifu ulikuwa mkubwa lakini hakuna jambo jema kama mwenzako unapomuambia jambo halafu anakubali na si kukubali tu, anakubali kujisahihisha! Hili ni jambo la kiungwana. Kwa hiyo, mimi nimefarijika sana kuona Mheshimiwa Waziri alichukua Maazimio yetu kwa uzito wa pekee, pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu mpya, ndugu yetu Eliakim Maswi na mpaka wamekuja kuyatolea majibu kama walivyowasilisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze sana Katibu Mkuu huyu mpya, kwa muda mfupi ambao nimefanya naye kazi, ameonesha uwezo wa juu sana na kulingana na mazungumzo yake anayoongea mbele ya watendaji wake, imetufanya sisi Wajumbe wa Kamati tujenge imani kubwa sana na yeye na tuna matumaini makubwa kwamba ataisaidia Wizara hiyo kwa kiwango kikubwa. Hivyo basi, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tumpokee huyu Mtendaji Mkuu mpya, tufanye naye kazi, tupokee na mapendekezo aliyotoa, ninaamini kwa muda mfupi yatazaa matunda mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo mimi limenifurahisha ni kwamba, tumemwambia kila mapendekezo yetu watakavyokuwa wanafanya tuwe tunapata taarifa sisi Wajumbe wa Kamati na sio Wajumbe wa Kamati tu, Bunge liwe linapata taarifa. Hivi jamani, ni jambo gani zuri ambalo watendaji watakuwa wanafanya, sisi tunaletewa taarifa na sisi tunatoa maoni yetu, mimi nimeona ni njia nzuri sana ambayo itasaidia Wizara hii kuweza kujinasua kwenye matatizo na Wizara hii kuwa na mchango mkubwa kiuchumi na kuleta maendeleo kwa Watanzania kwa kipindi hiki ambacho tunacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya mapendekezo yetu kupitia majibu ya Wizara, wametueleza kwamba; kwanza sisi tuliwahoji kuhusu wao kuwa mbali na *TPDC!* Kwa nini *TPDC* inahangaika peke yake? Wakati mwingine Wizara ilikuwa inaweza kuunga mkono mwekezaji inasahau hata watendaji ambao ni kiungo chake lakini kupitia mchakato tulioufanya na wao, wamekiri kabisa ulikuwa ni udhaifu na wamekubali kwa nia moja na ndio maana wakawa wameunda sekta ndogo ambayo itasimamia uendelezaji wa sekta hii ya gesi asili.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nitoe angalizo pale, ninaomba sana hiki kitengo kidogo kitakachoundwa kifanye kazi za kisera, wasije wakaingia kwenye kazi za watendaji. Wakiingia kwenye kazi za watendaji, watawachanganya wenzetu wa *TPDC* na kama kutatokea mgongano wa kazi, tutakuwa hatujafanya jambo jema, tutakuwa tumeleta mtafaruku na kuharibu kazi zaidi. Kwa hiyo, hicho kitengo kiende kusimamia mambo ya kisera sio watendaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunashukuru Wizara kwa kukubali kwamba *TPDC* ina upungufu mkubwa sana wa watumishi. Wamekubali na kwa kuanzia Serikali imewapa watumishi 51. Nako tukaona tumepewa heshima kubwa kama Wajumbe wa Kamati na vilevile wale wengine waliobaki Serikali imekiri kabisa itaendelea kulifanyia kazi jambo hili na hatimaye *TPDC* itakuwa na wataalamu wa kutosha. Tuna hakika kwamba, watumishi wakiwa wa kutosheleza katika Shirika la *TPDC* ufanisi wa kazi utakuwa mkubwa zaidi kuliko ulivyokuwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie kuhusu madai ya fedha ambayo wenzetu wa *PanAfrican Energy Tanzania Limited,* ambayo walijirejeshea wenyewe huku wakijua kabisa hela hizo sio zao, ni halali yetu! Mimi nasema, haya hayahitaji tena kuingia kwenye majadiliano! Yako ambayo tumeafiki yaingie kwenye majadiliano, lakini yapo ambayo tunahitaji yatekelezwe mara moja. Shilingi za Marekani milioni 20.1, tunaomba wenzetu wa *PanAfrican* wazirejeshe mara moja. Katika hili, naiomba Serikali iwe na meno. Hawa wawekezaji na wenyewe walikuja kwa shida zao na sisi tuliwakaribisha kwa tabu zetu, kwa hiyo, isiwe kigezo cha kutumia tabu zetu kuanza kutuibia. Naomba Serikali kwa uzito wa pekee iwaagize mara moja fedha hizo zirejeshwe. Hizo sio fedha za majadiliano kwa sababu hata wao walishakiri lakini yale yote ambayo yanahitaji majadiliano sisi kama Wajumbe wa Kamati, tumekubali kabisa yaingie kwenye majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee pia Azimio Na.26, kama alivyoongelea mwenzangu Mheshimiwa Limbu, kuhusu matumizi ya gesi. Ni ukweli usiofichika kwamba, sekta ya gesi haijatoa matunda ipasavyo katika nchi yetu. Uzalishaji wake bado ni duni. Kuna kila sababu ya Serikali kuweka uzito wa pekee kuhakikisha gesi inazalishwa ipasavyo ili matumizi ya gesi yaweze kufika vijijini.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano wa Mkoa wa Singida, Mkuu wetu wa Mkoa amezuia kabisa wananchi kuchoma mkaa kwa sababu wanapoteza misitu mingi sana ambayo inasababisha ukame. Sasa hivi wauza mkaa ukipita barabarani, hawapangi magunia kama zamani. Muuzaji anakaa na kaa moja kwa kuibia, akiona gari linakuja lina bendera, anarudi, anajificha. Akiona magari ya kawaida, anasimama anaendelea na kamkaa kake. Suala hili tutaendelea nalo mpaka lini? Mimi naamini, kama uzalishaji utaleta tija, matumizi ya gesi yakafika vijijini, akina mama watapika kwa gesi, wataachana na masuala ya mikaa ambayo kwanza inaleta moshi ndani ya nyumba na ni sumu kabisa kwa watumiaji na bei itakuwa imeshuka kuliko ilivyo sasa hivi. Kwa hiyo, naomba sana sekta hii ipewe umuhimu wa pekee ili iweze kuleta tija katika nchi yetu kama sekta nyingine zinavyofanya katika kuzalisha mali ya nchi hii na kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa kuwa nilikuwa Mjumbe wa Kamati na mengi yaliyoongelewa na Msomaji wa Kamati, tumeyashughulikia sisi wenyewe, nimalizie tu kwa kuwashukuru na kuwapongeza kwa kutoa heshima kwa Kamati kwa sababu, kama taarifa waliyoileta kutoka Dar-es-Salaam ingekuja hivyohivyo, kizaazaa kingewaka hapa lakini tukaipitia taarifa hiyo kwa pamoja, tumesahihisha kitu kimoja baada ya kingine. Tukiwaambia hivi, wanakubali. Ukiwaambia hivi, wanakubali. Mimi ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niwatakie kila la kheri, hasa Katibu Mkuu huyu mpya, sisi tumejenga imani naye. Moto alioingia nao uwe huohuo ili Wizara hii isiendelee kuwa gumzo kwenye magazeti. Tumechoka kusoma magazeti yenye kueleza habari ya Nishati na Madini kila siku. Tunataka magazeti yaandike habari

nyingine, sio habari za Nishati na Madini na hii kuandikwa-andikwa itasitishwa tu kutokana na tija katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, namalizia kwa kuunga mkono maelezo ya Wizara kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia katika suala zima la gesi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nitoe pongezi zangu kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kufanikisha suala zima la umeme wa dharura. Jambo la kweli likifanyika katika Serikali, lazima tupongeze. Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana katika kutekeleza mpango mzima wa kutafuta umeme wa dharura. Nchi yetu iligubikwa na giza kubwa sana, jambo ambalo lilikuwa kero kwa wananchi lakini baada ya Serikali kukaa na kutafakari, walipanga mipango ya umeme kupitia kwenye Kamati na kuchukua maoni ya Wabunge; mipango ile mimi nasema imefanikiwa kwa 80% au 90% kwa sababu, umeme sasa upo.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda tena nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara na Watendaji wake. Naomba nitoe tena shukrani kwa Kamati Ndogo ya Bunge ambayo imeshughulikia suala zima la gesi. Kwa kweli Kamati Ndogo hii, pamoja na mimi ni Mjumbe wa Kamati lakini, naipongeza kwa jinsi ilivyowajibika katika kufuatilia suala zima la gesi mpaka wanakuta kuna upungufu kadha wa kadha. Hongereni sana Kamati Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipongeza Serikali yangu na hasa kwa kununua mitambo mingi ya umeme na mingine kukodisha kuondoa shida hiyo, mitambo ya umeme ambayo imenunuliwa au imekodishwa, tuna mitambo ya *AGGREKO, JACOBSON, IPTL, SYMBION,* ni mitambo mingi kweli imenunuliwa. Changamoto ambayo inaikabili mitambo hii ni kwamba, inatumia mafuta mazito ya *jet* na dizeli. Kwa kweli, gharama za mafuta ni kubwa katika uendeshaji wa mitambo hii. Mkombozi wa mipango hii ni gesi kama itapatikana kwa wingi. Iwapo sekta hii ya gesi itaboreshwa vizuri na gesi ikapatiakana kwa wingi basi manufaa makubwa sana yatakuja kwa Watanzania kwa sababu, hata hii kero ya kupandisha *tarrif* za umeme itapungua. Umeme wa kutumia mafuta una gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu kwanza, iiangalie sekta hii ya gesi kwa unyeti wa aina yake ili kusaidia maisha ya Watanzania kwa kuondokana na gharama kubwa za umeme vinginevyo itakuwa ngumu kwa sababu umeme maji sasa hivi umekumbwa na utata wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa hii ya Wizara ya Nishati, mimi nitachangia katika Azimio Namba 12, 15 na 26.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio namba 12, *TPDC* imepewa kibali cha ajira, nashukuru Wizara imelifuatilia kwa umakini wake jambo hilo kuwapatia *TPDC* kibali cha ajira. Niombe kwenye ajira hizo waangalie utaalam zaidi kwa sababu ndani ya *TPDC* katika miaka miwili, mitatu ijayo kutakuwa na wastaafu wengi sana ambao ndiyo wanaotegemewa na Serikali na ambao ndiyo ambao wanaijua sekta hiyo ya gesi. Sasa tutakapochagua watu wa kuingiza, tuingize mapema na tuwaingize vijana ambao wataanza kufanya mazoezi huko ndani ili kuitambua vizuri sekta hiyo tupate wataalam endelevu wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kulichangia hilo Azimio Na.12, kwa mawazo yangu naona hata hao 51 waliopewa ni wachache. Serikali ingejitahidi tukapata hata ajira mia kwa hatua ya kwanza ili waende katika maeneo mbalimbali, kwa sababu sekta ya gesi tumeiona chanzo kingine cha kufanyiwa utapeli ni upungufu wa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta hii inakosa hata wale Wakaguzi wa Ndani ambao wangewezesha kutambua huu utata ambao unajitokeza wa kupoteza mabilioni ya shilingi katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba nichangie Azimo Na.15 ambalo *TANESCO* ilikuwa inasikitika kwa mikataba tata ambayo inafanyiwa. Kwa kweli jambo hili liliniuma sana, *TANESCO* imeingia

mikataba na *PanAfrica* na Songas wa kununua gesi na mkataba wao unaeleza wazi kwamba iwapo gesi haitapatikana wao watagharamia gharama za mtambo huo kuuendesha kwa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale ilipotokea utata wa visima vya gesi, visima vile vikafungwa, *PanAfrica* akiulizwa sasa hebu toa mafuta uliyoahidi kwa ajili ya mitambo ile, anamrushia *Songas*, Songas anamrushia *PanAfrica*, matokeo yake hakuna wa kumwadabisha, matokeo yake walioadabishwa ni wananchi wa Tanzania kwa kuachwa kwenye giza ghafla jambo ambalo lilisababisha minong'ono na maneno mengi, kumbe waliosababisha ni wao. Mkataba wao unaeleza wazi iwapo gesi itakosekana, ile mashine ni *duo*, ina *operate* kwa gesi na kwa mafuta na waliyakubali yote ili wao wajipatie fedha. Baada ya kupata fedha, sisi tunateseka na giza, wao hawakuona haja sasa ya kurudi nyuma kuangalia ule mkataba wao na kuweza kutupatia mafuta kuendesha mitambo hiyo. Mimi nasema tabia hiyo waache mara moja, Watanzania tunaelewa na tunajua sasa, Watanzania tumeelimika na tunafuatilia kwa kina mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walikuwa wanaona wao kuna watu wa kuwaviringaviringa, sasa hawapo, wanafunzi wapo kwenye Vyuo Vikuu wanasoma na wanaangalia nchi yao inafanya nini. Kwa hiyo, niwaombe haya mambo yasitokee tena, haya ya ukiukwaji wa mikataba kwa yale masuala ambayo wamekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niliongelee Azimio Na. 26 ambalo linaeleza mpango mzima wa usambazaji wa gesi katika Jiji la Dar es Salaam. Naomba niipongeze Serikali kwa mpango huu mzuri. Kwa kweli mpango huu ni nafuu na ni maendeleo makubwa kwa wananchi wa Dar es Salaam na pale itakapoendelea katika Mikoa mingine itakuwa maendeleo kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze na kuishukuru sana Serikali kwa sababu Mkoa wa Dar es Salaam peke yake unatumia zaidi ya magunia 40,000 kwa siku, kwa mwezi karibu magunia milioni 1,200,000, kwa kweli tunamaliza mazingira kwa kukata miti hii. Niombe Serikali iweke umuhimu wa kipekee katika suala hili kwa sababu Dar es Salaam ina mahitaji mengi ya gesi ya viwanda, ya majumbani, mahospitalini na mashuleni. Kwa kuwa mradi utaanzia pale Ubungo, nina imani kubwa mradi huu utaenda moja kwa moja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vyakula vya wanafunzi wale vitakavyopikwa kwa kutumia gesi vitatayarishwa kwa gharama nafuu, wanafunzi wetu wa Chuo Kikuu angalau watanunua vyakula kwa gharama nafuu kidogo.

Mheshimiwa Spika, pia nishukuru kwa kuona unyeti wa Mji wa Dar es Salaam. Kwa kweli Mji wa Dar es Salaam una unyeti wa aina yake kwa sababu una changamoto za aina nyingi sana. Tunavyo vyuo vinavyozunguka eneo la Ubungo, Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo cha Ustawi wa Jamii cha Kijitonyama na mojawapo ya changamoto za wanafunzi na kuyaona maisha magumu ni gharama za chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chakula kile kinapikwa, kama sasa hivi gunia moja la mkaa ni shilingi 50,000 itakapokuja ile gesi, nina imani gesi ya shilingi 50,000 mtu anaweza akatumia kwa mwezi mmoja. Niiombe Serikali yangu ijitahidi sana kuwekeza kwenye mradi huu. Mradi huu una unyeti wa aina yake, ni mradi ambao unatengeneza faida, kama mtu atawekeza kwa dola za kimarekani milioni 55 na ikaleta faida hiyo kwa dola za kimarekani takribani milioni 85, kwa kweli huu ni mradi ambao ni mzuri, uko hai, maendeleo yake yanaonekana moja kwa moja, si mradi ambao utapoteza. Niiombe Serikali kama wameliona hilo basi kuanzia leo watafakari waone jinsi gani wataisaidia *TPDC* waweze kuimarisha mradi wao huu na wananchi wa Tanzania waweze kufanikiwa kupata urahisi wa maisha kwa kutumia gesi katika mitambo ya umeme, majumba, mahospitali na viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Murtaza.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu hivi sasa…

**SPIKA:** Atakayefuata ni Mheshimiwa Zitto maana naona ananiangalia kwa jicho... *(Kicheko)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze sana Kamati ya Nishati na Madini kwa kuweza kufikiria na kuona ni jinsi gani maslahi ya Watanzania yanavyopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hukufanya kosa kumteua Mwenyekiti kijana na Kamati hii imejaa vijana ambao wanaonyesha kabisa wana nia na dhamira ya dhati katika kuikomboa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati anachangia Mheshimiwa Dkt. Limbu hapa alisema 'ndugu yangu Ngeleja endelea kukandamiza' na mimi nasema Ngeleja ukifanya mchezo na Maazimio haya tutakundamiza wewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku ambayo hoja hii ilikuwa ikijadiliwa Bungeni, nashukuru nilikuwa mchangiaji wa mwanzo kabisa na sababu zilizopelekea mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo naamini kabisa mimi ni mmoja kati ya wale wahusika wakuu wa jambo hili linalozungumzwa hapa. Gesi hii inachimbwa Kilwa na mimi ni Mbunge wa Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye hoja, naomba tu nianzie kwenye Azimio Na.1 na kwa ruhusu nilinukuu kama ifuatavyo:-

*"Serikali hususan Wizara ya Nishati na Madini itambue kuwa pamoja na TPDC kuwa msimamizi wa sekta ya gesi kwa niaba ya Serikali, lakini Wizara ya Nishati na Madini ndiye mdau mkuu katika mikataba hii…"*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi niseme tu kwamba Wizara ya Nishati imepewa wajibu mkubwa sana wa kusimamia utekelezaji wa nyanja hii ya gesi.

Mheshimiwa Spika, binafsi sina tatizo na Waziri wa Nishati na Madini lakini nina tatizo na yeye katika usimamiaji wake. Mara zote hata kabla ya sisi hatujaingia hapa Bungeni, Bunge limekuwa likiangalia ni jinsi gani ambavyo Watendaji wa Serikali na taasisi nyinginezo wanaacha mianya ya makusudi ili wanaokuja kuwekeza hapa wachukue rasilimali zetu na kutuacha sisi mahali ambapo hatujui wapi pa kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, katika hili, mapendekezo ya Kamati yameainisha bayana na ninamshauri na kumwomba Mheshimiwa Waziri suala hili alisimamie kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, Azimio la pili lenyewe limeainisha jinsi gani tumekuwa tukiibiwa na kampuni hii ya wachimbaji wa gesi ambao wanaitwa wawekezaji. Mimi nasema hawa ni aina tofauti kabisa ya wawekezaji ambao tunawafahamu katika dunia hii. Inaonekana mpaka sasa kuna pesa ambazo wao wenyewe wamekiri na Wabunge wengi wamezungumza hapa, dola milioni 20.1 na bado dola milioni 35 tunaendelea kukokotoa ili tuweze kubaini, tunachelewa nini kuweza kubaini hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siamini kama Mheshimiwa Ngeleja hili anataka nalo vilevile amulikiwe na tochi ili aweze kuliona. Mimi nilidhani katika Maazimio haya yote kwanza angehakikisha kwamba pesa zetu zinapatikana na zinachangia katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kuzungumzia Maazimio yote kwa sababu tangu mwanzoni nilikubaliana na Maazimio mengi, nitakwenda kwenye Azimio Na.9. Azimio Na.9 kwa majibu ya Serikali wameridhia kuanzisha Sheria ya Gesi lakini Sheria hii inakuja kutungwa, hivi ni lini ambapo kama Wizara ama Watendaji wa Serikali wamewahi kuangalia ni jinsi gani wananchi wa Kilwa ambako gesi inachimbwa kwao mpaka leo hii hata senti moja ya Mtanzania haijaingia kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria zetu na ipo *By Laws* ambayo ilisainiwa na Waziri Mkuu aliyepita, tulikuwa tunatakiwa tupate asilimia tatu kwenye gawio la gesi kama *service levy*. Nitapenda leo Mheshimiwa Waziri aniletee majibu, hizi pesa tangu wakati huo ambapo Sheria hii imepitishwa na Bunge hili zinakwenda wapi? Wananchi wa Kilwa kwa nini wasinufaike na uchimbwaji huu wa gesi kama vile ambavyo wananchi wa maeneo mengine ambapo madini mengine yanachimbwa ikiwemo kwao kule, maana huyu Waziri sisi tunawaita hawa ni wajukuu zetu kwa hiyo ataniambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, tukienda kwenye Azimio Na. 26, linasema kwamba:-

*"Ili kulinda misitu na kupunguza gharama kwa wananchi, Kamati inashauri TPDC iwezeshwe ili kuweza kutekeleza miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari".*

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumnukuu Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu ambaye alikumbusha tu kwamba nchi kama ya Qatar uchumi wake wote unategemea gesi zaidi lakini naamini kwa kuwa yeye ni mtafiti aangalie nchi ya Ukraine ambayo haina gesi lakini asilimia 40 ya mapato ya nchi nzima yanategemea na upitishwaji wa bomba la gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunachimba gesi lakini mpaka leo hii tunazungumzia Halmashauri ya Kilwa ambayo watu wake wanaishi katika kiwango cha chini kabisa cha umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe tu, ni aibu na ni jambo ambalo mimi na ninaamini Wabunge wengine wote watalikubali, leo hii tunapoteza pesa zetu za kigeni kuagiza gesi kutoka nje ya nchi hali ya kuwa gesi tunayo hapa nchini, hili ni jambo la ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu, wananchi wa Kilwa tunaomba na tunashauri na tunaitaka Serikali mradi huu wa ujenzi wa kiwanda hiki cha gesi ujengwe Kilwa, tusipate yote japo basi machache na sisi tuambulie kuyapata. Tutakuza ajira, lakini vilevile tutakuza uchumi katika eneo letu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, Bunge hili limekaa na kutoa Maazimio ambayo Serikali imekubali kuyatekeleza kama vile ambavyo Bunge lilikuwa limeazimia. Tunaomba hadithi hii isijirudie, wananchi wamechoka kusikiliza matatizo kila siku tunasubiri mambo ya michakato, tunasubiri mipango, upembuzi sasa tunataka utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kengele imenililia nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa Azimio la Kilwa halimo humu, Azimio la Kilwa lilirukaje humu? *(Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya utekelezaji wa Maazimio ya Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wenzangu walivyozungumza, napenda kuwapongeza sana Kamati ya Nishati na Madini iliyoundwa kwa ajili ya kuangalia suala hili. Siwapongezi kwa kuangalia namna ambavyo mkataba wa *PanAfrica Energy* ulivyotusababishia hasara lakini nawapongeza zaidi kwa sababu wameliangalia suala hili kwa mapana. Maazimio yao yote ambayo wameyaleta, kuna mambo ambayo wameangalia matatizo ya sasa, lakini hawakuishia kulalamika na kuonyesha matatizo, wamependekeza suluhisho na namna ya kwenda kwa siku za usoni. Ndiyo jambo ambalo nadhani ni vizuri sote tuweze kulizingatia kwamba tulalamike lakini tutoe na suluhisho ili tuweze kuona namna ambavyo nchi yetu itakwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuamua kuwa Nigeria ambayo katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita mafuta yao yamewaingizia zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 250 lakini katika kipindi hicho watu ambao wanaishi katika dimbwi la umaskini Nigeria wameongezeka kutoka watu milioni 15 mwaka 1970 mpaka watu milioni 84 mwaka 2010. Pato la kawaida la mtu wa Nigeria, kipato kwa mwaka, katika miongo hiyo mitatu kimeporomoka kutoka dola 984 kwa mtu mmoja mpaka chini ya dola 300 kwa mtu mmoja. Kwa hiyo, nchi yetu inaweza ikaamua ikawa Nigeria.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukaamua Abazaijan, ambayo mji wake wa Bocco, ulikuwa ni mji tajiri sana baadaye ukarudi ukawa mji maskini sana. Kwa hiyo, leo tunaweza tukaamua Kilwa iweze kushamiri, Mtwara iweze kushamiri au tuamue zisishamiri na maamuzi yatatokana na utekelezaji wa Maazimio haya. Bunge hili likiisimamia Serikali, tukatekeleza Maazimio haya ipasavyo maana yake ni kwamba tutaweza kuifanya nchi yetu iweze kufaidika na rasilimali ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo mawili na napenda kuchangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye Maazimio mawili. Azimi la 1 na la 9. Azimio la 1, kuhusiana na usimamizi wa sekta na hapa ndipo ninapoona kuna tatizo kubwa sana na siridhiki sana na majibu ambayo Serikali imetoa na nimekuwa *disappointed* kidogo na majibu ambayo Serikali imetoa na nimekuwa *disappointed* kidogo na *approval* ya majibu hayo ambayo Kamati ya Nishati na Madini imetoa kwa sababu iwapo tutarekebisha eneo la usimamizi wa sekta, matatizo yote ambayo Kamati Ndogo na Kamati ya Nishati na Madini waliyaona, tutaweza kuyatatua na hayataweza kutokea tena. Kwa hiyo, ni eneo ambalo linahitaji marekebisho na utekelezaji wa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi *regulator* wa sekta hii upande wa *upstream* ni Wizara, *TPDC* inafanya kama *agent* wake, lakini *TPDC* hiyo ndiyo ambayo ikitaka kuajiri lazima iombe kibali Utumishi. Hebu tujiulize, *PPF* leo wakitaka kuajiri wanaomba kibali Utumishi? *NSSF* leo wakitaka kuajiri wanaomba kibali Utumishi? Kwa nini iwe *TPDC*? Kwa nini *TPDC* iwe ni shirika ambalo limefungwa? Lolote ambalo wanataka kufanya ni lazima Wizara iamue, kwa nini? Kwa nini mashirika yote ya Umma, na mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma, Mashirika yote ya Umma yaruhusiwe kukusanya mapato yake, kulipa kodi na kutumia fedha zao lakini *TPDC* waambiwe hapana, leteni zote huku halafu sisi tutawapa *OC*. Kwa nini iwe *TPDC*?

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2011, *TPDC* wameambiwa sasa mta-*retain* 50%, kwa nini isiwe *SUMATRA*? Kwa nini isiwe *TCRA*? Kwa nini isiwe *PPF* au *NSSF* au *PSPF*, Benki Kuu na Mashirika mengine? Kwa nini iwe *TPDC*? Hapa ndipo mzizi wa fitina ulipo. Serikali iiache *TPDC* iwe huru, *TPDC* ifanye kazi kama shirika lingine lolote, kama tatizo ni *Establishment Order* ya *TPDC* tuirekebishe iende *Cap.212* au tuwe na *Parliamentary Act* kuifanya *TPDC* iwe huru. *TPDC* isimame imara kama mashirika mengine ya mafuta duniani yalivyosimama imara, huwezi kuwa na Shirika la Mafuta Duniani ambalo ni maskini, unaiona *TPDC* tu. Mimi nirudie msemo wa Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba ukifanya kitendawili, 'shirika gani la mafuta maskini duniani' jibu litakuwa ni *TPDC*. Kwa nini isiwe *Petrol Bras,* kwa nini isiwe *Start Oil* ya Norway? Kwa nini siyo *Petronas* ya Malaysia? Kwa nini iwe *TPDC*? Tumeifunga mikono *TPDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio hili halijatekelezwa ipasavyo, *solution* ya kwenye hili ni kuhakikisha *TPDC* inakuwa huru. Tuna matatizo katika ukaguzi, tulianzisha kwenye Sekta ya Madini baada ya vurugu nyingi za Sekta ya Madini na ninashukuru kwamba aliyekuwa mjumbe wa Sekretarieti ya Kamati ya Jaji Bomani Ndugu Maswi ndiye sasa Katibu Mkuu wa Wizara hii anaweza akasaidia na tunamwambia kwamba aende asaidie.

Mheshimiwa Spika, tulianzisha *TMAA* ile Taasisi ya Kukagua Hesabu za Migodi lakini leo hii tunavyozungumza taarifa ya *TMAA* inaonyesha kwamba wamegundua *Audit Query* za thamani ya dola bilioni 1.7 kwenye Makampuni matano ya Madini nchini kwa mwaka 2009 na mwaka 2010. Dola za Marekani *1.7 billion,* hiyo ni *Audit Query,* hatusemi kwamba ndiyo *final,* makampuni yatajibu, wataangalia yale ambayo ni sahihi lakini naamini katika hayo tutakuta maeneo gani ambayo tulikuwa tunadanganywa, tunaibiwa tukapata pesa zetu. *TPDC* ndiyo ambayo wanafanya kazi hiyo, sasa haiwezekani kwani *TPDC* ni *investor*, *TPDC* ana-*participate* katika sekta nzima ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta kama *shareholder* kwenye *PSA* zote, tukaamua tuwe na *TMAA* kwenye sekta ya gesi na mafuta, kazi yake iwe ni ukaguzi na washirikiane na *TRA* na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuhakikisha kwamba wanaibua vitu hivyo. Naamini kabisa kwamba tukiwa na *regulation* ya aina hiyo itaweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda tuweze kuliangalia ni *reform* ya sekta hii. Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma imeshatoa *report* mara tatu kwamba tufanye *reform* ya *TPDC*, tuwe na Mamlaka ya Mafuta na Gesi kama *regulator* wa *upstream* na *downstream*, sijui kama sasa hivi *EWURA* wanaangalia *downstream* lakini *TPDC* ibakie kama Shirika lingine tu kama nilivyosema hapo mwanzo wawekeze, wawezeshwe na wabakie na fedha zao zote, watozwe kodi *Coorperate Tax,* walipe *VAT*, walipe *Loyalty* lakini mapato yao yote yabakie nayo waende wakawekeze. Ni aibu sana leo Waheshimiwa Wabunge *TPDC* wanapewa *OC* na Wizara. Mapato yote ya gesi nchini mwaka 2010 yalikuwa dola milioni 35, katika hizo ambazo sisi tunapata kama nchi ni shilingi bilioni 17 na katika hizo *TPDC* wanaambiwa chukueni 50% kuanzia mwaka huu wa 2010 na Wizara inabakia na 50%, hizo za Wizara zinakwenda wapi? Zinakwenda kwenye mfuko, zinatumika kwa vitu vingine, watanunua mafuta na kadhalika lakini hakuna *investment*, waachieni *TPDC* hela zote hizi. Tuwabane *TPDC* kwenye kodi, kwenye *Loyalty* na tuwabane kwenye masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la 9, ni *Legal Regime Registration* na Mheshimiwa Limbu amezungumzia hili. Katika barua ambayo Waziri wa Fedha amemuandikia Mkurugenzi Mkuu wa *IMF,* Ndugu Christian Lagai kuhusiana na mpango wa maendeleo wa Tanzania amesema kuna mambo manne ambayo tunataka kuyafanya. Anasema, *discussion in Tanzania on how to position the country to best take advantage of this potential resource, gas resource, have been initiated. One*, tunaandaa *Natural Gas Master Plan*. *Two*, tunaanda *Gas and Petroleum Revenue Management Bill.* Tatu, tuna-*lounge future generation fund which is a very good idea.* Nne, tunafanya *review ya tax regime*.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo mpango wa Serikali ambao umepelekwa kwa *IMF*, Wizara ya Nishati na Madini ambayo inahusika na hili eneo haijatuambia katika maeneo ya utekelezaji. Wanasema *Natural Gas Master Plan by June* lakini hawajaweka *timeframe* hapa. Wanasema *Petrolium revenue Bill by December* lakini hawajatuambia hapa. Hayo ndiyo mambo ambayo mnatakiwa muwaambie Watanzania, wafanyeni japo kwa dakika chache Watanzania waishi kwa matumaini, wajue kwamba kuna mipango ya kuifanya nchi hii iweze kufaidika na rasilimali zake na hii ndiyo kazi ambayo Mawaziri wanatakiwa kuifanya, hii ndiyo kazi ambayo mnatakiwa mlitaarifu Bunge, Bunge lijiandae na Kamati ya Nishati na Madini ijiwekee utaratibu kabisa ndani ya mwaka huu *Gas Master Plan* Serikali wahakikishe imekamilisha. *Petrolium and Revenue Bill* iwe imekamilika, *Future Generation Fund* iwe imekamilika *by the time master massive gas* inaanza kuwa *exported* Mtwara, tumekaa vizuri na Mtwara isiwe Lagos, wala isiwe Bacco lakini Mtwara iwe kama Oslo, ifaidike na rasilimali ya mafuta, Kilwa pia ifaidike na rasilimali ya mafuta na haya mambo yote ni kiasi cha kuyapanga na kuyaweka vizuri. Hizi *registration* naomba ziangaliwe na tuweze kuzifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Azimio Na.6, Serikali inasema imewaomba *CAG* wasaidiane na *TPDC* kwa ajili ya kukagua hizi *Production Sharing Agreements*. Mheshimiwa Cheyo amezungumza kuhusiana na *role* ya *CAG* na kumwomba kuagiza na kadhalika na kwamba anadhani kuna haja ya kufanya *amendment* kwenye *Audit Act* ili taarifa yoyote ambayo *CAG* ameifanyia *Audit* iweze kufika Bungeni. Jambo la msingi hapa ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba leo hii ukichukua *Auditors* wa *CAG* ukawaweka *TPDC* kushirikana na *TPDC* ku-*audit,* nani anakuwa *External Auditor?* Kwa sababu *CAG* ndiye *External Auditor wa TPDC, CAG* akishashiriki katika *Audit* ya kwanza atakayekuja ku-*oversee* na kuona *audit* hii ni nani? *Solution* ni moja, wala tusitafute majibu ya mkato, nendeni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nendeni *Dodoma University,* nendeni kwenye vyuo vyote vinavyo *train* Ma-*Accountant,* chukueni *the best brains* vijana wa Kitanzania, tumia fedha za mafunzo ambazo makampuni ya mafuta yanaipa *TPDC* wapelekeni vijana kusoma *the best schools in the world,* waende wakafanye kazi ya ukaguzi. *CAG* atakuwa na kitengo chake pale atakwenda kuangalia zile kazi kama zimefanyika na ataleta *report* kwenye Kamati za Bunge ambazo zinahusika ama ni *PAC* au ni *POAC* na vilevile Kamati ya Nishati na Madini ili tuweze kuangalia sekta kwa ujumla, tusitafute *shortcuts*, wapeni pesa *TPDC*, wa-*train* Watanzania tuweze kumiliki rasilimali zetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid halafu msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi na vilevile niishukuru sana Kamati na Wizara kwa kazi waliyofanya pamoja na kwamba tuna kazi kubwa mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kusema mambo mawili ya jumla, kwamba uchumi wa nchi yetu sasa hivi umeelekezwa sana katika sekta hizi mbili yaani ya *Energy* pamoja na *Mines*, ukiangalia kitabu cha Benki Kuu cha Hali ya Uchumi Tanzania, utaona sekta hizi zinavyochangia pato la Taifa lakini kwa bahati mbaya pato hili la Taifa bado halijamfikia Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa la kwanza ambalo naliona lipo, tukijiuliza humu ndani kwamba je, tunayo sera inayotuelekeza juu ya namna ya matumizi ya *industrial minerals* tulizonazo Tanzania, jibu litakuwa hakuna. Kwa hiyo la kwanza ambalo mimi naliona ni tatizo la msingi na haya matatizo bado tutaendelea kukumbana nayo, ni kukosekana kwa sera inayotueleza kwamba madini ya viwandani au rasilimali zenye kutoa *energy* bado hazijakuwa na utaratibu mzuri wa kisera kuweza kuzisimamia vizuri na ndiyo maana leo

tunakuja hapa tunaambiwa kuna Sheria fulani lakini hatuna mfumo maalum wa kusema hizi ni *industrial products* zinatakiwa zisimamiwe na nchi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya haya ni kwamba Taasisi tulizoziunda kufanya kazi hiyo kama *NDC, TPDC, STAMICO* na kadhalika, zote unakuta zinafanya kazi kama Idara za Serikali, hakuna popote duniani ambapo una rasilimali kubwa kama hizi halafu Taasisi zinazotakiwa kusimamia zinakuwa *treated* kama Idara za Serikali. *NDC* ilifika mahali ilitaka kubinafsishwa na hatimaye ikaachiwa tena iliporudi rasilimali zake nyingi zikachukuliwa na kuuzwa, ilianza hata mishahara ikawa hawana, wanaingia kwenye ubia, hawajui rasilimali walizonazo. Hali hiyohiyo imewakuta *TPDC* mpaka majengo yao mengine imebidi kugawiwa kwa *NSSF* na wengine. Sasa nasema, utaratibu huu bado ndiyo tatizo la msingi ninaloliona ambalo linahitaji kuwa *addressed* na Serikali ili tuweze kulinda rasilimali zetu, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, sina hakika kama Serikali inafahamu kwamba nchi nyingi duniani hasa zetu sisi, Serikali nyingi zimeanguka au kuendelea kulipa madeni yasiyokwisha katika sekta ya *energy*, ni sekta ambazo kila siku utakopa na kila siku utalipa mpaka siku ya mwisho wa dunia kama hamkujipanga vizuri na ndiyo sekta mataifa makubwa yanayopigania, China na Marekani wanapigania sekta ya *energy*, Warusi na Wa-European wanapigania sekta ya *energy*, ni vita kubwa sana, kwa hiyo, Serikali ni lazima iwe makini katika kujipanga kwake, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma nakumbuka tulipokuwa na *Wiliamson Diamond* tulikuwa na chuo lakini leo tukiuliza kwenye makapuni ya gesi kuna *any training centre* ya Watanzania? Pamoja na mikataba inasema ufundishe Watanzania lakini je, kuna chuo kinachofundisha Watanzania? Hakuna! Kwa hiyo, urithi wa Tanzania kujua rasilimali za nchi, urithi wa Watanzania kujua namna ya kusimamia rasilimali haupo kabisa na hauwezi kupatikana kwa sababu hakuna *institution* ndani ya migodi yenyewe inayotoa *training*. Tulikuwa na Mwadui lakini sina hakika kama inaendelea, nafikiri imekufa na kadhalika. Tunategemea bado vyuo vyetu vikuu na nadhalika lakini pale kwenye migodi yenyewe pakiwa na chuo, wanafunzi wanapata taaluma tofauti na yule aliyepo chuoni ambapo hakuna mgodi. Hii ni taaluma ambayo lazima tuifanye na kuisimamia. Hilo ndiyo tatizo moja ambalo mimi naliona kwa jumla na nilitaka nilizungumze.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye Maazimio. Mimi nirudi kwenye Azimio la 1 na la 2. Kwanza katika suala zima la kukokotoa *interest*, mimi nilitegemea katika taarifa hii katika kipindi chote hiki angalau tungeambiwa riba inayotakiwa kulipwa hapa ni kiasi gani, siyo leo tena tunarudi kwa *CAG* kuangalia riba italipwa kiasi gani. Kwa hiyo, hii 20.1 *million* tunayoizungumza hatuja-*calculate* riba mpaka leo, tunakuja ku-*calculate* riba lini? Kwa hiyo, huu nasema ni upungufu mkubwa ambao tunao, kile tunachokidai lazima tukidai kikamilifu ili tujue hasa kama Bunge ni kiasi gani tunasimamia mapato yetu na riba kiasi gani inatakiwa kulipwa lakini hiyo haimo ndani ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni la *TPDC* kuwezeshwa kupewa *a hundred percent*. Kwanza nakubaliana nalo kabisa lakini lazima nikubaliane na wenzangu kwamba kuna hitaji kabisa kuiangalia kwa upana kabisa sekta ya gesi. Kwa taarifa za Serikali ni kwamba nchi yetu inaweza kuwa ya tatu katika uzalishaji wa gesi duniani. Je, tumejiandaa na hilo? *TPDC* tumeiandaa kwa hilo? Wizara imejianda kwa hilo? Serikali yenyewe imejiandaa kwa hilo? Au tutangoja wahisani ndiyo watufanyie?

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili vilevile nasema kwamba ni rahisi sana kuwavamia wanaojenga karibu na barabara na ni rahisi sana kuwavamia wachimbaji wadogowadogo lakini hawa wakubwa wanapovunja Sheria mbona kunakuwa na kigugumizi? Leo ukisikia mgodi umevamiwa Watanzania wako tayari kupigwa risasi haraka sana lakini wenye mgodi wanapotunyima *gold* zetu basi tunakuwa na kigugumizi, tunakwenda kwenye mazungumzo na usuluhisho. Wamevunja sheria za nchi, ni lini tutakuwa na *enforcement system* ya amri za Sheria zetu ambazo zinavunjwa kwa makusudi, toka 2004 mpaka 2009 watu wanavunja Sheria, niambie ni Mtanzania gani anayevamia mgodi akangojewa kiasi hiki hajapelekewa *FFU* akapigwa na risasi. Wanatuchezea hawa wawekezaji na kuna-*curtail* huko imekaa wanatuchezea kabisa wanavunja Sheria kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali na Wizara palipovunjwa Sheria hatua za kisheria zichukuliwe, hakuna *negotiation* katika kuvunja Sheria. Wabunge wako hapa, wakivunja Sheria wanaswagwa wala huambiwi wakati mwingine jamaa wanavunja Sheria, wanachukua mabilioni ya pesa halafu sisi bado tunakwenda kwenye *negotiation*, ni *negotiation* gani na wamevunja Sheria?

Tumewekeana mkataba na wamevunja mkataba tunachukua hatua za kisheria *immediately* hakuna *negotiation*, mna-*negotiate* mahali ambapo unahisi kwamba ama kiasi fulani unaweza ukapata au ukagawana lakini siyo mahali ambapo mtu amevunja Sheria. Sasa ukisoma mkataba wa *PSA* unakuta sehemu nyingi kampuni hizi zimevunja Sheria na bado tunabembelezana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzo kuna mapendekezo ya kuvunja mikataba lakini kwa bahati mbaya Serikali imeingia kwenye mikataba ambayo mingi ni mibovu sana, kwa hiyo ukienda Mahakamani tayari wewe uko katika eneo la kushindwa. Kwa hiyo, unachofanya ni kupoteza muda na gharama na kuongeza gharama za kesi, kuongeza gharama za kulipa. Tulikubaliana tu-*review these contracts*. Mimi naiomba sana Kamati ya Nishati na Madini kwa sababu tumekubaliana, mikataba ije Bungeni. Hebu tujifungieni katika Kamati ndogondogo ili tupitie hiii mikataba, Bunge hili lina *power* kubwa sana, Kamati zetu zinaweza kufanya kazi kubwa sana, kuisaidia Serikali, tusije tena humu ndani kulalamika bali tuje hapa tusema mkataba fulani tumegundua makosa kadhaa, tunataka kurekebisha, vinginevyo tutaendelea kwenye *Negotiation Team* na huko hakumaliziki kitu na taarifa haziji hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu kwa Kamati zetu zote madhari tumekubaliana mikataba tutaipata hapa kwa utaratibu, tuutazame ni mkataba gani unanyima haki za Watanzania, tuipitie mikabata hiyo, tuone upungufu wake na pale ambapo tunaona tunaweza kushtaka na pale ambapo tunaweza kupata haki yetu kwa kubadilisha mkataba basi Bunge hili ni kazi yake kutunga Sheria, tutunge Sheria na tuache kulalamika kwani *time* ya kulalamika imekwisha, Watanzania wataendelea kuwa maskini na sisi tutaendelea kulalamika humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru *spirit* ya Wizara, mimi Katibu Mkuu namfahamu, tulikuwa nae Hazina, ni mchapakazi mzuri, naomba sasa asimamie vizuri hii sekta na njia moja ya kusimamia ni kuzishirikisha Taasisi zetu hizi za elimu ya juu. Tunapenda sana sisi kutafuta wataalam wengi kutoka nje na kwa sababu tayari katika *shops* za *IMF* na *World Bank* zipo tayari, ma-*theory* yameshawekwa pale, watu tayari wanakwenda wana *cut and paste,* wanakuletea bila ya kuangalia maslahi ya Watanzania.

Nimemwuliza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Zabuni ni tafiti ngapi zilizofanywa na taasisi mbalimbali ambazo zimetumiwa angalau asilimia 40, hakuna. Angalia Kamati ya Bwana Bomani ni asilimia ngapi mapendekezo yake yamefanyiwa kazi leo. Hiyo ndiyo hali halisi, lakini fedha zinazotumika ni mamilioni ya dola, *value for money* haipatikani.

Naomba sasa kazi hii tuzikabidhi vyuo vyetu, vyuo vyetu vikuu vina uwezo kabisa, wana wataalam wamekaa pale wamefanya kazi mbalimbali tuwawezeshe kufanya kazi za kutuandikia mikataba, kazi ya kutufanyia utafiti na kadhalika badala ya kutegemea hawa watu wageni ambao kwa kweli kazi kubwa wanayoifanya asilimia 90 ya kazi ni *information* tunazotoa sisi wenyewe Watanzania, hakuna jipya wanalokuja nalo. Kwa mfano ukiangalia utengenezaji wa *ID* asilimia 80 ya taarifa ni jiografia ya Tanzania, asilimia kumi ilikuwa ni kazi waliyoangalia mashirika wanafanya nini na asilimia kumi ndio wameingiza huo utaalamu wao kidogo sana. Lakini wamechukua dola milioni kumi kwa kazi hiyo. Sasa nasema hizi kazi zinaweza kufanywa na Watanzania, hebu tuwawezesheni Watanzania kutumia rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa suala la matumizi ya gesi ninasikitika sana kama Serikali inatafuta dola milioni 50, hata *CRDB* wanazo hizo, *FMB* wanazo, *PTA Bank* wanazo, tuchangamkie hili jambo haraka sana. Misitu inapotea, wananchi wanagharimika sana kwa kutumia mkaa, gharama zinaongezeka na bado bei ya mkaa inapanda kila siku, lakini gesi haipatikani. Usambazi wa gesi hauonekani hebu tuwe na *programme of action* sasa tuwaambie katika mwaka mmoja au miwili inayokuja sasa Watanzania hata angalau wa Dar es Salaam kwa kuanzia asilimia ngapi wataweza kutumia gesi asilia ya Tanzania, tuondokane na huu utaratibu wa kutumia kuni. Hadithi zimekuwa nyingi, maneno yamekuwa mengi, hakuna shida ya Serikali kupata dola milioni 50 hata kidogo, tumezitumia nyingi tu kwenye sherehe zetu za Uhuru, kwa nini tukose kwenye gesi, kwa nini tusiweze kutumia kwa Tanzania? Tunahitaji kujielekeza kwenye *priority* ambazo ni muhimu kwa kuwapunguzia maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa tunataka tuone gesi hii inapunguza ukali wa maisha. Hatupunguzi ukali wa maisha bado tunazalisha vitu vyetu Tanzania, lakini bado gharama zake ni kubwa nalo linahitaji kuangaliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hujasema shilingi ngapi zinatumia kwenye maharusi, basi tena. Mheshimiwa Kirigini sasa ni msemaji wetu wa mwisho wengine watanisamehe muda umekwisha.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuchangia hoja hii muhimu iliyoko mbele yetu na kama walivyofanya wenzangu wote wenye nia njema naomba nichukue fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kabisa kuipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya kwa maazimio muhimu sana ambayo wamekuja nayo na kuyawasilisha katika Bunge letu Tukufu, nina imani wanayo nia njema ya kutaka kuisaidia sekta hii na hasa Wizara hii ya Nishati na Madini katika kurekebisha mambo ambayo yameonekana hapa na pale hayaendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba maazimio haya ambayo yametolewa na Kamati hii ya Nishati na Madini yanahitaji utekelezaji mgumu na niiombe tu Serikali iweze kuwa na moyo mgumu katika kuyatekeleza haya kwani naona kama utekelezaji wake kwa kweli unahitaji nguvu za ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo niipongeze sana Serikali, nimepitia jedwali lao la utekelezaji wa maazimio hayo na kwa kweli napenda kusema kwamba nawapongeza sana kwa namna moja wamekubali. Karibu kila azimio wamekubali kwa maana kwamba wamekubali *idea* ya Kamati na wameeleza kwamba wako tayari kabisa kushughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo nimeliona katika jedwali lile kwa upande wa Serikali hakukuwa na *time frame*, tumepewa tu maelezo kwamba tunakubali, tunapokea ushauri wa Kamati, tutayashughulikia, tupo mbioni na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningependa kuwe na *time frame*. Ni lazima tukubali kwamba sekta ya nishati ya gesi asilia ulimwenguni kote ni nishati ambayo inakuwa na sisi kama nchi na dunia kwa ujumla ni lazima tukubali kabisa kukabiliana na changamoto zote ambazo zinaweza kutupata kama nchi.

Niseme tu kwamba suala ambapo naliona hapa ni suala zima la utawala bora, hakuna kabisa *accountability* na *transparency* kwa maana ya kwamba Wabunge wengi hapa tunasema, tumesema tunahitaji mikataba yote ya nishati na madini iweze kuletwa ndani ya Bunge na ipitiwe upya kwa maana ya kwamba Wabunge kama Wabunge tunakuja kugundua kwamba mikataba hii ina matatizo kama ambavyo Kamati imeainisha, matatizo ni mengi sana lakini tunakuta kwamba *it is too late* na fedha nyingi za Serikali zimepotea.

Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali na Bunge lako Tukufu, Wabunge wote tukubali mikataba yote inayohusiana na madini na nishati na hasa nishati hii ya gesi kwa sasa yote iletwe Bungeni ili sisi Wabunge tuweze kuipitia na kuweza kuona namna gani tunaweza kuokoa fedha za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia maazimio kama yalivyotolewa Serikali inasema kwamba itaunda *negotiation team* ni sawa, lakini kuna maazimio ambayo maoni ya Kamati yako *direct.* Suala kama Azimio namba 2, 4 na 19 yanahusiana na wizi wa fedha, kukosa uaminifu kwa mwekezaji na uzembe wa mwekezaji uliopelekea visima kuharibika. Sasa najiuliza swali kama hili hivi Wizara inahitaji *negotiation team* ya kazi gani, huu ni uhaini. *(Makofi)*

Mimi napenda kuishauri Wizara ipeleke suala hili moja kwa moja kwa *DCI* aweze kushughulika na hawa watu haraka iwezekanavyo na ikiwezekana tunaomba maazimio haya yasiwe kama maazimio yaliyopita. Kwenye Bunge lijalo la mwezi Aprili tunaomba tupate majibu kutoka kwa *DCI* namna ambavyo mwekezaji huyu amechukuliwa hatua kwani ni fedha nyingi sana za nchi zimepotea kutokana na ukiukwaji wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kununukuu Azimio Namba 18 kwa ruhusa yako ukurasa 25 linasema; "Katika hali ya kusikitisha, kuvunja moyo Kamati imejiridhisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa haitoi ushirikiano wa kutosha kwa *TPDC* na *EWURA* hasa katika kusimamia masuala ya sekta ya gesi. Vitendo vya ukiukwaji wa taratibu, udanganyifu na uhalifu vinafanywa na *SONGAS* na *PAT* kwa lengo la kuibia nchi na vitendo hivi vinafanywa pia kwa kushirikiana na Wizara."

Mheshimiwa Spika, sasa suala hili pia linahitaji *negotiation team.* Mimi nadhani ni wakati umefika sasa kwa Waziri husika kufanya maamuzi magumu. Kamati kusema kweli naipongeza sana imekuwa

imeweka wazi/bayana kabisa yaani ni kiasi cha Waziri sasa ku-*act.* Kuna watu pale Wizarani wanafanya vitendo hivi kama Azimio hili Namba 18 lilivyosema na ningemwomba Waziri husika achukue hatua. Lakini kuna suala la upotevu wa fedha, tunamjua *CAG* wetu alivyo hodari, mimi najiuliza hivi hata fedha hizi kweli hakuziona? Kwa hiyo, niombe hatuhitaji hapa *negotiation,* huu ni wizi na tunaomba tupate taarifa kwenye Bunge linalokuja namna gani taarifa ya fedha hizi *USD* milioni 36 za nchi yetu tunahitaji kupata taarifa kutoka kwa *CAG* na iletwe hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tumekuwa tukihangaika sana na *TRA* kutafuta kupanua wigo wa mapato. *TRA* kama *TRA* ina walipa kodi wachache sana. Kamati imeainisha kuna upungufu mkubwa sana wa mapato kwenye eneo lile la gesi. Sasa niwaombe *TRA* kupitia Bunge lako Tukufu waweze kabisa kuangalia kwa mapana na kina eneo hili la gesi na kuhakikisha kodi yote inayotakiwa kukusanywa kwenye eneo hili liweze kukusanywa na nchi yetu iweze kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena naipongeza sana Kamati, mmekuwa mfano mzuri na kwa kweli Kamati nyingine inabidi tuige mfano, mmejitoa kweli kweli katika kushughulikia sekta hii ya nishati na madini. Niseme tu Waziri wala usijisikie vibaya, huu ni wakati wako sasa wa ku-*act.* Umeambiwa ukandamize, kandamiza wala usione haya, huu sio wakati wa kuoneana haya, utakapoona haya ndipo mapato ya nchi yanavyozidi kupotea. Kwa hiyo, tunakutegemea sana, una Katibu Mkuu mahiri, kaka yangu Maswi nina imani kama timu mna timu nzuri sana pale Wizarani, tuna imani nishati hii ndogo ya gesi mtaisimamia ipasavyo na mapato mengi zaidi yataweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mchangiaji wa mwisho sipendi kupoteza muda ninaomba kuunga mkono Maazimio yote na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kusema machache ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusiana na Maazimio haya ambayo Bunge lako Tukufu lilileta kwa ajili ya kuboresha sekta nzima ya gesi na mwelekeo wake wa jumla wa namna tunavyokwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa William Ngeleja, Katibu Mkuu Bwana Eliakim Maswi na watendaji wote wa Wizara yetu na Taasisi zake na hasa *TPDC* kwa kazi kubwa iliyofanywa ya kufanyia kazi Maazimo haya lakini pia naomba kwa namna ya kipekee niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wakiongozwa na Mheshimiwa January Makamba na Makamu wake Mheshimiwa Diana Chilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliongoza ujumbe wa Wizara kwenye kikao cha mwisho cha kupitia ripoti hii Jumamosi kwa sababu Waziri alikuwa amehitajika mkoani kule kwa shughuli za chama na naomba nikiri kwamba pamoja na kazi kubwa ambayo sisi tulikuwa tumeamini kwamba tumeifanya ndani ya Wizara kujibu zile hoja, lakini bado palijitokeza maeneo mengi ya ushauri mzuri tu ambayo Kamati ilikuja nayo kwa siku ile ya Jumamosi na kwa kipindi chote ambacho tulikuwa tukilifanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

Mimi kwa upande wangu pamoja na kwamba nimelifanyia kazi jambo hili kwa muda mrefu, lakini nilifarijika sana na kiwango cha kazi kilichofanywa na Kamati kwenye masuala *very specific,* kwa mfano suala la *human resource capacity building* na umuhimu wake na suala la kuboresha watendaji mle ndani ambalo limekuwa tunalifanyia kazi, lakini kwa sasa kwa kuwa limepata msukumo wa Kamati naamini litapata utekelezaji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni hili la *financial management* na masuala yote yanayohusiana na mapato na matumizi ya gesi. Lazima niseme naamini kwamba tumeyafanyia kazi kwa kina sana na baada ya hapa tulipofikia huko mbele tunakokwenda hakuna sababu ya kurejea nyuma na kulalamika kusema kweli tumeshajiwekea misingi mizuri sana ya kufanyia kazi jambo hili na kuweza kupata utekelezaji mzuri zaidi. Niseme tu juzi kulikuwa na mkutano baina ya watendaji wakuu wa Benki ya Dunia na wale watendaji wakuu wa *EITI* na nchi mbalimbali za Kiafrika, Afrika ya Kusini mimi niliwakilisha ujumbe wa Tanzania na katika hayo sisi ni miongoni mwa nchi ambazo tuko kwenye mpango unaitwa *Gas for Development (G for D)* ambao ni mpango mpya ambao umeletwa na Benki ya Dunia kujaribu kuangalia namna ambavyo gesi inaweza kupata matumizi zaidi katika maendeleo ya nchi zinazoendelea, lakini hata kwa nchi ambazo zinazalisha gesi na kiini chake ni kwamba imeonekana hata zile nchi ambazo zinazalisha sana mafuta, gesi walikuwa wanaichoma tu moto. Sasa ikiangaliwa kama *resource,* gesi ni *more cost*

*effective* lakini ni *more friendly to the environment*. Kwa hiyo, hata hizo nchi nyingi ambazo zina mafuta ya kutupa kwa sasa hivi zinaangalia namna ya kuelekea kwenye gesi na sisi kama *a future country of a future export of our gas* tumeshakaa vizuri na tunaamini kwamba kuna *forum* kama *Gas Exporters Country Forum* ambazo tumeshapata mwaliko wa kuwa *observe country,* naamini kwamba ushiriki wetu katika maeneo kama haya yanatupa uwezo wa kufahamu mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nilitaka nizungumzie tu hili suala ambalo Mheshimiwa Festus Limbu na Mheshimiwa Mariam Kisanji wamezungumzia suala la matumizi ya gesi majumbani. Ni kweli ni suluhisho kubwa sana hasa kama mkakati huu ambao upo unalenga miji mikubwa kwa Tanzania itakuwa ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza ambayo *generally speaking* katika miji hii tu watu ambao wanatumia mkaa kila siku hawapungui watu milioni 15 *between* Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na kadhalika. Sasa ukipata *strategy* ya kuwa na mitungi ambayo kwanza utaanza na Dar es Salaam na ni *culture*/ni kitu ambacho lazima iwe ni tamaduni ambayo tunaifanyia kazi.

Mimi nadhani ushauri wa Kamati ni mzuri na kwa kuwa limeshazungumzwa sana humu Bungeni nadhani tunaelekea kwenye kulipatia ufumbuzi wa utekelezaji na nimefarijika sana hili la Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed aliyezungumza suala la *domestic mobilisation and financing.* Lazima tufike hatua ambayo tuache utegemezi wa bajeti za Serikali, lakini kama jambo lina misingi ya kibiashara na lina *generate income* na *commercial viability* halina sababu kwa nini saa zote tulielekeze kwenye bajeti za Serikali. Kwa hiyo, hilo naomba niseme kwamba na sisi tumekuwa tunaliangalia, tumekuwa tunalizungumza miongoni mwetu nataraji kwamba tutalifanyia kazi kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kupeleka gesi Kenya, Mombasa ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Festus Limbu, naomba nilisemee, hili pia limejadiliwa kwenye *East African Community Sectoral Council.* Wakenya walikuwa wameomba kwamba bomba liende mpaka Mombasa *which is fine* na hapo walipoomba Wakenya na Waziri wa Rwanda akasimama akasema na sisi tunataka gesi na Mganda akasema na sisi tunataka gesi. Kama ambavyo na sisi tutakavyosema wakati Uganda wanaanza kuzalisha mafuta na sisi tutawaambia na sisi tunataka mafuta yenu kwa *concession* tutakapofika kwenye *Community*. Lakini tulisema wazi na hili naomba niliseme kwa sababu naona linasemwa hata kwenye magazeti linapotoshwa. Hatujasema kwamba tutaanza kupeleka gesi Mombasa na wapi kabla sisi wenyewe hatutajitosheleza na sisi wenyewe *we have our own priorities* na la kwanza kabisa ni umeme, la pili ni mbolea, la tatu ni *LPG* kwa maana ya kupata *compress natural gas* ya kutosha na kupeleka majumbani. Sasa tukifika hatua ambayo tume-*address* maeneo ambayo ya kwetu wenyewe yanatutosheleza *then* tuna *excess,* hatuna sababu ya tusizungumzie masuala ya kuwa *gas exporter*. Lakini kwanza tukifanikiwa kuweka gesi kwenye hayo maeneo matatu niliyoyasema umeme, mbolea na hili la matumizi ya gesi majumbani hata gharama za maisha ya watu itapungua kwa kiasi kikubwa sana na hilo lazima tuliseme ndio lengo ambalo tunataka tulipeleke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nimeona pia nilisemee pamoja na lile la *royalty* za gesi na haki za wananchi wa Kilwa ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Hili mwaka jana tulipokuwa Kilwa na mwaka juzi pia tulipokwenda Kilwa, limesemwa na wananchi wa Kilwa na wanalizungumzia lina mkakati kidogo wa kisheria ili liweze kufanyiwa kazi. Lakini mimi naomba niseme tu nalo limekuwa linafanyiwa kazi na naamini kwamba limefika wakati ambao sasa lipatiwe ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilisemee hili la makampuni haya makubwa ya duniani ya gesi ya Kitaifa ambayo yametajwa *Petro gas, Petro Brass* na kuna Kampuni hasa hii ya *Trinidad and Tobago* ambayo nadhani kwetu sisi zaidi ndio Kampuni ya mfano. Kwa sababu *Trinidad and Tobago* wameanza muda mrefu wanavuna gesi kama miaka 70 na hawakuwa na teknolojia ya kuvuna gesi kama ambavyo sisi tulianza. Sisi tulikuwa hatuna hiyo taaluma, lakini wameleta uwekezaji kutoka nje, sasa wamekwenda, wame-*review* hili jambo na kwa bahati nzuri Mwanasheria wao Mkuu anasema ni jambo ambalo tumekaa tumezungumza nae anasema ni jambo ambalo linataka maamuzi ya msingi na tulifika hatua ya kusema labda tungekaa nao wenzetu hawa ambao sio tu kwamba wana *resource* za gesi lakini wamepitia *process* ile ya kufanya mabadiliko ya mikataba na ya kisheria na kadhalika ili kwenda na wakati na mahitaji ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nimeshukuru kwamba hili limesemwa, kwanza ndani ya Kamati limesemwa sana na hapa Bungeni leo limesemwa na naomba niseme tu kwamba ni jambo ambalo tumelipokea na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la *structural adjustment* ambalo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amelisema lakini hata kwenye Kamati limezungumzwa sana. Suala la taaluma kuwa na mfumo wa *specialized capacity building.* Hili sisi tuna tatizo moja na ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na lazima lifanyiwe kazi kwa haraka. Huwezi ukamchukua Mwanasheria au Mhasibu ametoka Chuo Kikuu uende ukampambanishe kwenye masuala ya nishati na gesi. Kwenye ma-*contractual*, *accounting and auditing,* wenzetu hawa *have specialized accountants* na *auditors* wa masuala ya gesi na nini na nini. Sasa hili ambalo limezungumzwa hapa ni *so relevant,* ni jambo muhimu sana. Kwa maana hiyo hata *CAG* mwenyewe tukimwambia twende ukaangalie masuala ya *TPDC* lazima mwisho wa siku aende akawaone wataalam wenyewe wa *TPDC* ndiyo wamsaidie kwa kiwango hicho kidogo walichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani hili ambalo Bunge lako Tukufu limelisemea leo la kwamba ni lazima tuwe na *specialized accounting, auditing* na *legal framework, specialized to the field of gas* ambalo hata watu wa *extractive industry EATI* wameji-*commit* pamoja na Benki ya Dunia kutusaidia naamini kwamba kuanzia wiki ijayo hili jambo litaanza kupata ufumbuzi na ikifika mwezi wa nne tutakuwa na nafasi zaidi ya kusema tutafika nalo wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la *contractual review* na masuala ya kuvunja Mikataba, mimi nilikuwa nashauriana na Waziri hata pale anasema ni jambo zuri kwa sababu kwanza sisi sio wa kwanza ambao tutalifanya. Kwa bahati mbaya huwa tunapokaa na wawekezaji au nini huwa inatoka *impression* kwamba sisi Watanzania tunataka kulifanya kwa mara ya kwanza, si kweli. Wenzetu wengi wamelifanya; lakini nao litataka kuangalia *legal precedents* na mimi sio Mwanasheria lakini naamini kwamba Wanasheria wakilikalia chini hili jambo tunaweza kulifanya na likawa na manufaa kwa Taifa letu, si kuvunja mikataba lakini *even to review the contractual obligations* za nchi katika misingi hii na naishukuru sana Kamati kwa sababu kwenye taarifa yao na kwenye mjadala wa *face to face* hili jambo limesemwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza kuhusu utaratibu wa kisheria wa humu ndani Bungeni wa kuchukua hatua kali za kisheria pale ambapo pana upotoshaji wa makusudi, *false declaration* ya *revenue* na *expenditure*. Hili linatokana na masuala ya udhaifu kwenye *reconciliation* ambalo tumeanza kulisemea na tumegundua kwamba nchi nyingi ambazo hawa mabwana wakifika sehemu ambayo na ninyi wenyewe mnakiza kidogo na wao wanaendelea. Lakini sasa hivi kuna *a deliberate process* kwenye nchi nyingi duniani kama sisi ambao tunaangalia mikakati ya kuboresha taaluma ya *reconciliation* ili usifike hatua mtu anakwambia "ahha!! risiti zangu za miaka saba iliyopita sizioni." *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba niseme hili limezungumzwa kwenye Kamati Jumamosi na tumeafikiana na tumekubaliana nao kwamba hivi tunavyokwenda kwenye Mabunge yanayofuata tulete taarifa kwenye Bunge lako kwamba tumefikia hatua gani za kuboresha *capacity building* hasa kwenye masuala haya ya kuwawezesha watu wetu kuwa makini zaidi kwenye *monitoring of income and expenditure* za makampuni haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kasi ya utendaji kazi kwenye Sheria, kwenye miongozo na kwenye utendaji wa *GNT* na ni kweli kwamba tukikaa tunasema labda *GNT* itafanya kazi lakini kwenye masuala ya *time frame* nadhani pia Mheshimiwa Waziri atalisemea tumeridhia kwamba ni vyema tukajiwekea *time frame*. Haya mambo yanapokwend *endlessly* hayatusaidii wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Tanzania ina *estimated reserves* za *10 TCF trillion cubic feet* za mafuta ndiyo tunazotaraji kuwa nazo huko mbele. Tunaweza tukazipata zingine ziko *offshore*, nyingi ziko baharini lakini zinataka uwekezaji mkubwa sana ili mwaka 2018 tuwe nchi ambayo ni *gas exporter* mkubwa dunia nzima, tutashindana huko na kina Qatar na nani. Lakini lazima tukubaliane kwamba pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu ametupa hizi *resources,* ni lazima tuingie kwenye *deliberately expenditure and some of it* lazima iwe *domestically mobilized* lazima itokane na sisi wenyewe humu humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kuweza kufikia huu uzalishaji wa gasi mkubwa wa gesi namna hii ni lazima tutaingia humu Bungeni na tujue kwamba itabidi tujifunge kwenye kuacha mengine ili tufanye

mengine kwa maana ya kwamba kama wanavyosema wataalam wa *choice theory* tunachukua hili ili baadae tuweze kuingia kwenye nini. Hili jambo ni muhimu sana kwa sababu tutakapokuja Bungeni na masuala ya kuongeza uwezeshaji kwa ajili ya sekta ya gesi sio haya tu, ya *TPDC* yenyewe iwe na *participation* kwenye uchimbaji huo. Sasa mtu anapokuja pale kuna *risk element* na wewe unataka uweke pesa yako ili tutakapofika sehemu na sisi tunasema tuna asilimia 40 ya mapato yote yanayotokana humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapofika hapo ni lazima tukubaliane kwamba tutakuja Bungeni na mapendekezo ambayo yatakuwa yamefanyiwa kazi na tutawaomba Wabunge wenzetu waturidhie. Hili tutabana matumizi fulani ili ndani ya miaka minne, mitano Tanzania iweze kufikia kwenye uzalishaji wa *10 TCF*.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naomba nilishukuru Bunge lako Tukufu na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kwa mara nyingine tena kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini kuwashukuru sana wote waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kusema au kwa kupitia maandishi. *(Makofi)*

Lakini kikubwa tunaishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini kwa jinsi ambavyo imeshirikiana na Serikali katika kujadili Maazimio haya ambayo kimsingi yalitokana na ile Kamati ndogo iliyoundwa ndani ya Kamati ya Nishati na Madini. Tunajivunia kuwa na wataalam ndani ya Kamati hii, lakini pia tunajivunua kuwa na Kamati ambayo imesheheni uelewa katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ilivyo ada nipende kutumia nafasi hii kwa kuanza kuwatambua wale ambao wamepata nafasi ya kuchangia. Wa kwanza kabisa aliyechangia baada ya sisi kuwasilisha taarifa yetu alikuwa ni Mheshimiwa Charles Mwijage, ambaye aliwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na kwa hili tunamshukuru sana kwa uwasilishaji wake mahiri na jinsi ambavyo alikuwa anavutia. *(Makofi)*

Lakini wa pili baada ya hapo alifuatiwa na Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati lakini katika nafasi hii alichangia hoja. Wengine walikuwa ni Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa  Dokta Festus Limbu, Mheshimiwa Diana Chilolo huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Rosemary Karigini. Mwisho lakini si kwa umuhimu waliopata nafasi ya kusema alikuwa ni Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini na kwa hili nampongeza sana pamoja na kwamba amefika dakika za majeruhi lakini ameweza ku-*follow* kwa sababu mambo haya amekuwa akiyashughulikia siku hadi siku. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri karibu sana, pole na safari lakini tunakushukuru sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dokta Festus Limbu, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa  Abdul Mteketa, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis na  Mheshimiwa Moza Abedi Saidy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama itatokea kwamba wapo baadhi ambao nimewasahau kwa bahati mbaya basi naomba nirekebishe na taarifa inifikie ili tuweze kuwatambua na *Hansard* ichukue kumbukumbu sahihi. *(Makofi)*

Baada ya ya kusema haya napenda kusema kwa dhati kwamba sisi kama Serikali tunaendelea kunufaika sana na michango ya Bunge lako Tukufu na hasa uchambuzi ambao umekuwa ukifanywa kupitia Kamati zetu. Kama nilivyosema sisi tunajivunia sana mawazo na michango mahiri ambayo imetolewa na Kamati yetu ya Nishati na Madini.

Katika michango ambayo imewasilishwa leo kwanza tunapokea ushauri, maoni na hata ule msisitizo wa mambo mbalimbali ambayo yamejitokeza kwenye taarifa katika maazimio haya 26. Niseme tu kwa ufupi kwamba pamoja na kwamba Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mengi kwa nyakati tofauti lakini yapo masuala ambayo yamejitokeza ambayo kwa mtazamo wa jumla tunaona kwamba haya ndiyo yalichukua nafasi kubwa katika kujadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya mambo ambayo tumeyabaini ambayo yamejitokeza katika mjadala ama kwa kusema lakini pia kwa maandishi ni pamoja na masuala yafuatayo:-

La kwanza ni kuhusu Muswada wa Sheria ya Gesi uharakishwe. Hili tumelipokea na kama tulivyosema tunakusudia katika Mkutano ujao wa Saba, Muswada ule utakuwa tayari kuwasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa. Lakini pia kuhusu Muswada wa Kusimamia Mapato yatokanayo na Gesi *(Gas Revenue Management)* uandaliwe limejitokeza hapa na Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza na sisi tumeanza kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udanganyifu wa *Pan-African Energy,* hatua za kisheria zichukuliwe. Tumesema na nataka niseme kwa mara nyingine tena Serikali imedhamiria, hatuna sababu yoyote ya kumhofia mwekezaji yoyote katika nchi yetu hii. Tunafahamu zipo changamoto za utaratibu ndiyo maana tukasema hata katika taarifa yetu wakati wowote Serikali hutumia vyombo vyake vyote vinavyohusika chini ya usimamizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutajitahidi kuhakikisha kwamba maslahi ya Watanzania yanazingatiwa. Lakini yanazingatiwa katika utaratibu ambao hautufikishi mahala ambapo athari zinaweza kuwa kubwa kuliko tulivyokusudia. Ndiyo maana tunasema pamoja na kwamba mikataba tuliyonayo inatoa utaratibu, Serikali itajitahidi kwa kadri inavyoweza kuhakikisha kwamba utaratibu huo hauwi tena kikwazo kulinda maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa uchungu sana haya mapunjo ambayo hatimaye yanaonekana kama kwa mfano ingekuwa tumesharudishiwa dola milioni 20.1 Waheshimiwa Wabunge wanasisitiza na sisi tunaelewa uchungu walionao kama ambavyo Serikali inao; kwa nini fedha hizi zisilipwe mara moja?

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla nataka nikumbushe jambo moja kwamba mahusiano yetu na hawa wawekezaji; leo tunamjadili *Pan African Energy Tanzania* yanatokana na Sheria zetu lakini pia inatokana na mikataba ambayo tumefunga nao, hatuna mahusiano nao yoyote zaidi ya hayo maeneo. Hatuna nasaba nao na kwa sababu mahusiano hayo yamefungwa kimikataba, ni jambo la kawaida tu kwamba lazima tuzingatie huo utaratibu wa kisheria. Lakini kama ninavyosema Serikali itakuwa makini, ipo makini kuhakikisha kwamba tunafikia hatua ya kulinda maslahi yetu bila kuathiriwa na utaratibu. Ndiyo maana tunasema mikataba hii tunaipitia upya tena ili kubaini mahali ambapo hata kama tumefungwa kimikataba basi kama kuna eneo ambalo tunahisi kwamba linatukwanza lirekebishwe na kwa wale watakaopinga mapitio mapya ya mikataba hii hatuhitaji kuwa nao kwa sababu sisi bado tunaamini sio mwekezaji mmoja au wawili ambao wanaweza kuiyumbisha nchi kwa sababu ya maslahi yao wenyewe binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado tunaamini kwamba Tanzania ni sehemu mwafaka, nzuri na inavutia kwa uwekezaji kwa sababu ya rasilimali tulizojaliwa kuwa nazo. Kwa hiyo, hatuna shaka na hilo, hatuna hofu na kwa kufuata utaratibu huu hatumaanishi kwamba tunapata kigugumizi wala tunawahofu wawekezaji. Hakuna mwekezaji anayeweza kuitisha Serikali yotote na Tanzania ikiwemo. Kwa hiyo, tupo makini katika hili naomba Watanzania kwa ujumla waamini Serikali itaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa mujibu wa mikataba iliyopo ambayo ndiyo inatupa mahusiano na wao na Sheria za nchi zilizopo, kwa sababu mikataba mingine hii pia inahusu hata kutambua mambo ambayo Mataifa kwa ujumla yamekubaliana kuzingatia. Kwa hiyo, tutazingatia kwa yote lakini mwisho wa yote lazima haki itendeke na maslahi ya Tanzania yata-*prevail* wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limejitokeza suala ambalo limejadiliwa pia kwa uchungu sana kuhusu ukarabati wa visima vyenye kutu. Tumeitolea ufafanuzi na tumesema ni kwa nini tumewaruhusu *Pan-African Energy* baada ya kuzingatia yote kwamba waendelee kuchoronga ili gesi iwepo ya kutosha wakati utaratibu huu au maandalizi ya kurekebisha visima ambavyo vinahitilafu vinafanyiwa kazi. Tumefanya kwa kuzingatia jambo moja tu. Katika mazingira tuliyonayo leo ni lazima tuwe na gesi ya kutosha ili tupate umeme lakini pia kwa matumizi ya viwandani. Hatuna mbadala ya kutokuwa na gesi leo kwa sababu kutokuwa na umeme katika mazingira yoyote yale madhara yake ni makubwa sana kuliko pengine kuvumilia hili kwa utaratibu ambao tunaamini kwamba haututii hasara tena mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hili nalo tumekuwa makini tumelinganisha athari na madhara yake lakini tumesema hawa hawana pa kukimbilia kwa sababu hatimaye urekebishwaji wa visima hivi upo pale pale na sasa mpango huo wa kurekebisha tunao na wameshawasilisha kupitia *TPDC* na sisi Serikali kama wasimamizi tumeridhika kwamba mipango ambayo imetekelezeka na hakuna namna ambayo watakwepa kurekebisha hivi visima.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limejitokeza hapa ni uimarishwaji wa *TPDC*. Waheshimiwa Wabunge wamechangia sana na nashukuru kwamba leo tunakubaliana kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kuna umuhimu pamoja na mambo mengine, *TPDC* iachwe ijiendeshe yenyewe. Huo ni mkono wa Serikali na ndiyo tunachokitaka. Jambo hili tumelifanyia kazi kwa miaka kadhaa iliyopita na kuna wakati kabisa *TPDC* hawakuwa na chochote tukasema *retention* ikaanza, tukaanza na asilimia 25, imefikia asilimia 50, tunafarijika sana kusikia habari hii kwa sababu hili jambo halihitaji kulisema kwa nguvu nyingi sana. Kuna taasisi za Kiserikali ambazo *ownership* yake ni ya Serikali kwa asilimia 100 zinajiendesha na zina *retain* asilimia 100. Kwa nini *TPDC* ambayo ni *agency* ya Serikali leo iendelee kukusanya fedha inazipeleka Hazina halafu zikarudi wakati tunafahamu zipo taasisi nyingi zinafanya vizuri na zinajiendesha kwa kuwa na *retention* ya asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalishukuru sana Bunge lako Tukufu na tunaamini kwamba kwa jambo hili tutaimba wimbo mmoja, tupo kwenye ukurasa mmoja, tulisimamie kwa pamoja na sisi tupo tayari kulitekeleza hili jambo kwa sababu *TPDC;* leo unaona nchi nyingine za Afrika Mashariki zinasema zinatafuta gesi, zinagundua nini walimu wao ni *TPDC,* kwa nini tuendelee kuwanyanyapaa na kuwanyanyasa *TPDC?*

Mheshimiwa Spika, siamini kama tunanyanyasa na sitaki kutumia neno la kuudhi lakini nasema nadhani katika mazingira tuliyonayo ni vyema *TPDC* iachwe ijiendeshe, tuisimamie vizuri kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumesisitizwa sana suala la Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Mahesabu ya Serikali *(CAG)* akamilishe uhakiki haraka. Tumeweka ratiba, katika hili Serikali yote kwa ujumla inalitizama kwa mtazamo mmoja tu. Jambo likamilike, hatima ijulikane na maamuzi yachukuliwe. Kwa hiyo, katika hili hatuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa usambazaji wa gesi asili usihusishe *PSA*. Tumetolea ufafanuzi, ugatuaji *(unbundling)* inaendelea na utaratibu kwa kweli katika hili hatuna mashaka nalo. Serikali ijenge uwezo wa ndani katika nyanja za mikataba, majadiliano, ukaguzi wa mahesabu pamoja na kasi ya matumizi ya gesi asili kwenye viwanda, magari na majumbani uharakishwe. Tumesema, kwanza katika hili la mafunzo na kujenga uwezo niseme tu kwamba zipo hatua kadhaa tumechukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi, Mheshimiwa Naibu Waziri na wengine pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili wanafahamu, wameshafika katika nchi mbalimbali. Lakini mojawapo ya nchi ambazo zimefanikiwa sana katika usimamizi wa eneo hili ni *Trinidad and Tobago*. Tumefanya mawasiliano rasmi katika eneo hili, tunaendelea kufaidi mahusiano yetu haya na wao kwa kutujengea uwezo. Kwa hiyo, hili ni namna moja ambavyo tunajijengea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini michango ya Waheshimiwa Wabunge mliyoitoa hapa, tutumie *top brain* ambazo tunazo katika vyuo vyetu, hilo zoezi limeshaanza Chuo Kikuu cha Dar es salaam na *UDOM* tumewaelekeza waanzishe mitaala sasa ambayo itafanya *orientation* na ita-*concentrate* katika maeneo haya, kuwe na *focus* katika sekta ndogo ya gesi ambayo siyo jambo ambalo kila msomi anaweza kulifanyia kazi. Kwa hiyo, tumeshaanza kuwasiliana nao, tunashirikiana nao na tunaamini kwamba kwa

kadri muda unavyokwenda na sisi uwezo wetu utakuwa unaimarika. Lakini hatuishii hapo tu, wadau hao wanakuja kufanya kazi na sisi kama Taifa kwa maana ya uwekezaji wa hayo makampuni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tunashukuru, leo ukiongelea makampuni makubwa matano yanayofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi duniani, mengi ya hayo yapo hapa Tanzania, ama wamenunua hisa ama wameingia mikataba ya kushirikiana na makampuni ambayo yameingia mikataba na *TPDC* ama wao wenyewe wamepata vitalu.

Sasa tunawaambia, mojawapo ya namna ambayo wao wanaweza kusaidiana na sisi tukanufaika katika kile ambacho tumekuwa tukisema uwiano sawa wa manufaa katika sekta hii ni pamoja na kutusaidia kujenga uwezo wa Watanzania. Makampuni haya tumekuwa tukishirikiana nayo na nipende kushukuru kampuni ya *Petrobras* ambayo tayari imeshaanza kwa kushirikiana na taasisi zetu kama *VETA* na wengine kuanza kutujengea uwezo. Zoezi hilo tunalifanya liwe ni *cross cutting* kwa makampuni yote kuhakikisha kwamba jambo hilo linafanyika kusaidiana, ku-*complement* juhudi za Serikali ambazo zimekuwa zikifanywa katika eneo hili kwa ajili ya kujenga uwezo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna vyuo vyetu wenyewe, kwa mfano, *DIT*, Arusha, Mbeya na hata hivyo vyuo vya *VETA*. Tunaamini kwamba tukishirikiana navyo katika kozi mbalimbali, kwa sababu katika shughuli hii ya uchimbaji na utafuaji wa mafuta ama uchimbaji wa gesi si kwamba kinachohitajika ni elimu ya kuwa mpaka na *Degree* ama *Ph.D*, hapana, ni maarifa ambayo yanapatikana katika kiwango mbalimbali cha elimu.

Kwa hiyo, ndiyo maana tunatumia vyuo vyetu hivi vya *DIT*, Arusha, Mbeya na *VETA* ili kuona namna ambavyo wao wenyewe wanaweza kutusaidia kujenga uwezo na hatimaye tupate nguvu kazi ambayo itashiriki katika shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea sana ni hili la kuimarisha usimamizi kwa ujumla na usimamizi huu nasema ni pamoja na kuona namna gani *TPDC* inasimama. Jambo moja ambalo tumelifanya sisi ni kuanzisha kampuni ya usambazaji gesi. Kampuni hii, ukisoma taarifa yetu, tumeitolea maelezo. Lakini kuanza kazi kwake, itakuwa kwenye mwaka ujao wa fedha, katika bajeti itakayokuja ya mwezi Juni, kati ya maeneo ambayo mtaona tukiyaombea fedha kwa ajili ya kuanza hii shughuli ni kampuni hii ya usambazaji gesi. Tunaamini kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunazidi kudhibiti vizuri, kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa eneo hili la gesi asili nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo limejitokeza hapa ni kuwa na mamlaka ya udhibiti katika eneo hili. Nitaje Waheshimiwa Wabunge wachache ambao wamelisema hili ni Mheshimiwa Gosbert Blandes amelisemea sana, Mheshimiwa Nimrod Mkono ametoa mchango wake, lakini pia Mheshimiwa Richard Ndassa amelisema, Mheshimiwa Dokta Festus Limbu kwenye mchango wake wa maandishi amesema na Mheshimiwa Kabwe Zitto amelisisitiza sana. Tunakubali ni wazo zuri, tunayo mamlaka ambayo sisi kwa maana ya *input* za kuanzia, tunayo *TPDC* watatushauri, tutashirikiana na watalaam wengine, tutajifunza uzoefu wa watu wengine ambao wamefanikiwa katika maeneo haya ili hatimaye tuhakikishe kwamba sisi katika eneo hili, tunafanya kwa ubora na ufanisi kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba kwa leo tunavyoongea, sisi Tanzania bado ni wachanga katika eneo hili, kwa hiyo, yapo mambo ya kujifunza kwa wenzetu na hatuoni haya kujifunza kwa wenzetu kwa sababu tunaamini kwa kufanya vile tunaendelea kuboresha usimamizi wa rasilimali tulizonazo ambazo Mwenyezi Mungu katujalia. Lakini kwa kufanya hivyo tunaongeza manufaa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa ni mambo ya jumla yaliyojitokeza. Sasa kwa haraka haraka tu labda nipitie sasa michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kadri walivyopata nafasi. Wa kwanza aliyepata kuongea kwa mdogo alikuwa ni Mheshimiwa Charles Mwijage kama nilivyosema, ametushauri mambo mengi, taarifa tumeipokea na tunashukuru sana. Lakini kikubwa katika mambo haya ambayo tumeyasemea ni yale maoni ya Kamati kwenye Azimio Namba 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ambayo imeaminiwa na Bunge hili, baada ya Maazimio haya kupitishwa Bungeni, ilipewa kazi ya kuchambua utekelezaji na mikakati na mipango ya Serikali katika kusimamia hii sekta ndogo ya gesi asili. Kamati ya Nishati ya Madini kupitia taarifa ambayo imewasilishwa

hapa imeridhika, imeipongeza Serikali kwenye Azimio Namba 18, imeipongeza Serikali kwa kuongeza kasi ya kusimamia sekta hii muhimu na nyeti kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, kasoro zitakuwepo, Wizara hizi, taasisi zinaongozwa na wanadamu, haiwezekani kabisa kuwa timilifu. Lakini, katika suala la kusimamia maslahi ya Taifa kama ambavyo tumeleezea kwa kina kwenye Kamati ya Nishati na Madini na kama tunavyoendelea kuwaaminisha Watanzania, hatuta-*compromise*. Tunashukuru kwamba Kamati imeliona, inatuunga mkono, imetutia moyo Serikali na tunawaahidi kwamba pongezi hizi ni changamoto kwetu ili tuendelee kufanya vizuri zaidi kuliko ambavyo ilishajitokeza huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengine mazuri ambayo tumeyapokea, Mheshimiwa Charles Mwijage, ushauri huo ambao umejitokeza kwenye taarifa hii tunaupokea na tunaendelea kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limesemewa sana ni kuhusu ratiba. Ratiba ya utekelezaji wa mambo ambayo tunasema yanafanyiwa kazi, tutaendelea kutoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na kulithibitishia kwa jinsi ambavyo tumejipanga kuhakikisha kwamba haya tuliyosema haya kama sehemu ya utekelezaji ndani ya Maazimio hayo 26, yatatekelezwa kwa kadri ambavyo tumekubaliana na namna mojawapo ni kuhakikisha kwamba sisi tunapokuwa tunakutana na Kamati yetu ya Nishati na Madini kila baada ya kipindi kile kikifika, kila wakati kipindi kinapofika cha Kamati ya Nishati na Madini tutakuwa tunatoa taarifa za utekelezaji wa Maazimio haya kwa sababu hiyo ni namna moja nzuri ya kupima utekelezaji wa yale ambayo tumeyasema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, yapo mambo ambayo yana *specific time frame*. Kwa mfano, tumesema Sheria ya Gesi inakuja kwenye Bunge lijalo. Lakini pia tumesema kwamba kwa kadri itakavyowezekana *Gas Master Plan* lazima ikamilike mwaka huu na tumesema Juni *specifically* kwa sababu iko kwenye taarifa yetu. Sasa lengo letu ni nini? Lengo letu ni kuhakikisha kwamba mambo haya tunayafanyia kazi kama vile ambavyo tumeahidi na kama vile tulivyokubaliana na Kamati ya Nishati na Madini na katika hili hatuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, wa pili kuchangia kwa mdomo alikuwa ni Mheshimiwa January Makamba. Alichangia mambo mengi, lakini kikubwa alisisitiza kwamba kwa yale maeneo ambayo hayana utata na hili limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana, hasa hili suala la mapunjo kwamba hili jambo lifanyiwe kazi, hatua zichukuliwe mara moja na ikibidi *DCI* ashirikishwe.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ushauri tunaupokea. Lakini pia kama nilivyosema, tutaendelea kufanya kazi hizi kwa kuangalia sheria zetu, taratibu ambazo tumefunga na hao jamaa bila kufikia mahala ambapo sisi kama Taifa tunaathirika kwa sababu ya taratibu zilizopo.

Mheshimiwa John Cheyo, amepongeza ripoti kwa pande zote mbili, lakini akasisitiza kupitia mikataba hii. Mikataba hii tunaendelea kuipitia, sisi katika hili hatusimami, yapo mambo na tuna hakika kwamba katika eneo hili, kwa sababu shughuli hii ni endelevu *(sustainable),* huwezi kusema ukipitia mara moja, yamekwisha, hapana! Hata tutakapomaliza kuipitia pamoja na kushirikisha Bunge, kwa kadri ambavyo maendeleo ya sekta hii yanaendelea, teknolojia inavyokuja upya, lazima tutafikia mahali tutasema hata ambayo tumefanya mapitio, tunahitaji tena kuyapitia.

Kwa hiyo, sisi tunachosema, kwanza, zoezi limeshaanza huko Serikalini, lakini bado tunasema, tutaendelea kushirikiana na Bunge lako Tukufu, wakati mwingine kupitia Kamati, lakini pia kama itafikia mahali kushirikisha Bunge lote, tutashirikisha. Lakini kikubwa ni kwamba lazima tuendelee kuipitia mikataba hii ili Serikali iendelee kuimarisha ulindaji wa maslahi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Cheyo alikuwa na wasiwasi kuhusu *Government Negociating Team (GNT)* kwa sababu aliona kama huko nyuma imeishajitokeza. Lakini nasema huu ndiyo mfumo bora wa namna ambavyo Serikali inaweza kutoa maamuzi. Kwa hiyo, ipo namna yake, inawezekana kama mlivyosema, *GNT* inaundwa na wanadamu, yawezekana tuna uzoefu kwamba yapo mambo hayakufanyika au kulikuwa na kasoro fulani, lakini siku zote hiki ni chombo muhimu cha Serikali ambacho

hakiwezi kuwa na dhamira ya kufanya jambo ambalo hatimaye linakuwa halina manufaa kwa Taifa ambalo wao wenyewe wanalitumikia. Sisi tunasema katika hili, tutajitahidi kadri inavyowezekana na kwa sababu tunashirikiana na Kamati, kuhakikisha kwamba *GNT* hii inaleta yale ambayo Watanzania wanataka kuyasikia, inaharakisha maamuzi ya mambo ambayo Watanzania wanataka kuyasikia kwa maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naahidi kwamba jambo hili tutashirikiana vizuri pamoja na taasisi zingine akiwemo *CAG. (Makofi)*

Mheshimiwa John Mnyika, amesema mambo mengi, lakini tunamshukuru kwamba ametambua walau anasema kwa sasa taarifa ilivyokuja kwa maana ya maazimio haya na utekelezaji wa Serikali pamoja na maoni ya Kamati, ni kwamba tunapiga hatua. Tunamshukuru Mheshimiwa John Mnyika ambaye ni Waziri Kivuli katika Wizara hii. Lakini katika yale aliyosema alikuwa na mashaka kuhusu usimamizi huu wa kodi zinazopaswa kulipwa na makampuni yanayofanya shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta Tanzania. Hili wenzetu wanafanya *audit* na katukumbusha kwenye *NGO* moja ambayo ilifanya kazi hii na hesabu zilizoripotiwa kuhusu ukwepaji kodi wa Kampuni ya *Pan Africa Energy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huo tunaupokea, tunashirikiana na wenzetu wa *TRA* kuhakikisha kwamba mambo haya yanashughulikiwa kwa namna ambayo kama hilo jambo ambalo sisi linatutia hasara, basi hasara hiyo irudi kwa hawa wawekezaji, kwa sababu nasema kumkosa mwekezaji mmoja ama wawili, Taifa hili haliwezi kuumia ili mradi utaratibu umefutwa kwa sababu tunaamini wapo wengi wanaotaka kuja kuwekeza Tanzania leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika alihoji, kwa nini majadiliano haya ya mkataba wa *Songas* hayakukamilika tangu mwaka 2008. Muda wote huu tumekuwa tukifanya majadiliano na kama tulivyosema, yapo maeneo ambayo tangu kipindi kile mwaka 2008 tulifanya hitimisho la mojawapo ya maeneo ambayo tulikuwa tunayapitia. Kwa hiyo, kwa muda wote Serikali imeendelea kufanya kazi. Yapo masuala ambayo kimsingi kwa utaratibu uliopo yanachukua muda mrefu kidogo. Lakini niseme tu kwamba yapo mambo ambayo pia ametushauri Mheshimiwa Mnyika, tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Mkosamali, yeye alikuwa na mashaka na alisisitiza; "kuandika ni rahisi, lakini wakati mwingine kutekeleza…." Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mkosamali kwamba sisi kama Serikali, lengo letu haliwezi kuwa kutoinufaisha nchi, haiwezekani, kwa sababu pia tutaadhibiwa kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, maamuzi magumu yatachukuliwa lakini maamuzi magumu haya yasiwe…, maana unaweza kuchukua maamuzi magumu leo, lakini kesho ukawa umeliingiza Taifa kwenye korongo. Kwa hiyo, tunachosema, maamuzi magumu yatachukuliwa lakini baada ya tafakuri ya kutosha kuhakikisha kwamba katika wakati wowote ule Taifa halifikwi na madhara makubwa ya maamuzi hayo ambayo wakati yanafanywa, yalionekana kuwa maamuzi magumu, lakini mbele ya safari yanaligharimu Taifa. Kwa hiyo, tuko makini katika hili kuhakikisha kwamba tunandelea kuwa imara.

Mheshimiwa Selemani Jafo aliipongeza Serikali, lakini na yeye akawa na mashaka na *commitment* ya baadhi ya watendaji wa Serikali. Tunasema, kwa ule upungufu, tunaahidi na kwa kweli ni kwa sababu tu mambo haya hayawezi kuandikwa yote kwenye taarifa moja. Kwenye Kamati tumeelezana mambo mengi ambayo kwa minajili ya utayarishaji wa taarifa kama hii huwezi kuyasema yote, lakini hatua zimeanza kuchukuliwa na tutaendelea kuchukua hatua hizo kwa wale ambao tunaamini kwamba hawafanyi kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Alphaxard Lugola, yapo mambo mengi ameyasisitiza hapa, lakini kikubwa ni kwamba kwenye Azimio Namba 2, yeye ana mashaka sana na ame-*declare*, ametamka hapa kwamba yeye haungi mkono hili suala la uundaji wa *Government Negotiating Team* wakati *Pan Africa Energy (PAT)* wamekiri kwamba wamekwapua. *(Makofi)*

Kaka yangu Mheshimiwa Lugola, hoja yetu na maelezo hapa ni kwamba, hoja ya msingi tunaiona, hasira, uchungu walionao Watanzania kwa kusikia kwamba tumepunjwa fedha kiasi cha dola za Kimarekani milioni 20.1, inauma na haihitaji nguvu nyingi kuelezea kwa sababu kila mwananchi, kila Mtanzania mzalendo anayeipenda nchi hii jambo hilo linauma. Lakini kama nilivyosema, mahusiano yetu

sisi na hao wawekezaji, kwanza ni ya kisheria, sheria za ndani na nje ya nchi ambazo ni sheria za Kimataifa. Lakini, pili ni kupitia mikataba tuliyofunga nao, mikataba hii inatoa wajibu na haki, na haki hizi hata namna ambazo unaweza kushughulikia au kudai haki yako. Lakini pia tuna wajibu ya kuheshimu yaliyomo mle ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachosema sisi, yapo mambo yanaweza kuonekana ni magumu kuyaamua sasa kwa sababu ya utaratibu uliopo, lakini tunasema pia tupo makini kuhakikisha kwamba hatuchukui uamuzi ambao leo unaweza kuwafurahisha Watanzania wote, lakini kesho unaweza kuligharimu Taifa na hatimaye tukaanza kuulizana. Tupo makini katika hili, kufuata utaratibu wa kisheria uliopo na kwa sababu mwisho wa yote, kwa sababu utaratibu huu unakubalika kwa pande zote mbili, makosa ama hitilafu ambayo itajidhihiri baadaye, hakuna atakayeikwepa na sisi tupo tayari kulisimamia hili. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Lugola, uwe na imani, uwe na amani, tuko makini katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio Namba 18, Mheshimiwa Lugola amekuwa na hofu na akasema kwa nini wawekezaji waliruhusiwa kabla ya kutungwa sera mahsusi, sheria na mpango kabambe wa kuhusu gesi asili. Kilichotokea ni kwamba katika hili, kwanza, sera ya nishati ipo, ile sera ya mwaka 2003 ndiyo inatoa maelezo, ufafanuzi, mwongozo, kwa maana ya uwekezaji katika sekta ya nishati. Lakini tulichosema na kama mtakavyofuatilia kwenye taarifa yetu ya utekelezaji kwenye hiki kitabu ambacho tumesambaza na Waheshimiwa Wabunge mnacho, mkisoma taarifa yetu pamoja na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, tumesema sera mahsusi, tumetumia neno mahsusi yaani tunataka tuiondoe katika hii sera ya jumla hii ya mwaka 2003 ambayo imeelezea mambo mengi kuhusu sekta ya nishati. Tunataka tutunge sera mahsusi katika eneo hili na hii imetokana na nini, kama nilivyosema, uwekezaji katika eneo hili kama ilivyo shughuli nyingine ni endelevu. Yapo mambo yanayoibuka leo, maendeleo yanayojitokeza yanalazimisha tufanye mambo mengine mara moja sasa kwa kuzingatia hali halisi ambayo ina-*prevail* katika kipindi hicho. Sera tuliyokuwanayo tunaona kwamba haiwezi kuhimili maendeleo ya gesi yanayotokea sasa hivi. Umesikia habari ya kuwa na kiasi cha rasilimali nyingi ya gesi, sisi tumeshaanza kuwekwa kwenye kundi la wale ambao wana gesi nyingi sana katika Bara la Afrika na hata duniani.

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema hapa, tunatunga sera mahsusi, tunatunga sheria mahsusi, lakini ile sera ya ujumla ipo. Sasa hii imetokana na maendeleo ambayo tumeyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kama mfano wa madini ya *uranium*, wapo Watanzania wengi wamekuwa na hofu, sera ya *uranium* ipo, sheria ya *uranium* ipo wapi! Tulichofanya, madini ya *uranium* ni kama madini mengine tu, sera yake ni ile tuliyotunga mwaka juzi, 2009. Lakini tunasema kwa unyeti wa shughuli za madini ya *uranium*, tumezitungia kanuni zake maalum ili kurahisisha usimamizi wake isiwe katika usimamizi wa jumla, maana yake ni nini, ni kurahisisha usimamizi, lakini pia kuweza ku-*facilitate* wanaoshiriki katika kujenga mazingira ambayo ni ya wazi na ya haraka yanayowezesha kufanywa kwa kushughuli hizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema kwa Mheshimiwa Lugola, ni kwamba asiwe na mashaka kwa nini tunafanya hivyo na hata tunayofanya, tutakayofanya mwaka huu na mwaka kesho, mbele ya safari kutokana na maendeleo yatakayojitokeza, tunaweza tena kuhitajika kurekebisha. Kwa hiyo, hayo ni mambo endelevu na tuendelee tu kushirikiana, tuwe na imani na tuendelee kutoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa wakati Mheshimiwa Lugola alikuwa na mashaka makubwa katika Azimio Namba 18, ukisoma maelezo au maoni ya Kamati ya Nishati na Madini, utaona ambavyo Kamati hii kwa sababu yenyewe imezamia na kuchambua na mengine ambayo tumeyasema kule, hatukuyasema kwa sababu ya utayarishaji wa taarifa, imeridhika sana. Na haikuridhika na taarifa, imekwenda mbele zaidi ikasema inaipongeza Serikali kwa kuongeza kasi ya usimamizi katika sekta hii. Hii ikizingatia na hofu ambayo Mheshimiwa Lugola unayo. Kwa hiyo, katika hili, namuomba asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dokta Festus Bulugu Limbu ameanza na pongezi kwa taarifa zote, ametoa changamoto,  kwanza suala la kudhibiti mgao wa umeme, ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo siyo siku ya kuongelea habari za umeme, pengine tutapata siku yake. Lakini tunavyoongea leo ni ukweli ulio wazi kwamba uwezo wetu wa kuzalisha umeme kwa maana ya *capacity* iliyopo leo unazidi mahitaji yaliyopo leo. Leo mahitaji yaliyopo Tanzania kwa siku ya leo ni *MW 710.* Uwezo tulionao leo ni *MW 1028.70.* Kwa hiyo, kwa mipango tuliyofanya kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu, tumejipanga vizuri, tunaendelea vizuri. Lakini hatujasema kwamba hapo ndiyo mwisho wa safari, hapana tunaendelea. Tuendelee kushirikiana na hii itaendelea kutujengea uwezo zaidi na kutuimarisha katika kukabiliana na kero mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Dokta Festus Bulugu Limbu katika maeneo ambayo yana maslahi kwa Taifa tutaendelea kukandamiza kama kawaida kama ambavyo Taifa linakusudia kusikia. Lakini pia na yeye Mheshimiwa Limbu alielezea kuhusu *Gas Revenue Management Bill* kwamba iandaliwe, ushauri huo tunaupokea na akasema uzalishaji na usimamizi wa gesi tuuimarishe, una manufaa mengi, akataja baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme alikumbusha kutumika katika viwanda vya mbolea na kwa kufanya hivyo itaimarisha hata uimara wa shilingi yetu au fedha yetu ya Kitanzania. Akatukumbusha kwamba *TPDC* iongezewe uwezo, lakini pia sasa *focus* kubwa tujielekeze katika kuisimamia, kuiendeleza rasilimali ya gesi asili. Tunaupokea ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Diana Chilolo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ulitoa pongezi, ninazipokea zote kwa niaba ya wenzangu, lakini ukatutahadharisha kwamba kitengo kitakachoundwa hiki tulichokisema tunakianzisha katika Wizara ya Nishati na Madini, kisimamie masuala ya sera tu na hilo ndiyo kusudio na ndivyo tulivyojipanga kufanya. Umesisitiza kwamba tuongeze matumizi ya gesi, miradi mingi tumeibuni tumesema, lakini kikubwa pia umesisitiza kwamba mapunjo yetu turudishiwe haraka na kama nilivyosema mapunjo haya tutajitahidi kuyasimamia ili mradi tunafuata taratibu zilizopo ambazo tunaamini kwamba zitatufikisha mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kisangi umetoa pongezi, tunazipokea kwa ujumla, Serikali iangalie sekta ya gesi kwa aina yake, na ukaongelea sana kuhusu Azimio Namba 13 kuhusu ajira, tunashukuru sana. Katika hili pia nimshukuru sana Mheshimiwa Charles Mwijage na Kamati kwa ujumla imeliona inasema hata kama Taifa kwa sasa tupo katika mazingira pengine hatuwezi kuruhusu ajira nyingi sana katika sekta zote, lakini Kamati imeshauri na kutahadharisha ni vema tuangalie na tutofautishe sekta kwa sekta. Sekta ambazo pengine zinaweza kuongeza kasi ya maendeleo kwa Taifa letu tuzipe kipaumbele katika kuruhusu kutoa vibali vya ajira. Tunashukuru tunaamini kwamba Serikali kwa ujumla tutaendelea kushirikiana kwa hili, tumepata wafanyakazi 51 kwa mwaka huu wa fedha, tumeruhusiwa tuajiri, mchakato utaanza lakini tunakusudia mpaka kufikia mwaka 2014 tuwe tumeajiri karibu wafanyakazi 200 kwa sababu namba iliyopo ni 192 lakini inaweza kuwa inazidi hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Mariam Kisangi umeongelea habari ya Azimio la Namba 15 kuhusu visima na Azimio Namba 26 kuhusu mradi wa gesi. Mheshimiwa Murtaza Mangungu umesema mengi lakini kubwa ulisisitiza kwamba dola milioni 20.1 zilipwe mara moja, maelezo yake yanafanana kama nilivyosema, lakini ukatahadharisha kuhusu Azimio Namba 9 uanzishwaji wa gesi, sheria ya gesi lakini pia ukakumbusha hivi sisi ambao tunatoka katika maeneo ambako gesi inapatikana na ukatoa mfano wa wale wanaotoka katika maeneo ya dhahabu kumekuwa na kitu kinaitwa mrabaha lakini pia ukaja na *concept* hii ya *service levy*, tunafanyaje sisi watu ambao tupo katika maeneo ambako gesi hii inatoka.

Hili ni jambo ambalo linahitaji maamuzi ya msingi ya Kiserikali pengine na ya kisera, lakini nasema kwamba sisi hili tunalichukua na hili siyo mara ya kwanza leo kusemwa, hili limekuwa likisemwa na sisi tutakaa, tutalifanyia kazi ili kuona namna ambavyo tunaweza kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na hasa katika eneo hili la *service levy* unafanyaje, ni lazima tuliangalie kwa sababu kwa mfano kwenye minara ya simu, unaweza ukaona mnara ambapo unapakana na Wilaya tatu sasa mgawanyo wake katika *service levy* unafanyaje, wenzetu tunaamini watalaam wa Wizara ya Fedha watatusaidia na pengine kujifunza kutoka nchi zingine tunafanyaje katika eneo hilo ili hatimaye yale maeneo au Halmashauri ambazo rasilimali zinapatikana zinufaike zaidi. Ukasisitiza pia mradi wa gesi Dar es Salaam ukaomba na Kilwa, Spika alikumbusha kuwa hiyo haimo katika taarifa yetu lakini ni hoja ya msingi kwamba kwa kadri tunavyoendelea miradi hii ya usambazaji gesi, utumiaji wa gesi na kwa sababu kuna bomba ambalo limetoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ambao ujenzi wake utafanyika mwaka huu ni lazima tuwafikishie wananchi wengi hauwezi kuwa Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Kabwe Zitto umepongeza pande zote mbili, tunashukuru lakini umesema mambo makubwa kuhusu Azimio Namba Moja pia Azimio Namba Tisa, uimarishaji wa usimamizi katika sekta hii na hasa eneo la *upstream* na kikubwa ulichokuwa unasisitiza ni kwamba *TPDC* iachiwe huru, ifanye kazi zake na ukasisitiza kwamba ipate *retention* na ndiyo jambo ambalo tumelisema, lakini kwenye Azimio Namba Tisa ukasema kwamba Watanzania wanataka kusikia habari za *Gas Master Plan, Gas Revenue Managemen*t na mambo ambayo yanahusisha usimamizi lakini yakiwa yanatokana na misingi ambayo imejengwa, *policy* na *legal frame work* masuala ya kisera pamoja na kisheria, ni ushauri mzuri na sisi tunauzingatia. Azimio Namba Sita ulikuwa unatukumbusha kwamba *CAG* ni *External Auditor* kwa *TPDC* sasa inakuwaje katika mazingira ambayo ameshirikishwa katika ukaguzi wa kwanza, ushauri tunaupokea na katika mazingira kwa sababu Serikali kimikataba iliyopo inaruhusiwa kufanya *auditing* zaidi ya inayofanywa na *TPDC* ndiyo maana umekuwa msingi wa kumruhusu *CAG* afanye hiyo kazi, lakini mbele ya safari kadri uwezo utakapokuwa umeimarika nadhani tutafikia mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amesisitiza kuhusu masuala ya sera, tunakubali, kama nilivyosema sera kwa ujumla kwa sasa ipo lakini tunahitaji sera mahsusi, tunahitaji sheria mahsusi kuhusu eneo hili la sekta ndogo hii ya gesi. Lakini pia ukasisitiza kuhusu mafunzo *(capacity building)* lakini ukahoji pia mapunjo kwenye riba kuhusu mapunjo ambayo tunayasema, yote haya yatajitokeza baada ya shughuli kufanywa na *CAG* lakini pia *Government Negotiating Team* tutajua hatua ambazo zitafuata baada ya hapo. Ukasisitiza mikataba kupitiwa upya hii ni hoja ambayo tunakubaliana nayo na hatimaye ukasisitiza mradi wa gesi Dar es Salaam na sisi tunaamini kwamba pengine mradi huo usiwe wa Dar es Salaam tu, huo utakamilika lakini tunaendelea kubuni miradi mingine katika maeneo mengine ya nchi. Kwa ujumla ushauri wako tunaupokea na tunaendelea kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rosemary Kirigini amesisitiza suala la ratiba ya utekelezaji wa haya tunayoyasema, yapo ambayo ni *specific* tumeyasema kwa mfano utungaji wa sheria unakuja katika Mkutano ujao, *Gas Master Plan* tumesema mwezi wa sita na hatimaye utekelezaji uanze, kampuni ya usambazaji gesi tumesema imeshaundwa lakini kazi kwa sababu inategemea kasma baada ya bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, pia ulijielekeza katika Azimio Namba 18, unaona kama kuna watendaji wanakwaza, tunasema kwa wale ambao wanakwaza kwa sababu za uzembe hatua zitaendelea kuchukuliwa lakini ni katika eneo hili ambalo tumelisema, kwenye Kamati Azimio Namba 18 baada ya kutoa maelezo ya kina kwa yale mengine ambayo tumeshindwa kuandika kwa sababu ya nafasi, tunaamini kwamba Kamati imeelewa vizuri na tunaendelea kulishirikisha Bunge lako Tukufu ili liendelee kujua hatua ambazo Serikali inazichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliyepata nafasi ya mwisho kuchangia kwa kuongea alikuwa ni Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Naibu Waziri amesema mambo mengi kimsingi lakini kikubwa ni kati ya hatua ambazo Serikali imechukua kuendelea kuisimamia, kuimarisha usimamizi, lakini pia kulinda maslahi ya Taifa katika sekta hii ya nishati hasa katika eneo la sekta ndogo ya gesi asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mwisho kabisa taarifa hii imechangiwa na wachangiaji 52, waliochangia kwa kuongea walikuwa ni Wabunge 15 na waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi walikuwa Wabunge 37 jumla yake ni wachangiaji 52, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya mwisho kwa Bunge lako Tukufu, ushauri, maoni na tahadhari ambazo mmetupa Serikali tutaendelea kuzifanyia kazi, na yote haya kwa sababu hatimaye lazima yatekelezwe kama nilivyosema ratiba yake kwa yale ambayo yapo *specific* tutaendelea kama tulivyosema kwenye *commitment* yetu kupitia taarifa yetu lakini kwa yale ambayo mengine ni *progressive* tutaendelea kutoa taarifa kupitia Kamati za Bunge na kwa kadri ambavyo inabidi tutakuja kushirikiana pamoja kupitia taarifa ambazo tutaendelea kuziwasilisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo tena nawashukuru wote kwa sababu kufikia taarifa hii tulipoifikisha hapa haijachangiwa na Wabunge peke yao, wapo Watanzania wengi baada ya taarifa hii kutolewa kupitia vyombo vya habari, tunavishukuru vyombo vya habari vimeandika sana habari hizi, Watanzania wengi walivutika, wapo waliochangia kwa kututumbelea ofisini, wakaja kutupa ushauri wa maandishi, wengine wamefanya mikutano na sisi *official* na hata ambayo haikuwa *official* lakini walitaka

kushiriki kwa namna moja au nyingine kuboresha usimamizi wa sekta hii ndogo ya gesi asili. Nataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia Watanzania kuwa yote ambayo mmekuwa mkitushauri tumeyazingatia kwa kadri tunavyoweza na tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo tutaendelea kuimarisha usimamizi wa sekta hii ndogo ya gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru tena kwa mara nyingine kwa kutupa fursa hii na baada ya kusema haya naomba kuwasilisha lakini pia kutoa hoja kwamba taarifa hii tumeipokea na tunaifanyia kazi na utekelezaji utaendelea, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Toa hoja, mbona hukuomba kutoa hoja sasa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono nayo hoja inasema anaomba Bunge lipokee taarifa ya kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu uendeshaji wa sekta ndogo ya gesi nchini. Sasa nitawahoji wanaokubali kwamba taarifa ya sasa ipokelewe.

*(Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini Yalipokelewa na Bunge)*

**SPIKA:** Nadhani wote tumesema taarifa hii imepokelewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huu ndiyo mwisho wa safari yetu ya Kamati Ndogo ya Nishati na Madini, mimi naomba niwapongeze kwanza kabisa ninyi Wabunge, nilikuwa na wasiwasi sana namna ambavyo mtachangia nikajua tena tunaanza kufumua upya kama vile haijawahi kuwasilishwa katika Bunge lililopita, lakini mmejadili kwa umakini, kwa uhodari kwa *style* ya peke yake, mimi naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii pia imewezekana kwa sababu Kamati yetu nayo ilivyoandika taarifa yake kutokana na taarifa ya Serikali wameiandika vizuri sana kiasi kwamba ilikuwa rahisi kwenu kujadili kwa sababu wao wenyewe wameandika vizuri sana. Naomba niipongeze Kamati na Wajumbe wake wote. Lakini pia niwapongeze Serikali nao kwa kuleta maelezo ambayo yameweza kufanyiwa kazi na Kamati na sisi kupata kitu kimoja ambacho ni kizuri sana naomba niwapongeze watu wote mlioshughulikia hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ningependa pia kutoa angalizo kwa Wabunge wote na Kamati zetu, historia ya Kamati za Sekta zamani tulikuwa na Kamati tu, lakini baadaye tukawa na Kamati za Sekta, sababu ya kuwa na Kamati ya Sekta ni kwamba wakati wote Kamati hizi zinakuwa na Wizara zinazohusiana nazo kufanya kazi wakati wote, kwa hiyo, ukiona maoni ya Kamati wanasema wanasema Bungeni wasirudishe Bungeni wataendelea kufanya kazi na Kamati hizo wakati wote. Mkiangalia Kanuni yetu inayohusiana na mambo haya, hii ni Nyongeza Namba 8 Kanuni Namba 9 inayosema majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sekta yoyote ile yatakuwa, kushughulikia bajeti ya Wizara inayosimamia moja ya kazi yake.

Pili kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara zinazohusika; tatu, kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji za Wizara hizo; nne kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ambayo yenyewe inasema; "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza, kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yapo katika wajibu wake, kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti, kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu, wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo, (d) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo na sheria, (e) kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa." Hizo ni Kamati za Sekta. *(Makofi)*

Lakini Kamati hizi zingine za *watchdog committees* na zenyewe maana yake wakati mwingine huwa tunatumia muda mwingi sana kufanya vitu halafu tunakuwa tunafanya jumla zenyewe zote tatu zinatakiwa kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali, za Wizara au Halmashauri au Mashirika. Pamoja na kwamba tunafanya ile kazi lakini mnajua maeneo ambayo yanaonekana yana utata ndiyo hayo mnaweka nguvu zaidi kuliko kuzunguka halafu mnakuta mnapita kama mambo ya kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, ninasema haya kwa sababu nchi sasa hivi ipo katika mpito *(transition period),* katika kipindi hiki ni lazima ku-*manage* na watakaoshiriki ku-*manage* hii *transition* ni Wabunge kutumia Kamati zenu. Kwa hiyo, utakuta kama Kamati ya Nishati isiangalie sekta ndogo ya gesi tu, iangalie Wizara nzima na mambo yake makubwa yale, halafu Kamati inakaa inasema kwamba sisi safari hii tuna-*focus* huku, kwa hiyo, mnakuta mnaifahamu Wizara yote na mambo ambayo mnafikiria hapa ni maslahi makubwa ya nchi. Gesi kweli lakini kuna maeneo mengine, kwa hiyo, Kamati iingie katika mtindo huu wakati wote na mpo wengi mnaweza kujigawa katika sehemu na mkaingia kwa undani katika maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Sasa sisemi Kamati ya Nishati na Madini na Kamati zingine pia, tuache ule mzaha mzaha na ili kufanya haya tunahitaji Wabunge kuwa na *integrity*, ni lazima Wabunge wenyewe muwe na *integrity* ya kuisimamia Serikali hiyo ni lazima. Halafu kwa ujumla wetu wote na Serikali yenyewe iwe na *integrity* ya kuweza kusimamia maslahi ya nchi, tukifanya hivi na kwa mujibu wa Kanuni zetu tutakuta baada ya muda mfupi vitu ambavyo mlifikiria vimejikunja vitakuwa vimenyooka na mtaviona waziwazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nashauri kwamba katika Kamati hii utakuta mahali pengi wanasema wataleta taarifa hapa Bungeni, siyo hivyo fanyeni huko huko maana mkiwa mnaleta kila siku tutakuwa tunafanya kazi ya kusikiliza Kamati moja tu ya sekta ndogo ya gesi! Siyo lengo letu, fanyeni huko huko mnapoona hapa mnataka kutushirikisha sisi taarifa zenu zile ndiyo zinakuja na *highlights* kwamba hapa sisi Wizara yetu ilifanyia kazi lakini udhaifu wake moja, mbili, tatu, tunaomba Bunge tuwashirikishe hapo ndiyo itakuwa vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri kwa dhati tutakuwa na semina kwa Wenyeviti kuhusiana na mambo haya lakini baadaye tutakuwa na semina nyingine ili kusudi tufanye mambo kisayansi zaidi na tuweze kuwadhibiti wenzetu kisayansi zaidi. Sasa mnakuta hapa hatuendi kwa watu, tunakwenda kwenye taasisi yenyewe inayohusika Wizara na sera zake na sheria zake na kama tunaona sheria zingine zimekaa haziwezi kusimamiwa tunatunga sheria ya namna ya kuisimamia Wizara, mengine tutazungumza wenyewe kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja tu kwamba Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kwamba kutakuwa na kikao baada ya kuahirisha Bunge hili katika Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sina matangazo mengine naomba niwashukuru sana kwa kushiriki leo siku nzima, kesho tutakuwa na kipindi cha maswali na majibu lakini baadaye tutakuwa na semina ya Benki Kuu kuhusu hali ya uchumi nchini, tulikuwa tumedai kwa muda mrefu hatukuwa tumeipata lakini kesho baada ya kipindi cha maswali na majibu tutakuwa na kazi hiyo siku nzima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 8 Februari, 2012 saa tatu asubuhi)*